Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Tatu - Tarehe 3 Februari, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):**

Taarifa ya Utendaji na Hesabu za Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kwa mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2004 *(The Annual Report and Accounts of the Presidential Parastatal Sector Reform Commission for the Financial Year ended 30th June, 2004).*

**SPIKA:** *Agenda* inayofuata, lakini kuhusu utaratibu Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Kanuni namba 32 ipo kidogo tu. Kanuni ya kwanza.

**SPIKA:** Ngoja tuione, endelea Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, nimeshaiona Kanuni ya 32.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kutoa hoja kwamba Hati zilizowasilishwa Mezani na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji zijadiliwe na Bunge.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa kwa mujibu wa Kanuni hii haihitaji kutolewa taarifa na itaamuliwa bila mabadiliko wala mjadala wowote. Labda nitawahoji muiamuie hiyo hoja ya Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, tumeielewa wote.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi ya kutaka hati iliyowasilishwa mezani kujadiliwa na Bunge ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, hoja itajadiliwa kulingana na mpangilio wa *Order Paper* utakavyokuwa. *(Kicheko)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 22

### Uwasilishaji wa Taarifa Mezani

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa Mkutano wa Bajeti, Waziri na Mwenyekiti wa Kamati wa Wizara husika huwasilisha mezani taarifa zao kuhusiana na hoja husika kabla ya kusomwa rasmi baadaye:-

(a) Je, kwa nini Kambi ya Upinzani haipewi haki yao ya kuwasilisha mezani taarifa yake juu ya hoja hiyo hiyo ambayo msemaji husika wa kambi hiyo ataisemea baadaye?

(b) Kwa nini wasemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara husika hawapati nafasi hiyo ya kuwasilisha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu alioutaja Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, umetamkwa katika Kanuni Namba 81(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004. Kanuni hiyo imewataja Waziri Mhusika, pamoja na Mwenyekiti wa Kamati inayohusika, kwamba ndio watawajibika kuwasilisha mezani taarifa zao. Wasemaji wa Kambi ya Upinzani hawakutakiwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kanuni hiyo kutokuwapatia Wasemaji wa Upinzani jukumu hilo la kuwasilisha taarifa zao mezani, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge

amelileta rasmi suala hilo hapa Bungeni, naamini kwamba utakubali ombi la Mheshimiwa Mbunge lianze kutekelezwa sasa kwa kutumia Kanuni ile ya 31(1) (b), ambayo inaruhusu hati ziwasilishwe mezani na Mbunge yeyote asiyekuwa Waziri.

Na. 23

**Mchango ya Akiba ya Wafanyakazi**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika zoezi la ubinafsishaji Serikali Kuu imelazimika kulipa mafao ya watumishi pamoja na michango ya akiba ya uzeeni *(PPF, NPF, NSSF)* kutokana na mashirika yake kushindwa kulipa madai ya wastaafishwa; na kwa kuwa Halmashauri nyingi zina hali mbaya ya mapato na hivyo kushindwa kuwasilisha michango ya akiba ya wafanyakazi na kulipa mafao yao kwa wakati:-

(a) Je, Serikali itachukua hatua gani ili madeni ya aina hiyo yasilimbikizwe na baadaye kuwa mzigo mkubwa kwa Serikali?

(b) Je, ni Halmashauri zipi zilizolimbikiza madeni ya aina hiyo na kwa kiasi gani hadi kufikia mwezi Oktoba, 2004?

(c) Je, ni Halmashauri ngapi na zipi zimeandaa mafungu ya kuwalipa Waheshimiwa Madiwani mafao yao kwa wakati mara baada ya muda wa uongozi wao kwisha mwaka 2005?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa *(LAPF)* unapokea michango kutoka kwa Halmashauri za Miji na Wilaya na kwa waajiri wengine wanaoamua kujiunga na mpango huu. Kwa muda mrefu wachangiaji hawa wamekuwa wakichelewa kuwasilisha michango ya wafanyakazi wao hivyo kusababisha kuwepo kwa malimbikizo ya madeni makubwa ya michango. Baada ya Serikali kutambua kwamba baadhi Mashirika ya Umma na Taasisi zake hazikuwa zinawasilisha makato ya michango ya wafanyakazi wao kwa mamlaka zinazohusika, hatua zifuatazo zilichukuliwa:-

(i) Iliandikwa Waraka (kumbukumbu Na. *TYC/T/200/583/15* wa tarehe 20 Julai 2004) kutoa mwongozo wa kuboresha usimamizi na uwajibikaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali.

Katika waraka huo, watendaji wakuu wote wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali walikumbushwa kuzingatia taratibu na Sheria ambazo zinawataka kuwasilisha makato ya michango ya wafanyakazi wao kwa mamlaka husika ikiwa ni pamoja na mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya *PPF, PSPF, NSSF, TRA* kwa ajili ya *PAYE* na *LAPF*.

(ii) Serikali ilitoa waraka mwingine tarehe 22 Septemba, 2004 kuwakumbusha tena watendaji wakuu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wajibu wao ambao ni pamoja na:-

- Kuhakikisha kuwa waajiri wanawasilisha michango ya wanachama bila kukosa;

- Kutumia vipengele vya sheria kuwashughulikia waajiri ambao hawawasilishi michango;

- Kuwasilisha HAZINA kila mwezi taarifa za makusanyo na orodha ya majina ya Mashirika na Taasisi zote ambazo haziwasilisha michango ya wafanyakazi wao katika mifuko hiyo kwa wakati.

(iii) Kwa upande wa TAMISEMI ilichukua hatua ya kuhakikisha kwamba Watendaji Wakuu wa Halmashauri hizo ambazo zina malimbikizo ya makato ya Wafanyakazi wanaingia mkataba kwa niaba ya Halmashauri na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wa kulipa malimbikizo hayo katika kipindi maalum. Hatua hii ilipoonekana haitoshelezi kwa Halmashauri ambazo zimekuwa na malimbikizo ya michango hiyo Serikali ilichukua hatua ya kukata ruzuku za Halmashauri hizo kuanzia Novemba, 2002 moja kwa moja kutoka HAZINA.

(iv) Mheshimiwa Spika, kuanzia Septemba, 2002 Serikali ilichukua hatua ya kuzikata Halmashauri michango ya akiba ya wafanyakazi wao moja kwa moja toka kwenye ruzuku inayotolewa na kuwasirisha fedha hizo kwenye mfuko na hili limesaidia sana kukomesha kabisa malimbikizo tangu mwaka 2000.

(v) Kuimarisha shughuli za kuitawala na kiongozi ambapo ufuatiliaji na ukaguzi wa mahesabu ya Mfuko hufanyika mara kwa mara. Nayo hatua hii imesaida sana kuoondoa malimbikizo.

(b)Mhesimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa madeni uliofanyika hadi mwezi Oktoba, 2004 Mfuko ulikuwa unazidai Halmashauri na Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa jumla ya shilingi bilioni 16.8. Kati ya fedha hizi deni halisi ni shilingi bilioni 6.6 na riba ni bilioni 10.2. Kufuatia hatua niliyoieleza hapo juu jumla ya shilingi bilioni 1.67 zilikusanywa na Mfuko na hivyo kufanya deni lipungue hadi kufiki shilingi bilioni 15.1. Jumla ya Halmashauri 102 zinadaiwa kiasi hiki cha fedha hadi Oktoba, 2004.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa waraka namba *PMC/1/A100/98* wa mwaka 1997. Halmashauri zote ziliangizwa kutenga fedha kutokana na mapato yake kila mwaka kwa ajili ya kulipia mafao ya Waheshimiwa Madiwani wanapomaliza muda wao. Kiasi kinachotakiwa kutengwa ni asilimia 30 ya posho ya kila mwezi kwa muda wa miaka mitano. Makadirio ya malipo haya yanatakiwa yawepo katika Bajeti ya kila

Halmashauri kila mwaka. Hivyo Halmashauri zote zinahimizwa kutekeleza maagizo yaliyotolewa na tunaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika Halmashauri hizo kuhakikisha kwamba fedha hizo zimetengwa.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa. Lakini naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza tatizo kubwa ni kwa wafanyakazi wa Halmashauri walikwishaachishwa kazi au waliacha kazi au kustaafishwa ambao mafao yao hayo ya akiba za uzeeni pamoja na baadhi ya mishahara haijalipwa hadi sasa. Serikali inasema nini kuhusu hilo.

Pili ni kuhusu fedha zinazotengwa kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani watakapostaafu pamoja na kuwepo kwa waraka huo kutokana na ukata mkubwa wa baadhi ya Halmashauri. Baadhi ya Halmashauri nyingi hazijaweza kutenga fedha hizo hii ina maana kwamba madiwani watakapostaafu watakuwa bado hawajapata fedha zao. Je, Serikali itawasaidia vipi Halmashauri hizo ili kuwaondolea adha madiwani wakati wakimaliza muda wao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nijielekeze kwa swali lake la kwanza kwa wale waliostaafishwa. Kwa uelewa wangu ni ndani ya Halmashauri na sio nje ya Halmashauri. Tatizo hilo lilikuwepo hata mara ya mwisho tulipokuwa tunamemaliza kipindi kilichopita na tulihakikisha kwamba wale wote walikuwa wanastahili walilipwa. Kwa hiyo, tutakachofanya katika zoezi hili na tayari ofisi yetu imeshaanza kulishughulikia ni kuhakikisha kwamba fedha hizi ambazo zinatakiwa ziwe zimelipwa kwa wale wote waliokuwa wamestaafishwa zinalipwa kwa utaratibu ambao tutakuwa tumekubaliana nao. Tunatambua kwamba ni tatizo kubwa katika maeneo mengine lakini juhudi hizi zinaendelea kufanywa. Kuhusu suala la Halmashauri zetu kuto kutenga fedha kutokana na ukata.

Mheshimiwa Spika, tunaloweza kusema tu ni kwamba ukiona Halmashauri inatumia kisingizio hicho ujue tu kwamba Halmashauri hiyo haiko *serious.* Jambo hili na ni dhahiri kabisa Halmashauri ambayo imedhamiria kufanya jambo, haiwezi kushindwa kutenga kiasi hicho kwa kila mwaka. Kama ofisi sisi tutahakikisha kabisa fedha hizo muda utakapofika lazima zilipwe kwa madiwani hata kama itakuwa ni lazima kukata moja kwa moja kutoka kwenye ruzuku katika kipindi kitakacho husika.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la msingi kwa maelezo ya Naibu Waziri ni kuwa fedha zilikuwa haziwasilishwi kule kwenye mifuko na kwa kuwa kazi ya kuwasilisha kwenye mifuko ni ya utendaji na kwa kuwa sasa wameambiwa sasa watakatwa ruzuku kutoka *source* yani kule kule hazina. Ni kwa nini Serikali inakuwa tayari kuadhibu Wilaya

nzima kwa makosa ya kuitendaji ya wale ambao hawakuwasilisha fedha hizo kwa wakati wanaotakiwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kutokuwasilishwa kwa fedha hizi na baadhi ya Halmashauri ni mambo yanayofanywa katika Halmashauri zenyewe. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba Halmashauri inaporidhia jambo kama hili kama itaonekana baadaye kwamba imesababisha matatizo atakayewajibika ni Halmashauri yote kwa sababu ni Serikali na ilifanya jambo hili ama kwa kujua ama kwa kukubaliana. Ndio maana na Serikali inasisitiza tu kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba Halmashauri zinawasimamia vizuri hawa wakurugenzi wao na kuhakikisha kwamba maamuzi kama haya hayafanyiki kama hakuna ridhaa ya Halmashauri.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa kutowasilisha michango hii kumeipaka Serikali matope kutoka kwa wastaafu wanapokwenda kutafuta mafao yao wasiyakute na kwa kuwa Serikali imelazimika kutafuta fedha za ziada na kuchelewesha mipango mingine ambayo ingekuwa imepangwa.

Je, Serikali kwa ujumla wake imefanya nini kuwawajibisha watendaji ambao hawawakilishi hii michango? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, narudia kusisitiza kwamba nitajibu nikijielekeza katika Halmashauri zetu na si kwa Serikali kwa ujumla. Kwa sababu kama ni Serikali kwa ujumla basi itabidi pengine Waziri fedha asaidie jambo hili. Kuhusu wafanyakazi ndani ya Serikali za Mitaa ambao ama wamestaafishwa au wameacha kazi kwa mazingira fulani fulani ambayo bado yanawapa haki ya kulipwa fedha hizi naomba kurudia tena tumekuwa tunafanya kila linalowezekana kwanza kuhakikisha kwamba wanalipwa tunazibana Halmashauri wale wahusika wanapeleka fedha hizo *LAPF* na hatimaye mtumishi huyo analipwa.

Lakini kama nilivyosema jambo hili haliwezi kufanyika katika Halmashauri kama Halmashauri nzima haina ridhaa na jambo hili. Kwa hiyo, kama ni kuwawajibisha, naomba sana Halmashauri zenyewe zihakikishe zinawawajibisha wakurugenzi hawa ili kuacha kabisa tabia hii ambayo si nzuri kwa watumishi wetu. *(Makofi)*

Na. 24

**Posho kwa Vikosi vya Ulinzi**

**MHE. KIJAKAZI KHAMIS ALI (k.n.y. MHE. ALI MACHANO MUSSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina malengo mazuri tu ya kutoa posho kwa vikosi vyetu vya ulinzi ili kupunguza makali ya maisha yanayowakabili askari wetu; na kwa kuwa posho hiyo inatofautiana baina ya majeshi yetu wanalipwa kwa tofauti kubwa zaidi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa posho inayolingana kwa majeshi yote nchini?

(b) Kama hilo linawezekana, je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kurekebisha posho hiyo ili isitofautiane sana?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mbunge wa Tumbatu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria Na. 24 ya mwaka 1966 iliyounda Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Sheria Na. 8 ya mwaka 1990 iliyounda Jeshi la Polisi na Vikosi vyake, vyombo hivi vinatofautiana kimajukumu, kimahitaji na hata katika taratibu za kazi zao.

Malipo ya posho yanayotofautiana kati ya askari na watumishi katika vyombo hivyo yanatokana na tofauti zilizopo katika majukumu na mahitaji ya kila chombo. Tofauti katika majukumu na taratibu za kazi katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama zinasababisha kuwepo kwa tofauti katika mahitaji yao pia. Bajeti za vyombo hivyo hutayarishwa na kila chombo kwa kuzingatia mahitaji yao kwa mujibu wa taratibu za kazi zao na kupitishwa na Bunge lako Tukufu kupitia Bajeti za Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Serikali inaendelea na mpango wake wa kuboresha mishahara kwa Watumishi wake wote ikiwa ni pamoja na askari wetu ili kupunguza makali ya maisha.

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Spika, asante sana kunipa nafasi ya swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa askari wengi wanadai malimbikizo ya posho zao tofauti kama maposho ya safari posho za likizo, *disturbance* mbali mbali, uhamisho. Je, Serikali ina mpango gani wakuzilipa malimbikizo ya posho zao za nyuma hao askari? Asante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa watumishi wengine ni kweli kwamba kuna maaskari na watumishi walio kwenye Jeshi la Ulinzi na Polisi ambao hawajalipwa malimbikizo ya mafao yao ya posho. Utaratibu umewekwa na Serikali kuhakikisha kwamba malimbikizo haya au madeni hayo kwa askari wetu na watumishi walio katika majeshi yote mawili yanalipwa pale ambapo Serikali inakuwa na uwezo na inajitahidi kuona kwamba uwezo huo unapatikana ili watumishi hao wapewe haki yao.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza. Wakati askari polisi na wanajeshi wanapodai malimbikizo yao mbalimbali, mara nyingi wanafuatilia madai hayo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali haifanyi mpango ya kuwapelekea mafao katika vituo vyao vya kazi badala ya kufuatilia mafao hayo Dar es Salaam?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli watumishi wanasumbuka mara nyingi kufuata madeni yao au malimbikizo ya posho zao hadi Dar es Salaam.

Naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwakumbusha maafisa utumishi wote ambao wako kwenye majeshi haya na katika idara na Wizara za Serikali kufanya kazi zao ipasavyo ili wale wengine wafanye kazi zao na wao wafanye kazi ya kufuata malimbikizo hayo kwa sababu ni sehemu ya kazi zao.

Na. 25

**Uchimbaji wa Malambo ya Maji**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

Je ni nini mpango wa Serikali wa kusaidia uchimbaji wa Malambo na Mabwawa ya maji hasa kwa maeneo yanayokabiliwa na ukame mkubwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul N'gwala Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Katika kuwapatia huduma ya maji wananchi walioko sehemu kame, njia mojawapo ni kuwashirikisha wananchi wenyewe katika ujenzi wa malambo na mabwawa kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Wizara yangu imeandaa mkakati wa ujenzi na ukarabati wa mabwawa ambao unahusisha kikamilifu asasi mbalimbali, Sekta Binafsi na wananchi, chini ya mkakati huu Halmashauri za Wilaya na Miji kwa kushirikiana na wananchi huainisha maeneo yanayohitja malambo au mabwawa. Ili kuufanya mpango huu kuwa shirikishi wananchi huchangia asilimia 20, Halmashauri asilimia 30 na Serikali Kuu asilimia 50 katika kugharamia uchimbaji wa malambo. Utaratibu huu umeonyesha mafanikio hasa kwenye maeneo ya wafugaji na utaendelea kutumika. Hatua nyingine ambayo Serikali imechukuwa ni kuunda Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa mwaka 1998, kwa lengo la kuimarisha ujenzi wa malambo na mabwawa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2001/2002, Wizara yangu imetoa kiasi cha shilingi 957,000,000/= kwa ajili ya uchimbaji na ukarabati wa malambo 299

kwa ajili ya mifugo katika wilaya 58 zilizo kame. Hadi sasa malambo 220 yamekamilika na malambo 79 yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji kutegemea kasi ya uchangiaji wa Halmashauri za Wilaya na wananchi. Aidha, kuanzia mwaka 2003/2004, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula (Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya) imetoa fedha zingine shilingi 404,000,000/= kwa ajili ya uchimbaji na ukarabati wa malambo 34 katika Wilaya 15 ambazo ni kame, ambapo malambo 29 yamekamilika na malambo 5 yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumuarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi, inatekeleza programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini mkoani Shinyanga. Programu hii inagharamia ujenzi wa malambo na mabwawa katika maeneo ambayo wananchi wameonyesha mahitaji ya mabwawa na wako tayari kushiriki. Aidha, programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini itakayotekelezwa katika Wilaya zote nchini kuanzia mwezi Julai itatoa kipaumbele katika ujenzi wa malambo na mabwawa katika maeneo kame.

**MHE. PAUL. N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru samahani sauti yangu si nzuri na naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Wilaya ya Kishapu ni moja ya maeneo yanayokabiliwa na ukame, ningependa Mheshimiwa Naibu Waziri anifahamishe ni nini mpango wa Serikali kusaidia uchimbaji wa malambo na mabwawa katika Wilaya hii inayokabiliwa na ukame?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nimeleza kwamba kuna programu ambayo inaendelea ambayo inafadhiliwa na Serikali ya Uholazi. Programu hii ni kubwa ambayo ina kiasi ya fedha karibu bilioni tisa na ni kwa ajili ya Mkoa wa Shinyanga. Sasa kinachotakiwa ambacho ningeomba kwa niaba ya Wizara ni kuwahamasisha tena wananchi wa mkoa wa Shinyanga ikiwemo Wilaya ya Kishapu kwamba wajitokeze na kuchangia kama masharti ya msaada huo ilivyo. Lakini hata hivyo kama hawatautumia vizuri huu msaada ina maana kwamba hata hii programu ya fedha tunazozipata kutoka *World Bank* chini ya Mradi wa Maji Vijijini nao hawatautumia vizuri. Kwa hiyo, kitu cha msingi ni kusisitiza wananchi pamoja na uongozi mzima wa Wilaya Kishapu wajitokeze ili wachangie na kutimiza masharti yaliyotolewa na hifadhi hii.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Halmashauri nyingi zimeshindwa kusimamia uchimbaji wa malambo kutoka kwa fedha zinazotolewa na Wizara hiyo na kwa kuwa Madiwani wa Halmashauri hizo kwa mfano wilaya ya Kahama na Geita Madiwani waliochukua hatua watendaji waliofanya ubatilifu wa fedha hizo, lakini Wizara ya TAMISEMI inawalinda, je, Serikali iko tayari kutangaza sasa ni ruksa kufanya ubadhirifu fedha hizo? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna baadhi ya ubadhirifu umefanyika lakini sidhani kana kwamba tatizo kama hilo la ubadhirifu linatakiwa lichukuliwe na Serikali au Wizara anayoisema.

Mimi nadhani kwa kutumia Halmashauri ni vizuri mambo hayo yakaripotiwa kwa vyombo vinavyohusika ikiwemo polisi na kadhalika. Kwa sababau huo ni wizi au *mis-appropriation* ya fedha ambazo zimetolewa kwa ajili ya mradi wa kusaidia wananchi, lakini zinatumika vibaya na zimetumika vibaya bila ridha ya baraza la wilaya au baraza la Halmashauri ya wilaya. Kwa hiyo, huo ni wizi na ningeomba waripoti kwenye vyombo vinavyohusika. Kumwamisha mtu haitasaidia kwa sababu atakwenda kufanya hayo hayo sehemu nyingine.

Na. 26

**Tatizo la Maji**

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA** aliuliza:-

Kwa kuwa vijiji vya Mumagunga, Nakatuba na Soroti vina tatizo sugu la upatikanaji wa maji.

Je, ni lini tatizo hili litatatuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sera ya maji ya mwaka 2002 inasisitiza ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga, kusanifu, kujenga na kuendesha miradi ya maji vijijini kwa lengo la kuwa na miradi ya maji endelevu.

Wizara yangu kwa sasa inasimamia utekelezaji wa Mradi wa Maji Vijijini unaotekelezwa kwa mkopo nafuu wa fedha kutoka Benki ya Dunia. Katika mradi huo, wananchi wanahimizwa kuanzisha miradi yao na tayari taarifa tulizonazo maeneo mengi wananchi wameunda mifuko masharti yote ambayo yanahitajika chini ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Mumagunga, Nakatuba na Soroti vyenye tatizo sugu la upatikanaji wa maji vinahimizwa kuanzisha miradi ya maji katika sehemu yao kwa kuwasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, ambayo itatoa kipaumbele kwa miradi inayopendekezwa kujengwa kulingana na masharti ya Mradi huu wa Maji Vijijini.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nipewe nafasi kwa ajili ya swali la nyongeza.

**SPIKA:** Umeshapewa.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, tatizo la maji katika Jimbo langu upande wa vijiji hivi vya Mumagunga, Nakatuba na Soroti ni tatizo sugu na ni la muda mrefu na mpaka sasa hivi nimejitahidi, inavyoonekana ni kwamba ni vigumu kuchangia Wananchi kwa sababu mradi huu ni mkubwa. Kwa vile hivi sasa nafanya utaratibu wa kupata msaada kwa ajili ya kuweka matanki na pampu za kutumia *solar.*

Mheshimiwa Spika, je, Wizara itakuwa tayari pia kuchangia katika mradi huu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli maeneo aliyoyasema kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi yana matatizo ya maji. Lakini pia ni vizuri tukumbuke kwamba huko nyuma kwenye miaka ya 1960 na kurudi nyuma, malambo ambayo sasa hivi tunayachangia yalikuwa yanachimbwa kwa mkono na hii imedhihirisha kwenye maeneo mengi sana fedha tulipopeleka Halmashauari haikuchangia, lakini wananchi wametumia hizo fedha kama kulipwa posho kidogo na wamechimba malambo mazuri sana.

Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, huhitaji msaada wa kuchimba lambo katika *design* tunazozitoa utoke nje na utumie *solar* nadhani haitakuwa *cost effective,* lakini kama mradi huo utauleta, tutajaribu kuona Serikali itachingia kwa kiasi gani. Lakini ningeomba sana mambo haya tuyafanye wenyewe kwa kuwashirikisha wananchi vizuri, wakielewa watafanya.

Na. 27

**Mita za Kupokelea Mafuta Bandarini**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA** Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekamilisha kazi ya kufunga mita ya kupokelea mafuta bandarini *(flow meter)* pale *KOJ,* na kwa kuwa hatua hiyo ni muhimu katika kukabiliana na tatizo la ukwepaji kodi kwenye sekta hiyo muhimu katika uchumi wa nchi yetu.

(a) Je, ni manufaa gani yameanza kupatikana kiuchumi baada ya mita hiyo kufungwa ikiwa ni pamoja na ongezeko la kodi inayokusanywa na Serikali?

(b) Je, ni mipango gani iliyopo ya kuwezesha Mamlaka ya Mapato *(TRA)* kuhakiki uingizaji wa mafuta toka nje kwa kushiriana na Usalama wa Taifa ili kuhakikisha kwamba hakuna ufisadi wowote unaotumika kuikosesha Serikali mapato ya kutosha kutoka katika Sekta hiyo?

(c) Je, utaratibu uliowekwa na Serikali wa kutofautisha mafuta yanayosafirishwa na yale yanayouzwa katika soko la ndani unaofanywa na Kampuni ya *SGS* umesaidia kiasi gani kuongeza mapato ya Serikali na je, kwamba kampuni hiyo *(SGS)* imelipwa gharama ya kiasi gani ilipopewa Mkataba huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mradi wa kufunga mita za kupima mafuta *(flow meters)* Bandarini Dar es Salaam pale *KOJ,* ni kati ya hatua zilizochukuliwa na Serikali mwaka 2003/2004. Hadi sasa jumla ya mita 14 kati ya mita16 zilizotarajiwa zimefungwa na tisa kati ya hizo zimekwishaanza kufanya kazi tangu Novemba, 2004.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa muda wa miezi michache tu tangu baadhi ya mita zianze kutumika yaani tangu Julai, 2004 baada ya Serikali kutangaza nia ya kufunga mita kumetokea ongezeko la mapato ya shilingi milioni 16,507.3 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2004 ukilinganisha na Julai hadi Desemba 2003.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania imejiwekea utaratibu thabiti wa kuhakiki uingizaji wa mafuta toka nje. Utaratibu huo unajumuisha yafuatayo:-

- Kupata taarifa za awali za ujio wa vyombo vya kusafirishia mafuta.

- Kupima mafuta yote kwenye vyombo vya usafirishaji kabla ya kushusha mafuta.

- Kukadiria na kutoza kodi kwenye vituo vya kuingizia.

- Kudhibiti mafuta yote yaendayo nje ya nchi.

- Kufuatilia na kudhibiti matumizi kya mafuta yenye misamaha ya kodi kabla ya kurejesha kodi.

Aidha, Serikali inashirikisha taasisi nyingine kama Taasisi ya Kuzuia Rushwa na Usalama wa Taifa kwa mujibu wa Sheria na taratibu wanazosimamia hasa kuhakikisha usalama wa mafuta na mita zenyewe na katika kufuatilia mwenendo mzima wa biashara ya mafuta nchini.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka ya 2001 - 2004, kutokana na programu ya kutofautisha mafuta yanayosafirishwa nje na yale yanayouzwa katika soko la ndani na hatua nyingine za udhibiti, mapato yaliongezeka kila mwaka ambapo mwaka 2000/2001 yalikuwa shilingi bilioni 184,843 na mwaka 2003/2004 yalifikia shilingi bilioni 275,891.

Mheshimiwa Spika, malipo ya ada *(marking fees)* kwa huduma iliyotolewa na *SGS* yalitegemea mikataba iliyosainiwa baina ya *TRA* na *SGS* kila mwaka. Katika miaka ya 2001-2004, Serikali ilíilipa kampuni ya *SGS* gharama za uwekaji dawa jumla ya shilingi bilioni 4,711 *(USD 4.56m)* kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2001 | - | Tshs.127.6m | *(USD 137,851.01)* |
| 2002 | - | Tshs. 126.74m | *(USD 130,621.52)* |
| 2003 | - | Tshs.2.545bln | *(USD 2.416m)* |
| 2004 | - | Tshs. 1.911bln | *(USD 1.877m)* |

Mheshimiwa Spika, kwa vile tangu mwaka 2000-2004 Serikali ilichukua hatua nyingine nyingi za kudhibiti ukwepaji wa kodi kwenye Sekta ya mafuta. Hatua hizo ni pamoja na kuweka mita zinazopima mafuta yanayoingia nchini *(flow meters),* ulipaji kodi awali, ufutaji wa mabohari ya mafuta yanayo dhibitiwa na Forodha *(Bonded Oil Warehouses),* kuanzisha kitengo cha usimamizi na udhibiti wa mizigo inayokwenda nje ya nchi *(transit monitoring control),* kulipa kodi halafu kurejeshewa mafuta ya misamaha na kubadilishana taarifa na nchi za jirani. Hata hivyo Serikali baada ya kutathmini matokeo ya hatua hizo haikuendeleza tena Mkataba baina ya *TRA* na *SGS.* Hivyo kuanzia tarehe 1 Januari, 2005 hakuna tena Mkataba mpya wa uwekaji dawa kwenye mafuta kati ya Serikali na *SGS.*

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya niongeza. Lakini awali ya yote kwa ridhaa yako naomba niipongeze Serikali kwa hatua ambazo imechukua kufanyia kazi ushauri wa Wabunge baada ya kupiga kelele sana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Naibu Waziri inaonyesha kuna ongezeko la shilingi bilioni 16 katika kipindi cha Julai hadi Desemba baada ya ufungaji wa mita, na hii maana yake inadhihirisha kwamba kabla ya kufunga hizi *flow meter* kulikuwepo na tatizo la ukwepaji kodi wa kiasi hicho na zaidi.

(a) Je, Serikali itafanya uchunguzi ili kuweza kubaini watu waliohusika na ukwepaji wa kodi katika vipindi vya nyuma?

(b) Kwa kuwa sasa tumeweza kukamilisha zoezi la ufungaji mita katika pale *Kurasini Oil Jet (KOJ),* Serikali ina mpango gani kufunga *flow meter* katika maeneo mengine ambayo yanapokea mafuta toka nje ya nchi ili kuweza pia kueondokana na tatizo la ukwepaji kodi za Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, Serikali inapogundua kuna mtu amekwepa kodi, sio tu kwenye mafuta lakini mahali popote, basi hatua za kisheria zinachukuliwa na anatakiwa kulipa hizo kodi alizokwepa. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na itafanya uchunguzi kwa wale waliokwepa kodi na inapogundulika na itakapogundulika kwamba wamekwepa kodi basi hatua za kisheria zinachukuliwa.

Pili mpango huu wa *flow meter* ndio tumeuanza na matokeo yake kama alivyosema Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, yameanza kuonekana. Tunaanza na Dar es Salaam kwa kuweka *flow meter,* lakini maeneo mengine ya nchi kavu ni vigumu kuweka *flow meter.* Lakini hatua nilizozitaja kwenye jibu langu la msingi zinachukuliwa na zimeonyesha matunda tayari kwa ongezeko kubwa la mapato yanayotokana na kodi inayolipwa kwenye mafuta. Kwa hiyo, hatua zitaendelea kuchukuliwa na kuboresha pia utendaji wa *meter* zilizofungwa katika Bandari ya Dar es Salaam pale *KOJ.*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baada ya kufunga *flow meter* tayari imebainika kwamba kuna tofauti ya makusanyo ya mapato pale ambapo *flow meter* hazijafungwa na kwa hiyo wamebainika watu ambao walikuwa wakikwepa kodi.

Kwa nini Serikali inashindwa kuwataja hasa hao waliokwepa kodi wakati huo ili wadhibitiwe?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, utaratibu uliokuwa unatumika ulikuwa na mapungufu ambayo yalisababisha Serikali kuamua kufunga *meter.* Kwa hiyo, sio kwamba tulikuwa tunawajua waliokuwa wanakwepa kodi, lakini utaratibu ulikuwa una matatizo ya ukwepaji wa kodi na tatizo hili sio kwamba linakwisha 100% tunalipunguza kadri inavyowezekana. Kwa sababu kadri Serikali inavyoweka utaratibu pia wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu wanabuni mbinu nyingine za kukwepa kodi. Kwa hiyo, Serikali itaendelea nao na itaendelea kubana taratibu ili makusanyo ya Serikali yaweze kuongezeka.

Na. 28

**Malipo ya Watumishi Waliostaafishwa**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa wapo watumishi waliostaafishwa ambao walikuwa katika mpango wa *operation service* na kwa kuwa Serikali sasa inawarudishia wastaafu ambao walikuwa chini ya Mkataba wa pensheni ya malipo ya uzeeni.

Je, Serikali haioni kuwa hata wale waliostaafishwa yaani *(operation service)* wanastahili malipo ya kudumu kama wastaafu wengine?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, watumishi waliostaafishwa ambao walikuwa katika mpango wa *operation service* hawamo kwenye Sheria ya Utumishi wa Kudumu na Malipo ya

Uzeeni (Pensheni). Watumishi wa *Operation Service* wamo kwenye mfumo wa Utumishi wa kuchangia *NSSF* na Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini *(GEPF)*. Chini ya utaratibu huo mtumishi anachangia na mwajiri anamchangia. Mara mtumishi anapostaafu au kumaliza mkataba wa kazi hulipwa michango yake yote ikiwa ni pamoja na ya mwajiri na riba itokanayo na kuwekeza michango hiyo kwa muda wote aliokuwepo kazini.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo ni tofauti na wa pensheni ambapo mtumishi hulipwa sehemu tu ya fedha (kiinua mgongo) na kisha hulipwa malipo ya kila mwezi hadi anapofariki.

Mheshimiwa Spika, kuwaingiza katika mpango wa pensheni wastaafu ambao waliajiriwa katika masharti ya kawaida *(operational service)* itakuwa vigumu kwani walikwishalipwa kiasi chote walichochangia ikiwa ni pamoja na michango ya mwajiri na riba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mifuko hiyo *NSSF* na *GEPF* ina taratibu zake, Serikali itaishauri mifuko hiyo ili wastaafu walio katika masharti hayo nao waweze kupata nafuu ya maisha kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Mifuko hiyo zitakavyoruhusu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, napenda kumwuliza maswali kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa mpango huu wa *operation service* si mpango endelevu wa mtumishi unaostaafu, wengi wao hudhoofu na kufa upesi. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuifanyia marekebisho sheria hii ili watumishi wote wawe katika mtindo wa aina moja?

(b) Kwa kuwa wapo watumishi waliokuwa kwenye mpango wa *operation service* ambao walistaafishwa yaani waliachishwa kabla ya muda wao, je, Serikali kwa nini haikuwapa mafao ya kutosha ili waweze kulipia muda wa utumishi uliobakia katika mkataba wao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi nilisema kwamba hawa watumishi waliostaafishwa walikuwa katika mpango maalum wa *operational service* na hawa watumishi walikuwa kwenye mfumo wa Utumishi wa kuchangia. Hata Mashirika mengine ya umma walikuwa kwenye utaratibu huu kwamba unachangia na mwajiri anachangia na unaposimamishwa basi michango yako uliyochangia na ile aliyochangia mwajiri pamoja na riba unalipwa malipo yako moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nilivyosema katika jibu langu ni kwamba Serikali itaishauri mifuko hii ili watumishi walio katika masharti hayo waweze kupata nafuu ya maisha kwa kuzingatia Sheria na kanuni.

Kwa hiyo, hili tutaendelea kuliangalia kama kuna mahali pa kuboresha, Serikali itaboresha kwa kushirikiana na mifuko hii.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kwamba waliachishwa kabla ya muda wao itakuwaje?

Mheshimiwa Spika, watumishi hawa walikuwa katika utumishi chini ya masharti maalum na masharti hayo yalikuwa chini ya taratibu za kisheria. Kwa hiyo, tunaamini kwamba walioachishwa, waliachishwa na taratibu zote zilifuatwa na masharti ya ajira yao yalifuatwa na kama kuna matatizo basi yanaweza yakaletwa yakashughulikiwa kisheria.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nilikuwa na swali dogo la nyongeza.

Katika utaratibu wa kuwalipa wale waliochukua mafao yao kwa mkupuo, kuna wengine ambao wao waliamua kuvumilia. Sasa wanauliza, kwa kuwa wale walikwisha maliza mgao wao lakini Serikali ikawakumbuka kuwarudisha katika huu utaratibu. Je, wale waliovumilia kuna uwezekano na wao wa kuwafikiria angalau kuwaongeza kwa sababu kiasi wanachopata ni kidogo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiongeza kiwango cha malipo ya pensheni kadri uchumi wetu ulivyokuwa unaboreka. Kwa hiyo, hao ambao walivumilia kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge wamefikiriwa katika nyongeza kama ambavyo wengine wote wamelipwa.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kutamka kwamba Serikali inakamilisha taratibu zote za kuwalipa wale waliorejeshwa kwenye malipo ya pensheni ya kudumu na pale ambapo matatizo yanajitokeza basi naomba wastaafu wavumilie na Wizara inatoa matangazo kwenye magazeti ya leo na kesho wayasome na wazingatie yale yatakayokuwa yametangazwa kwenye tangazo hilo la Serikali.

Na. 29

**Umiliki wa Silaha za Moto**

**MHE. SALOME J. MBATIA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwananchi yeyote anaweza kumiliki silaha ya moto baada ya kukamilisha taratibu zote zinazohitajika:-

(a) Je, ni wakati gani mume au mke asiyemiliki silaha ya moto anaweza kutumia silaha ya moto anaweza kutumia silaha inayomilikiwa na mwenzake iwapo silaha inamilikiwa na mmoja wao tu?

(b) Je, ni silaha gani za moto zinatengenezwa humu humu nchini?

(c) Kama hatujaweza kutengeneza silaha hizo, je, ni utaratibu gani unatumika ili kuagiza silaha hizo nchini kwa biashara na kwa mtu binafsi kutoka nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome Mbatia, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya silaha na risasi *(The Arms and Ammunition Act* ya mwaka 1991), kifungu Na. 32(1) hairuhusiwi mtu yeyote kutumia silaha inayomilikiwa na mtu mwingine. Kwa hiyo, mume au mke haruhusiwi kisheria wakati wowote kutumia silaha ambayo inamilikiwa na mmoja wao.

(b) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Tanzania haina kiwanda cha kutengeneza silaha za moto. Hata hivyo wapo watengenezaji wa silaha za kienyeji yaani magobore ambao wanadhibitiwa na kuratibiwa na Halmashauri za Wilaya. Vile vile kuna kiwanda cha kutengeneza risasi kule Morogoro kinachomilikiwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

(c) Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika kuagiza silaha kwa wafanyabiashara na watu binafsi ni kama ifuatavyo:-

(i) Mfanyabiashara au mtu binafsi anapotaka kuagiza silaha za moto (bunduki na risasi) toka nchi za nje, lazima apate leseni ya kuingiza silaha nchini *(firearms impute licenses)* maombi ya leseni hiyo ya kuagiza silaha yanatakiwa yatumwe kwa Mkurugenzai wa Makosa ya Jinai *(DCI)* kupitia kwa *RPC* wa Mkoa husika. Idhini hii ya kuagiza silaha hutolewa na Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai *(DCI)* kwa mujibu wa kifungu Na. 9(1) cha Sheria ya silaha na risasi ya mwaka 1991.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la kumuuliza. Kwa muda mrefu sisi wananchi wa Zanzibar (Unguja na Pemba) tulikuwa salama sana dhidi ya vitendo mbalimbali vya kijambazi, lakini kwa kuwa sasa vitendo hivyo vinaonekana kushamiri katika Visiwa vyetu.

Je, Serikali inafikiria vipi ili kuwaruhusu watu wenye uwezo na kwa kufuata sheria waweze kumiliki silaha ili kujilinda na ujambazi huu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa mujibu wa sheria ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kule bado watu binafsi hawaruhusiwi kumiliki silaha zaidi ya vile vyombo vya dola. Sasa kama wananchi kule Visiwani wanaona iko haja kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kurekebisha sheria, basi inafaa suala hili walipeleke katika Baraza la Wawakilishi ili lifikishwe rasmi kwenye Serikali litazamwe kwa mujibu wa mazingira ya sasa.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa mujibu wa sheria hiyo iliyoitaja na Naibu Waziri ya kumiliki silaha nchini, je, mwanamke au mwanaume anayetumia silaha ya mwenzake kupambana na jambazi linalomshambulia ndani ya nyumba atahukumiwa kwa sheria gani ili kujilinda?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika hali ya mazingira aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge kwamba baba au mama ambaye hamiliki silaha, lakini yuko katika hali ya hatari ya kuvamiwa na jambazi maisha yake yako hatarini. Sasa katika mazingira hayo sheria inaruhusu utumie silaha yoyote kujihami. Maana katika mazingira hayo unapojihami katika namna hiyo kuokoa maisha yako na ya mtu mwingine na hata kama ukimuua yule jambazi alikuwa anahatarisha maisha vile vile bado sheria itaangalia mazingira yale na itakulinda. *(Makofi)*

Na 30

**Wananchi Kuchukua Sheria Mkononi**

**MHE. EDSON M. HALINGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali mara kwa mara imekuwa ikisisitiza kwamba wananchi wasichukue hatua/sheria mkononi za kuwaadhibu majambazi wanapowahujumu mali zao na wakati huo huo majambazi wanachukua hatua mkononi mwao kuua na kuwadhulumu wenye mali:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kwa msingi huo unawafanya majambazi wajione kuwa wana haki ya kuendekeza hujuma zao?

(b) Je, kwa nini Serikali isiweke kipengele cha sheria kwamba majambazi wanaotumia silaha wakibainika wanyongwe mpaka kufa?

(c) Je, kwa nini Serikali isiandae sheria ya kuwabana majambazi kulipa fidia ya madhara na mauaji yanayotokana na vitendo vyao kwa familia husika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edson Halinga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria, kila mtu anayo haki ya usalama wa maisha yake na mali zake, hivyo majambazi wanaoiba au kunyang’anya mali za watu wengine, wanakiuka sheria za nchi na hivyo wanastahili adhabu kali. Adhabu hizo hutolewa kwa mujibu wa sheria Na. 4 ya mwaka 2004 *(Miscellaneous Amendments).*

Kwa upande mwingine sheria pia inawakataza wananchi kuchukua sheria mkononi mwao kwa kuwahukumu na kuwaadhibu wahalifu. Sheria inaelekeza kwamba wawapeleke wahalifu hao kwenye vyombo vya sheria ili wahukumiwe kisheria. Huu ndio

utawala wa sheria, ambao ni msingi wa kudumisha amani katika jamii. Hivyo vitendo vya wananchi kuchukua sheria mkononi mwao ni ukiukaji wa utawala wa sheria na kiashiria cha fujo na uvunjaji wa amani na kwa vyovyote vile uzingatiaji wa utawala wa sheria hauna lengo la kutetea wahalifu, bali ni mbinu sahihi ya kupambana na wahalifu katika jamii.

(b) Mheshimiwa Spika, adhabu ya sasa kwa jambazi wa kutumia silaha, kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ya mwaka 2004, ni kifungo si chini ya miaka 30 na viboko au bila viboko kutegemea na uamuzi wa Mahakama. Kwa sasa Serikali inaona adhabu hiyo ni kubwa na inatosha. Kwa sasa Serikali inaona adhabu hiyo ni kubwa na inatosha. Hata hivyo, iwapo wananchi wanaona ipo haja ya kuongeza kiwango cha adhabu ili iwe ya kunyongwa hadi kufa, wanayo haki ya kuleta maoni yao Serikalini kupitia kwa wawakilishi wao (Wabunge) na Serikali itayatafakari maoni hayo na kuyafikisha Bungeni ambacho ndicho chombo pekee chenye madaraka ya kutunga sheria kwa mujibu wa Katiba.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Na.9 ya mwaka 1985 kifungu 348 kinawabana wahalifu ikiwa ni pamoja na majambazi kulipa fidia kwa madhara waliyosababisha kwa mtu au watu au mali kutokana na vitendo vyao vya uhalifu. Kwa mujibu wa sheria hiyo, baada ya mhalifu au jambazi kutiwa hatiani, Mahakamani inaweza kuamuru mshtakiwa huyo kulipa fidia kwa mtu aliyedhurika na kitendo cha uhalifu. Fidia hiyo iwapo itaamriwa, hulipwa pamoja na kutekeleza adhabu iliyotolewa na Mahakama.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya niongeza.

(a) Je, katika kuwafunga hawa wahalifu ambao wanakuwa wamethibitika wameua kwa muda mrefu na hata Serikali inakubali hao ni majambazi sugu haioni kwamba inawalinda hawa wahalifu na kutokuwajali wale wananchi wasio na kosa kuuwawa bila sababu?

(b) Kwa nini polisi wanawaachia na kuwawekea dhamana wahalifu ambao wamethibitika na vithibitisho kwamba ni wahalifu, ni wezi hawaoni kwamba hii inawakatisha tamaa wananchi na upoteza imani yao kwa polisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza wahalifu wanaouwa aliowataja Mheshimiwa Mbunge au adhabu ya kuuwa sio kufungwa. Adhabu ya kosa la mauaji kwa sheria zetu za sasa ni adhabu ya kifo kwa hiyo, hawa hatuwafungi, hawa wanahukumiwa adhabu ya kifo wale waliouwa. Hawa ambao hawakuuwa ila wamefanya ujambazi hawa wanafungwa ili kuwapa muda na nafasi ya kujirekebisha na wakijirekebisha wakimaliza kifungo chao wanarudi katika jamii tukiamini kwamba watakuwa raia wema.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu dhamana. Kwanza dhamana nyingi sana zinatolewa Mahakamani na chache zinatolewa Polisi. Dhamana inatolewa kwa makosa

yale ambayo sheria imeainisha kwamba yana dhamana, kuna makosa mengine hayana dhamana. Kwa makosa ambayo yana dhamana ile dhamana ni haki ya kila raia. Kwa hiyo, ningependa wananchi wa Tanzania waelewe kwamba kwa makosa yale ambayo hayamo kwenye kundi la kunyimwa dhamana kama vile uuaji, kubaka, dawa za kulevya ni machache, yaliyo mengi ni haki ya mwananchi kupata dhamana. Kwa hiyo, wasivunjike moyo wanapoona mtu kapata dhamana kwa kosa ambalo kisheria ana dhamana, waone kwamba ndio utaratibu wa nchi na ndio utawala wa sheria.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma nchi hii ilikuwa na sheria ya kuwaondoa majambazi na hasa wale sugu katika maeneo ambayo wanatendea makosa na kuwapeleka katika maeneo mengine ili kupunguza ghasia ya kuungana wakawa wengi na kufanya *chains* za makosa katika maeneo hayo, hii ilisaidia sana. Je, sheria hiyo kama ilifutwa itarudishwa ili kupunguza matatizo ambayo yanawaletea adha sana wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli huko nyuma utaratibu huo ulikuwepo wa majambazi, walevi wa gongo na kadhalika kutolewe sehemu moja ya Tanzania kupelekwa sehemu nyingine. Lakini jinsi muda ulivyokwenda sasa hivi hata ninyi wenyewe mtakubali kwamba utaratibu huo hautumiki na haufai. Hivi ni nani katika Jimbo lake ambaye yuko tayari tumletee majambazi wote, walevi wote, watasema Jimbo la Mheshimiwa fulani ndiko wanapopelekwa wabakaji na walevi, wapi? Ni utaratibu ambao kwa kweli haufai kwa hiyo hawa wahalifu sasa mahali pao ni Magerezani na sio katika sehemu yoyote ya Jamhuri. *(Kicheko)*

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa pamoja na jitihada kubwa sana za kuelimisha wananchi juu ya ubaya wa kujichukulia sheria mikononi lakini bado wananchi wanajichukulia sheria mikononi, je, Serikali itakubaliana nami kwamba hiyo inaonyesha wananchi wamekatishwa tamaa na utendaji wa vyombo vyetu vya haki hususani Mahakama na Polisi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mara kwa mara Serikali tumekuwa tunatoa wito kwa wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mikononi kwa sababu utaratibu huo ukiachiwa uendelee unaweza kuleta madhara makubwa sana katika jamii. Kwa hiyo, kwa dhati kabisa tunasema tutumie vyombo vilivyowekwa kuliko kila mtu akiwa na mwizi wake kumalizana naye huko huko, itaingiza fujo, vurumai na itavuruga kabisa utaratibu wa utawala wa sheria.

Kuhusu kuwa wananchi bado wanaendelea na hicho ni kiashiria kwamba wamekata tamaa, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza matukio hayo yapo lakini si mengi kiasi cha kuonyesha kwamba Tanzania utaratibu ni kila mtu

kuchukua sheria mkononi, hata kidogo. Ni matukio machache na bado tunaendelea kuwaelimisha wananchi na ninyi Waheshimiwa Wabunge mtusaidie tuwaelimishe ili tukomeshe tabia hiyo.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya dola, Mahakama au Polisi vinapokuwa vina matatizo, maana vyombo vya dola vinaendeshwa na binadamu, tunaomba wananchi watuarifu huyo ambaye anadhorotesha utaratibu huko aliko kama ni Polisi au Mahakama ili tumchukulie hatua kuliko kuacha wananchi wananung'unika na badala yake wanafanya vitendo ambavyo vinahatarisha amani ya nchi.

Na. 31

**Tatizo la Usafiri na Nyumba za Askari wa Kituo cha Polisi Unguja Ukuu**

**MHE. JINA KHATIB HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Askari wanaofanya kazi katika Kituo cha Polisi Unguja Ukuu wanapata usumbufu wa kwenda na kurudi mjini kwa sababu kituo hakina makazi ya Polisi na Serikali haijafikiria kuwakodishia nyumba Askari hao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapunguzia mwendo Askari hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Askari katika kituo cha Polisi Unguja Ukuu wanaishi mjini mbali na kituo chao cha kazi kutokana na ukosefu wa nyumba. Hali hii inaathiri ufanisi wa kazi za Askari. Hata hivyo, katika jitihada za kupunguza athari hii, Serikali mwaka huu wa fedha 2004/2005 ina mpango wa kuendeleza ujenzi wa nyumba ya kuweza kuishi familia mbili za Askari kituoni hapo. Aidha, kwa sasa kituo hicho kina gari moja aina ya *Land Rover 110* ambayo inatumika kila siku kuwapeleka Askari kazini na kuwarudisha Askari majumbani mwao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuchukua nafasi hii kwanza, kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia maslahi ya Askari na pili namwomba Mheshimiwa Mbunge awahamasishe wananchi wa eneo la Unguja Ukuu wajitolee kujenga nyumba za kuishi Askari katika kituo hicho ili Askari hao waweze kuishi kambini ili waongeze ufanisi wa ulinzi katika eneo lao.

**MHE. JINA KHATIB HAJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina swali dogo la nyongeza. Kuna uhakika kwamba Askari wanapelekwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba kituo cha Unguja Ukuu

tumekipelekea gari *Land Rover 110* na Mheshimiwa Haroub Said Masoud, pale mwenye Jimbo anaelewa jambo hilo. Moja ya kazi ya gari hilo ni kitendea kazi cha kuwasaidia Askari kwenda katika doria na kuwarudisha nyumbani na kuwaleta kazini. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge unazo taarifa kwamba gari hilo sasa linafanya kazi za mtu binafsi halifanyi hizi tulizokusudia tunaomba taarifa ili turekebishe dosari hiyo mara moja.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, nimefurahi kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa mimi na yeye ni Waarabu wa Pemba tunajuana kwa vilemba, je, Mheshimiwa Waziri miongoni mwa pesa alizozitenga yuko tayari kuzimalizia nyumba za Tunguu ambazo wanaishi Askari?

**SPIKA:** Aaaah, ni swali jipya lakini unaweza kulijibu kama unayo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kujenga nyumba za Askari pale Unguja Ukuu zinatosha kwa mradi huo. Zile nyumba za kule Tunguu nazo zimetengewa fedha zake na mwaka huu wa fedha tutaanza kukarabati nyumba za Tunguuu.

Na. 32

**Mawasiliano ya Simu Jijini Mwanza**

**MHE. STEPHEN M. KAZI** aliuliza:-

Kwa kuwa Jiji la Mwanza linazidi kukua kwa kasi na wakazi wake wanahitaji mawasiliano ya simu ambayo ni muhimu pia: -

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza mpango wake wa kuondoa mitambo ya simu ya kizamani aina ya *analogue* katika Jiji la Mwanza na badala yake kuweka mitambo ya *digital* ambayo ni ya kisasa na ina uwezo mkubwa?

(b) Je, mtambo wa simu wa Mwanza una njia ngapi zinazotumika kwa wakazi wa Jiji hilo kwa mahitaji yao ya simu na huduma nyingine kama vile *internet* na kadhalika?

(c) Je, njia hizo zinatosheleza kwa kiasi gani wakazi wa Jiji la Mwanza?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* tayari imekwishatekeleza mpango wake wa kuondoa mtambo wa simu za kizamani aina ya *analogue (crossbar switch C400)* wenye uwezo wa laini 2,600 na kuweka mtambo wa kisasa aina ya *digital* katika Jiji la Mwanza wenye uwezo wa laini 3,000.

Kwa hiyo, huduma imeboreshwa kwa upatikanaji wa mtambo wa kisasa. Kutokana na kuboreshwa kwa huduma hizo, Jiji la Mwanza limeweza kuwa na huduma ya *internet* ambayo hutolewa na watoa huduma hizo, yaani *internet service providers* ambao wana makao yao Jiji Dar es Salaam, kuna *Internet café* sita. Aidha, Jiji la Mwanza lina vituo vya redio vitatu, vituo vya televisheni viwili na vituo vya televisheni vya kulipia *(cable TV)* viwili.

Mheshimiwa Spika, mtambo wa simu katika Jiji la Mwanza una uwezo wa kuhudumia wateja 8,702. Hivi sasa kuna wateja 4,544 tu. Mtambo huo unatosheleza kwa kiasi kikubwa mahitaji ya mawasiliano ya wakazi wa Jiji la Mwanza kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2001, Mheshimiwa Stephen Kazi, amefuatilia kwa karibu sana suala la kuboresha mawasiliano katika Jiji la Mwanza, tunamshukuru.

**SPIKA:** Eeeh, Mheshimiwa Stephen Kazi, nyongeza ya shukrani!

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, napokea shukrani za Waziri. Lakini pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba mabadiliko ya simu Mwanza yanaonekana na hata simu yangu ya nyumbani namba zake zimebadilika, hiyo nampa shukrani kubwa. Swali ni kwamba sasa tunakwenda na wakati na hali ya ushindani kibiashara na simu za mikononi, mitambo kama ya *Mobitel, Celtel* inazidi kutumika Mwanza.

Katika kuwahamasisha wananchi wa Mwanza watumie simu hizi za mezani, utaratibu wa gharama unaoletelezwa na *rental tax* ambayo inatozwa na kampuni yenyewe hauonekani kwamba ni kizuizi cha kampuni hii kufanya biashara zake vizuri na kuwafanya wananchi wa Mwanza waitumie vizuri simu hii kwa wakati huu walionao sasa hivi?

**SPIKA:** Gharama Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunakwenda na wakati na kuna ushindani mkubwa sana kati ya kampuni zenye simu za mkononi na kampuni za simu za mezani. Kutokana na ushindani huo mkubwa, ni matarajio yetu kwamba utazifanya bei za siku za mkononi na vile vile gharama za simu za mezani zipungue. Ni ushindani tu utakaofanya hilo liwezekane.

Na. 33

**Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA)**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA (k.n.y. MHE. KHADIJA SALEH NGOZI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) ni miongoni mwa Mashirika ya Umma lililokuwa likifanya kazi zake vizuri Jijini Dar es Salaam kwa kutoa huduma ya usafiri ulio bora na wa uhakika bila usumbufu na kwa wakati uliopangwa; na kwa kuwa, usafiri huo uliwasaidia sana wakazi wa Jiji hilo hasa wanafunzi na wanawake kutonyanyaswa kwa namna moja au nyingine:-

(a) Je, Shirika hilo linaendelea kutoa huduma zake katika Jiji la Dar es Salaam?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kulisimamia ili lifanye kazi kwa ufanisi zaidi kwa lengo la kuwaondolea wananchi usumbufu wanaoupata hivi sasa wa kupanda daladala za watu binafsi ikiwa ni pamoja na upandishwaji wa nauli kiholela?

(c) Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kubinafsisha Shirika hilo kama ilivyofanya kwa Mashirika mengine?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Usafiri Dar es Salaam linamilikiwa kwa pamoja kati ya Serikali yenye hisa asilimia 49 na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam yenye hisa asilimia 51.

Shirika liliwekwa chini ya Kamati ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* Agosti, 1997. Lengo lilikuwa ni kuuza asilimia 75 ya hisa kwa watu binafsi na kiasi kilichobakia asilimia 25 kuendelea kumilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, *PSRC* iliteua wataalamu waelekezi kampuni kutoka Uingereza iitwayo *Steer Davies Gleave* ili kutoa mapendekezo ya jinsi ya kulibinafsisha Shirika. Mapendekezo ya wataalamu yalipokelewa na *PSRC* na yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika kipindi hiki Shirika limeendelea na shughuli zake na limechukua hatua zifuatazo kuboresha Utendaji wake.

(i) Kupunguza gharama za uendeshaji;

(ii) Kuimarisha mapato yake ili kuongeza mtaji wa Shirika; na

(iii) Kusafisha mizania ya hesabu za Shirika kwa kulipa malimbikizo ya madeni ya miaka ya nyuma.

Hatua hizi zimeongeza ufanisi kwa kiasi fulani. Hata hivyo, Shirika halijaweza kufikia lengo lake la kutengeneza faida ya kutosha kutokana na hali ya ushindani katika usafirishaji wa abiria Jijini Dar es Salaam.

Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Shirika bado linaendelea kutoa huduma zake katika Jiji la Dar es Salaam kama inavyofanywa na watoa huduma wengine binafsi (daladala).

(b) Serikali imejitoa katika shughuli za biashara ya usafirishaji abiria Jijini. Hata hivyo, Halmashauri ya Jiji ina mpango wa kuboresha usafiri wa abiria Jijini kupitia Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka *(BRT).* Mradi huu uko katika hatua za awali za utekelezaji. Chini ya Mradi wa *BRT,* msafiri atapunguziwa usumbufu kwani aina ya mabasi yatakayotumika yatakuwa makubwa na yenye hali ya kupunguza uharibifu wa mazingira.

(c) Utaratibu wa kubinafsisha Shirika ambao ulianza mwaka 1997, chini ya *PSRC* bado unaendelea kwa ushirikiano kati ya *PSRC* na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa tangu kuanzishwa kwa soko huru, wanafunzi Dar es Salaam wamekuwa wakipata shida sana ya usafiri na kwa kuwa kulikuwa na mradi wa mabasi ya wanafunzi Dar es Salaam, je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza mradi huo na mradi huo uliishia wapi?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, mradi wa mabasi ya wanafunzi haukuwa mradi wa Serikali.

**SPIKA:** Ndiyo!

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Kwa hiyo, sina jibu la kukupa kwa wakati huu.

Vile vile kutokana na jibu hilo, nawaomba wote wenye nia ya kusaidia katika kuleta miradi ya namna hiyo, uwanja uko wazi.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na malalamiko kwamba wanafunzi wamekuwa wakisumbuliwa sana wakati wa kupanda kwenye daladala hizi wakati wa kwenda na kurudi shuleni kutokana na nauli yao kuwa ni shilingi 50/=.

Je, Serikali inafahamu tatizo hilo na kama wanafahamu wana mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanafunzi hawasumbuliwi na wenye daladala?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mara kwa mara wanafunzi Jijini Dar es Salaam wanasumbuliwa hasa na hawa ndugu zetu wa daladala lakini pale ambapo inabainika kwamba wanafunzi wamenyanyaswa basi huwa mkondo wa sheria unafuatwa na kama umemsikia mara nyingi ndugu yetu aitwaye David Mwaibula, amekuwa mkali sana katika jambo hili na mara nyingi huwa wanafutiwa hata na leseni. *(Makofi)*

Hivi sasa shughuli zote hizi zitaratibiwa na Mamlaka ya Uchukuzi wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA),* nadhani watafuata nyayo za ndugu Mwaibula katika kulisimamia suala hili la wanafunzi kutonyanyaswa Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Na. 34

**Barabara ya Dar es Salaam - Rungwe**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara kuu ya Dar es Salaam - Mbeya hadi Malawi katika eneo la Kijiji cha Ibula, Kata ya Kiwira Wilayani Rungwe pana kona mbaya ambayo madereva wengi mara kwa mara wamekuwa wakishindwa kuikabili ili kupita salama na matokeo yake husababisha magari kuacha njia na kupaa kama ndege inapoondoka ardhini na kusababisha ajali za mara kwa mara na maisha ya watu kupotea kwenye ajali hizo:-

Je, Serikali inatoa utaalamu gani wa kurekebisha barabara hiyo hususan kwenye eneo hilo hatari ili kunusuru maisha ya wananchi yanavyopotea kutokana na ajali zinazotokea karibu kila mwezi kwenye eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Dar es Salaam - Rungwe ambayo Kitaifa inatambulika kama barabara ya Uyole - Ibanda - Kasumulu yenye urefu wa kilometa 102.8 inaanzia Uyole kwenye barabara kuu itokayo Dar es Salaam kwenda Zambia na inapitia Tukuyu Makao Makuu ya Wilaya ya Rungwe na inaendelea hadi Kasumulu mpakani mwa nchi jirani ya Malawi.

Katika Kijiji cha Ibula kilichopo kati ya Uyole na Tukuyu ambapo barabara hii inapita, wasanifu wa barabara hii walilazimika kuweka kona kwenye mteremko ili kukwepa milima na makorongo ambapo endapo barabara hii ingenyooka ingesababisha gharama kubwa sana za matengnezo. Ni kweli kuwa baada ya barabara kukamilika

kumekuwa kukitokea ajali za mara kwa mara zinazosababisha magari kushindwa kukata kona yakiwa kwenye mwende mkali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Homeli Mwakyusa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutatua tatizo hili suluhisho la awali ni kuendelea kutoa elimu kwa watumiaji wa barabara na hasa madereva na pia kuongeza alama za barabarani katika eneo hilo.

Magari mengi yanayoanguka katika eneo hilo husababishwa na madereva wake kutokutii alama zinazowatahadharisha madereva kuwa kuna mteremko mkali na kuwataka kupunguza mwendo.

Mheshimiwa Spika, aidha, uongozi wa Wilaya ya Rungwe unashauriwa kujenga kituo kidogo cha Polisi wa Usalama Barabarani katika eneo hilo kwa ajili ya kuwakabili madereva wanaopuuza alama za barabarani na pia kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kutunza alama za barabarani.

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika barabara hiyo ya kutoka Dar es Salaam - Mbeya - Rungwe kuna sehemu inaitwa Kijiji cha Chimala ambako vile vile hutokea ajali nyingi mara kwa mara na bado haijafahamika kuna sababu gani zinazofanya ajali za mara kwa mara zitokee pale Kijiji cha Chimala. Je, Wizara ilishafanya utafiti kujua ni sababu zipi ili tuondokane na hisia kwamba kuna uchawi pale Chimala ambao unafanywa na ndio maana zinatokea ajali mara kwa mara na mimi nilishapata ajali pale pale? Naomba jibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Chimala hakuna uchawi. *(Kicheko)*

Barabara ya Chimala ni nzuri isipokuwa tatizo ni kwamba madereva wanakwenda mbio na baadaye tukaja kujifunza kwamba lami ya Chimala inateleza, ni laini. Kwa hiyo, tunajua tatizo hilo, tunalichukulia hatua, tunataka kujaribu kuweka matuta ili watu wapunguze *speed* kabisa pale Chimala, tunapajua.

Na. 35

**Barabara ya Mlowo - Msangano**

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA** aliuliza:-

Kwa kuwa jitihada zetu za kuomba matengenezo makubwa ya kiwango cha changarawe yafanyike kwenye barabara za Mlowo - Kamsamba zinaonekana kushindwa licha ya ahadi kadhaa za Serikali kuhusu tatizo hilo sugu kutotekelezwa:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani sasa?

(b) Je, wananchi wa maeneo hayo wategemee kutengenezwa kwa barabara hiyo au laa; na kuwa itatengenezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Barabara ya Mlowo hadi Kamsamba ya moja kwa moja ina urefu wa kilometa 130. Aidha, kuna barabara za kupitia Igamba - Msangano - Utambalila yenye jumla ya kilometa 90.4 pamoja na ile ya Igamba - Isanza hadi Itaka kilometa 41. Barabara hizi zilizopo katika Wilaya ya Mbozi ni sehemu ya mtandao wa barabara za Mikoa zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi na zinahudumiwa na Wakala wa Barabara Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zimepata matengenezo kama ifuatavyo:-
(a) Barabara ya Mlowo - Kamsamba (kilometa 130). Katika mwaka wa fedha 2001/2002 barabara hii ilifanyiwa matengenezo ya kawaida jumla ya kilometa 95 kutoka Mlowo hadi Mbao kwa gharama ya shilingi milioni 36.2896 na matengenezo ya sehemu korofi ya jumla ya kilometa 4 kwa gharama ya shilingi milioni 66.582 kati ya Kijiji cha Itaka na Mwanjelwa.

Katika mwaka wa fedha 2002/2003, jumla ya kilometa 4 zilipata matengenezo ya kawaida kwa gharama ya shilingi milioni 29.904 kati ya Kijiji cha Mlowo na Zelezeta. Aidha, jumla ya kilometa 12 kati ya Vijiji vya Halugu na Itaka na Nambizo hadi Ipapa zilipata matengenezo ya sehemu korofi kwa gharama ya shilingi milioni 81.286 pamoja na kukarabati sehemu ya Halugu kwa gharama ya shilingi milioni 28.362.

Katika mwaka wa fedha 2003/2004, jumla ya shilingi milioni 26.136 zilitumika kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ambapo kipande cha barabara chenye urefu wa kilometa 32 kuanzia Utambalila hadi Mbao kilitengenezwa. Hali kadhalika daraja la Kamsamba limejengwa upya.

Katika mwaka wa fedha 2004/2005, jumla ya shilingi milioni 184.3 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali katika barabara hii hasa kuanzia Mbao - Kamsamba kupitia Utambalila.

(b) Barabara ya Igamba - Msangano - Utambalila (kilometa 90.4). Jumla ya kilometa 58.4 kati ya kilometa 90.4 ya barabara ya Igamba - Msangano - Utambalila, kuanzia Igamba hadi Msangano imetengenezwa na inapitika majira yote ya mwaka. Sehemu iliyobaki yenye jumla ya kilometa 34 (Msangano hadi Utambalila) inahitaji matengenezo makubwa kutokana na sehemu hiyo kupita kwenye bonde kubwa la mto na hivyo kusababisha kutopitika wakati wa mvua.

Katika mwaka wa fedha 2002/2003, jumla ya kilometa 6 zilifanyiwa matengenezo ya kawaida, kujenga makalvati na kuweka changarawe kati ya Vijiji vya Wesa na Isalabo kwa gharama ya shilingi milioni 38.212. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 0.66 kilitumika kugharamia matengenezo madogo madogo ya madaraja.

Katika mwaka wa fedha 2003/2004, jumla ya kilometa 43 kuanzia Igamba hadi Msangano zimechongwa kwa greda na kujengwa mifereji na makalvati kwa gharama ya shilingi milioni 22.615. Aidha, matengenezo makubwa ya daraja la Chifula yamekamilika kwa gharama ya shilingi milioni 12.8022 na jumla ya shilingi milioni 0.2184 zitatumika kwa matengenezo madogo ya madaraja kwenye barabara hiyo.

Katika mwaka wa fedha 2004/2005, jumla ya shilingi milioni 63.4 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hiyo.

(c) Barabara ya Isanza - Itaka (kilometa 41). Jumla ya kilometa 31 ya barabara hii ni kati ya kilometa 53.2 zilizofanyiwa ukarabati chini ya mradi wa *Core Rural Roads Rehabilitation Programme* uliokuwa unafadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la *USAID* kwa gharama ya shilingi milioni 663.31 na kazi zilikamilika mwaka wa fedha 1999/2000. Aidha, katika mwaka wa fedha 2000/2001 na 2002/2003 shilingi milioni 6.57 zilitumika kugharamia matengenezo ya kawaida na katika mwaka wa fedha 2003/2004 shilingi milioni 7.678 zilitumika kwa matengenezo katika barabara hiyo.

Sehemu toka Iporoto hadi *NAFCO* kilometa 8 inapita kwenye udongo aina ya tingatinga ambapo matengenezo makubwa yanahitajika ili barabara iweze kupitika nyakati zote za mwaka. Matengenezo hayo yanahusisha kunyanyua tuta, kujenga makalvati makubwa na kuweka changarawe na inakadiriwa kugharimu shilingi milioni 200 kwa matengenezo hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi...*(Kicheko/Makofi)*

Sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kwa ufupi sana. *(Kicheko)*

Kama nilivyoeleza kwenye maelezo ya utangulizi, Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo kadri ya bajeti itakavyoruhusu. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili matengenezo makubwa yaweze kufanyika katika sehemu nilizozitaja ambazo zinahitaji fedha nyingi za ukarabati.

**SPIKA:** Swali fupi sana la nyongeza Mheshimiwa Eliachim Simpasa, kwa sababu muda unakaribia kwisha.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, mimi naona swali hili sitaridhika sana lakini acha niulize tu, sijaridhika ningetaka nipate muda mzuri.

Kwanza limevurugwa sana kiasi ambacho sielewi nimeuliza nini na ninajibiwa nini, maana nimeuliza swali la barabara ya Kamsamba sasa nimepigwa maneno ya Mkoa mzima na halafu waliompa taarifa hizo wamempa taarifa za uongo tu. Mimi nafikiri baadaye nije nijibiwe vizuri. *It is a serious question now* tunafanya mambo ambayo hayaeleweki, ni mambo ya ajabu! Naomba tu lije lijibiwe vizuri. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Basi uliandike upya swali lako kisha litafutiwe nafasi baadaye lijibiwe kwa ukamilifu zaidi. Kwa leo tuishie hapo.

Waheshimiwa Wabunge, naona muda wa maswali umekwisha, yaliyobaki yatapangiwa muda mwingine. Kabla hatujaendelea, leo sina matangazo ya Vikao vya Kamati, labda nitekeleze ombi la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mwanza, ameniomba nitambulishe wageni wake ambao ni wanawake viongozi wa vikundi vya uchumi kutoka Wilaya nane za Mkoa wa Mwanza ambao wako kwenye *gallery* hii leo. *(Makofi)*

Tunawakaribisha sana viongozi wa vikundi vya Wanawake.

*(Hapa wageni waalikwa wa Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa walisimama na kuonekana)*

**SPIKA:** Baada ya hapo tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Kumi na Nne katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa mwaka 2004

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wa Mabadiliko ya Katiba. Leo msemaji wa kwanza ni Mheshimiwa Philip Marmo, atafuatiwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa na Mheshimiwa Eliachim Simpasa, ajiandae.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya awali ili na mimi nitoe mchango wangu wa mawazo katika Muswada huu muhimu.

**SPIKA:** Ungesubiri kidogo wanaokwenda kunywa chai waondoke. Mheshimiwa Phillip Marmo, ungekaa kwanza nitakuita katika wakati muafaka. Ehe, Mheshimiwa Phillip Marmo unaweza kuanza sasa na muda wako wa kusema unaanza.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, nilisema kuwa nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niungane na wenzangu kuwapa pole na kutoa mkono wa rambirambi kwa familia na wananchi wa Jimbo la Kasulu Mashariki kwa kifo cha Mbunge wao mpendwa Marehemu Frank Mussati. Pia nachukua nafasi hii kuwapa pole

sana Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Benito Malangila kwa kuondokewa na wenza wao.

Mheshimiwa Spika, tuliwahi kusema mahali pengine kuhusu umuhimu wa Katiba na uangalifu unaohitajika wakati maamuzi ya kufanya mabadiliko ya Katiba yanapofanywa. Niliwahi kusema mahali kwamba kwa sheria ya kawaida unapoamua kulitungia jambo sheria, kuna tatizo zito katika jamii ambalo unahitaji kulitatua, hivyo, kwa Katiba unapoamua kuifanyia marekebisho au kuitunga mpya, kwa hakika unataka kutatua tatizo zito.

Kwa hiyo, mbele yetu tunao Muswada ambao pengine unatarajia kutatua tatizo. Napenda tujiulize hivi ni matatizo gani hasa yanataka kutatuliwa na Muswada huu na kweli matatizo haya yanatatuliwa kwa jinsi Muswada ulivyoletwa au laa!

Mheshimiwa Spika, Muswada umegawanyika katika maeneo kadhaa Ibara zaidi ya 10, Ibara 24, lakini mimi kwa ajili ya muda, naomba unipe nafasi ya kujadili Ibara ya tatu mpaka ya saba, kwanza ambazo zinaongea kuhusu Haki za Binadamu na haki za raia, nikirejea katika malengo ya kubadilisha maeneo haya ya Katiba nilikuwa najiuliza tatizo ni nini na katika hali hii matatizo yanatatuliwa kweli au lah!

Waziri alitumia muda mrefu kutoa maelezo kuhusu matatizo yaliyopo na uamuzi wa kuleta marekebisho haya ili matatizo yatatuliwe. Kwa eneo hili la Haki nafikiri la msingi ni kwamba Katiba inatoa haki lakini kuna manung'uniko bado kutoka kwa wananchi, wanaharakati na wadau mbalimbali kwamba haki inatolewa kwa mkono mmoja na inachukuliwa kwa mkono mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ibara hizi zote tatizo hili limetatuliwa? Mimi nadhani hapana. Nasema hapana kwa sababu haki kama ilivyoainishwa na Katiba yetu ya mwaka wa 1984 hasa tulipoingiza dhana ya Haki za Binadamu na Haki za Raia katika Katiba kikwazo kikubwa ilikuwa ni masharti fulani fulani ambayo yamewekwa katika kutoa haki hizi au wajibu. Ukweli ufafanuzi uliofanyika kwamba haki kwa mfano haki ya kutoa habari, sasa imeelezwa waziwazi imepanuliwa kuliko ilivyokuwa hapo awali lakini ina maana hiyo yote kwa sababu yale masharti bado yapo, sheria ambazo zilikuwa zinafanya haki hizi zitolewe bado ziko, Sheria ya Vyombo vya Habari kwa mfano bado ipo, Sheria ya Usiri wa Nyaraka za Serikali bado ipo, sasa tunafanya nini?

Kwa hiyo, ndiyo tunajiuliza, hivi tunafanya nini? Lakini la msingi zaidi mimi nilitarajia kwamba kwa sababu ya hali halisi ya mwaka 1984 na leo tofauti ni kubwa basi eneo hili ambalo linaongea juu ya haki kwa vile wakati ule mtiririko ulikuwa moja kwa moja mpaka kwenye masharti na wajibu, basi sasa unapoanza kufafanua hizi ufafanue pia ufafanuzi mpya wa leo kuhusu Wajibu wa Raia na masharti ambayo yanatolewa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano mmoja wa kunukuu Ibara ya Katiba ambayo ilitarajiwa, nayo ingefanyiwa marekebisho sambamba na marekebisho yaliyoletwa na Waziri ili marekebisho haya sasa yawe na maana zaidi, hasa mimi

nilitarajia marekebisho haya yangekuja na marekebisho katika Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruhusa yako ninukuu Ibara ya 30 ya Katiba; "Haki na Uhuru wa Binadamu ambavyo misingi yake imeorodheshwa katika Katiba hii havitatumiwa na mtu mmoja kwa maana ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya Umma." Mwisho wa kunukuu Ibara ndogo ya Katiba. Hapa wakati umefika wa kutafsiri, nini maana ya maslahi ya Umma?

Naomba pia ninukuu Ibara ndogo ya pili ambayo inasema kwamba; "Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika sehemu hii ya Katiba yanayofafanua misingi ya Haki, Uhuru na Wajibu wa Binadamu hayaharamishi sheria yoyote iliyotungwa wala kuzuia sheria yoyote kutungwa au jambo lolote halali kufanywa kwa mujibu wa Sheria." Sasa huu ni mzunguko ambao nafikiri wakati ule mwaka 1984 ulikuwa na maana, lakini leo hauna maana. Nilitarajia kupokea mapendekezo ya kuangalia eneo hili kwa upya lakini pia Waziri angetuambia hatma ya sheria mbalimbali ambazo bado tunazo, kwa mfano Sheria ya Magazeti, Sheria ya Nyaraka za Serikali na kutunga sheria mpya.

Mheshimiwa Spika, nilitarajia kwamba, ili kuvipa Vyombo vya Habari uhuru zaidi, sasa angesema basi katika eneo hili kwamba Bunge litatunga sheria itakayowapa wananchi na Waandishi wa Habari uhuru na haki ya kupata habari. Kwa hiyo, sasa kupata habari yoyote ni haki yako, kwani utaulizwa, huoni sheria zilizopo? Katibu Mkuu wa Wizara yoyote atatoa habari ambayo tunafahamu kwa hali ya siku hizi wala siyo siri. Hilo ni eneo moja ambalo mimi nilidhani kwamba ile dosari iliyopo na ilitakiwa irekebishwe bado haijarekebishwa na mimi naamini tatizo la haki litabaki pale pale na bado wanaharakati na raia wenye nia njema tutazidi kudai kwamba Katiba inatoa haki kwa mkono mmoja, lakini inachukuliwa kwa mkono mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nilidhani wakati umefika sasa wa kuliweka sawa kabisa ni hili eneo la Mkurugenzi wa Mashtaka *(DPP),* nashindwa nianzie wapi. Labda nianze kwa kusema kwamba miaka 30 iliyopita katika miaka ya 1975 na 1976 Tume iliyoongozwa na Mheshimiwa Pius Msekwa ilitoa taarifa yake Serikalini na kutoa maelekezo ya namna nzuri zaidi ya uendeshaji wa Ofisi hii. Pengine taarifa ya Tume ya Msekwa imewekwa kwenye *shelf,* lakini kwa hali ya kawaida bila hata kwenda shule hali ilivyo ya uendeshaji mashtaka nchini na maelezo haya ya Katiba ni kama tunaweka mkokoteni mbele ya punda, asilimia zaidi ya 95 ya mashtaka nchini hayaendeshwi na Mkurugenzi wa Mashtaka wala hajui.

Kuna maelfu ya Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, sidhani kama Mkurugenzi wa Mashtaka anafahamu kinachotendeka kule. Kwa kweli ni vurugu na ndiyo maana kazi kubwa ni watu kubambikizwa kesi katika Mahakama za Mwanzo na Wilaya na imefikia mahali pabaya zaidi, ndiyo maana wananchi wanasema tunaweka mkokoteni mbele ya punda. Tumefikisha Wilayani *PCB,* hiki chombo chetu cha rushwa lakini kinafanya nini Wilayani? Kwa sababu Wilayani hamna *DPP,* hamna Mkurugenzi wa Mashtaka kutoka Ngara itabidi waombe kibali Dar es Salaam. Tumetumia fedha

nyingi sana kuwapeleka watu Wilayani, sasa kesi haziendi. Je, haya ni mapambano dhidi ya rushwa? Haya maelezo maana yake ni nini ukilinganisha na hali halisi ya uendeshaji wa mashitaka na kuweka sawa utafutaji wa haki na utawala bora kwa ujumla wake wote wakati tuna maelezo haya kwenye Katiba, wakati asilimia 95 au zaidi ya 95 ya mashitaka yanaendeshwa na watu ambao hata kidogo hawawajibiki kwa Mkurugenzi wa Mashtaka hawa ni wanajeshi, Polisi, Polisi ni Jeshi, nidhamu yao ni ya kijeshi katika uendeshaji wa mashitaka, hata siku moja katika hali halisi hawajawajibika kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Ni maoni yangu kwamba yaliyoandikwa hapa ni *redundant,* hayana maana yoyote katika hali halisi ya uendeshaji wa mashtaka katika nchi yetu. Kwa hiyo, narejea kusema kwamba yaliyotarajiwa kurekebishwa hata kidogo hayarekebishwi na mimi nafikiri ni utaratibu mbaya wa kutunga sheria. Kujaza maneno mengi kwenye vitabu hata kwenye Katiba, maneno ambayo hayana maana yoyote katika hali halisi ya asilimia 95 ya raia wako ni namna mbaya ya kutunga sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningesema zaidi, lakini la mwisho kwa sababu muda unakwenda, ni hili la Viti vya Wanawake. Tupende, tusipende tutabadilisha Katiba kuhusu suala hili na napenda haki itendeke kwa sababu hawa ni zaidi ya nusu ya raia wa Tanzania. Kwa nini tusifanye uamuzi wa msingi kabisa wa kusema kwamba Wilaya moja iwe na Wabunge wawili, mmoja mwanamke na mmoja mwanaume wachaguliwe na watu wote. Najua itaumiza wengi ambao tuna Majimbo zaidi ya moja katika Wilaya lakini siku moja lazima tufikie hapo kwa sababu hii yenyewe siyo sahihi, kwanza ni ubaguzi. Katika hali halisi ni kwamba tunafumba macho na kwa hakika ni zoezi la muda mfupi tu, wenzetu wanaokuja baadaye hawatakubali hili.

Kwa hiyo, namna ambavyo nafikiri tutakuwa tumetulia kidogo na Katiba yetu haitakuwa na mabadiliko ya mara kwa mara katika eneo hili ni kufanya uamuzi kwamba Jimbo au Wilaya iwe na Wabunge wawili, mmoja mwanaume na mmoja mwanamke kwa sababu katika hali halisi ya Tanzania, hali halisi ya Afrika siyo rahisi wanawake kufikia asilimia 30 au 50, lakini tukichukua uamuzi huu kuwa wajasiri nafikiri tutakuwa mbali zaidi kuliko jinsi ambavyo tunalichukulia suala hili namna ambavyo wengi wanatulaumu kwamba tunakiuka haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi fursa hii ya kusema machache kidogo kuhusu *agenda* hii muhimu inayohusu nchi yetu.

Mimi niseme tu kuwa natumia fursa hii kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapigakura wangu wa Jimbo la Gando kutoa pole kwa wale wote waliofikwa na misiba ya aina mbalimbali Mungu awape subira na malipo yanayofaa.

Baada ya hayo kwa kweli wenzetu wameshasema mengi juu ya jambo hili lakini tuna wajibu wa kusisitizia baadhi ya mambo ambayo tunafikiri ni muhimu.

Mimi napenda nianze na *agenda* hii inayosema Kukaimu nafasi ya Urais na hapa labda nianze kwa kusema kuwa katika nchi yetu kuna Katiba mbili, tuna Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tuna Katiba ya Zanzibar.

Kwanza najiuliza, hivi kuna *supremacy* katika Katiba hizi mbili? Ipi ni *supreme?* Kama ipo au kama hapana, hilo ni suala la kujiuliza sasa tunapokuja hapo natazama hii nafasi ni kweli kuwa kumshirikisha labda Spika au kumshirikisha Jaji Mkuu katika kukaimu nafasi hii pengine kungekuwa na usumbufu wa namna fulani katika utendaji wa kazi. Lakini najiuliza kwa nini hakufikiriwa Rais wa Zanzibar kushika nafasi hii? Hivi *protocol* inasemaje? Ni nani *senior* kimadaraka baina ya Rais wa Zanzibar na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano? Ni nani *senior* ki-*protocal?*

Kama tutapata majibu ya maswali hayo, basi tungeweza kufikiria kwa sababu Rais wa Zanzibar anachaguliwa na watu hata ukiangalia anavyoapishwa ni tofauti na Waziri Mkuu. Mambo yote haya ni ya kuzingatia kwa sababu tunayaweka kwenye Katiba, sasa tukipata majibu hayo tutaweza kujua ni nani basi anaweza kukaimu. Sina tatizo na Waziri Mkuu aliyepo sasa, *in fact he is my friend* ningependa hata awe Rais achilia mbali kukaimu, lakini hizi ni *institution* ni lazima tufikirie kwa kina kikubwa.

Pili, hapohapo niunganishe katika suala la uwiano ambalo tumekuwa tukilizungumza. Nazungumzia nafasi zile tano za Baraza la Wawakilishi. Kwa sasa utaratibu ni kuwa wanaoingia mle kutoka vyama mbalimbali wanapeleka majina yao na yanapigiwa kura. Utakuta ni utaratibu wa kidemokrasi labda kuwa wanapigiwa kura wanaowakilisha lakini hata humu Bungeni tungeweza kutumia fursa hiyo ikafanywa bila ya kuzingatia mambo fulani labda watu wetu wanaokwenda katika *SADC,* wanaokwenda kwenye Bunge la Afrika kunazungumzwa uwiano na uwiano unakuwa ni uwiano wa kweli kwa sababu unakuwa na nafasi nane za kutoka Upinzani, Bunge zima linapiga kura kwa nafasi moja ya Upinzani kwa mfano au mbili lakini vyovyote itakavyokuwa atakayetoka mtu atakuwa ni wa Upinzani.

Hii ni hatari kwa sababu wale ambao wanakuwa wengi katika Baraza mara nyingi kama utatumika utaratibu uliopo sasa pamoja na kusema kuwa labda watakuwa wanawake watatu au wanaume wawili lazima iwekwe *proportional* ambayo itawapa watu wengine fursa ya kuweza kuwakilisha chombo kile muhimu katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, sasa nije katika nafasi ya Tume ya Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi ni chombo muhimu sana katika kuimarisha Demokrasi na Utawala Bora katika nchi kwa sababu ndiyo chombo ambacho kwa kupitia kwake na kwa uangalifu wake wanapatikana viongozi wanaoongoza Taifa. Sasa tuna hoja hii tunayoisema au kuna hoja hii inayojengwa ya kuwa chaguzi zote ziangukie kwenye mikono ya Tume ya Uchaguzi na msingi wake hapa ni kuondoa malalamiko kwa sababu sasa hivi tumejifunza kuwa kwa sababu chaguzi za *Local Government* zinapokuwa chini ya Waziri anayehusika na mambo hayo anakuwa na fursa ya kufanya mambo ambayo watu wengine walayalalamikia tena sana tu.

Sasa Tume pamoja na kwa kuwa Tume ni watu pamoja na kuwa hao watu wana *reservation* zao juu ya Tume lakini wakiangushiwa dhamana inakuwa ni Tume ya Uchaguzi na siyo watu wengine ambao labda wako chini ya mamlaka ya Waziri na kwa kweli wanafanya vitu ambavyo walio wengi wanavilalamikia labda waliokuwa hawavilalamikii ni wale ambao wanafaidika.

Sasa hapa niseme tu kwamba nafarijika kusikia kuwa kuna mabadiliko ambayo yata-*incorporate* mtu mmoja au wawili wa Upinzani. Ningependa labda iwe zaidi ya hivyo kama nafasi itaruhusu na hapo nipate fikra ya kuamini kuwa hilo litatusaidia kwa sababu watu wanasema kuwa Tume ni huru, hivi sasa wengine wanasema Tume ni huru, Wajumbe wake ni huru labda hiyo fikra siyo mbaya lakini tukiangalia historia ya nchi yetu hapa tumekuwa na Vyama vya Siasa, tumekuwa na Chama Cha Mapunduzi ambacho watu walio wengi hapo nyuma wamekuwa ni waumini aidha *direct* au *indirect* wa Chama Cha Mapinduzi. Sasa kama wanachaguliwa wanaingia kwenye Tume fikra ni kuwa wale watu hata kama hivyo sivyo lakini fikra ni kuwa wale bwana ni wana-CCM watupu. Lakini sasa ikiwa watu wa Upinzani wataweza kuingia na naomba waingie, itasaidia kuweka *balance* kidogo ingawa kuna uchawi unafanywa, inakuwa rahisi kuona na uchawi ukionekana haufanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, labda sasa nije kidogo katika sehemu hii ya Baraza la Ushauri. Mimi naona tuangalie udhaifu tulionao, tunaye Rais wetu hapa ameshafanya kazi katika vipindi viwili vya miaka kumi na washauri alionao na niwaelewa, hasa tunayemjua sana ni mshauri wake wa Mambo ya Siasa ambaye kwa sababu ni Mbunge mwenzetu na yupo Mshauri wa Mambo ya Ulinzi ambaye wengine tunamfahamu lakini hatujasikia kuwa Rais ameharibu sana kazi kwa kuwa hakuwa na washauri wazuri. Kama ameharibu atakuwa ameharibu na kama ametengeneza ametengeneza. Suala si washauri, hii mimi nafikiri ni *continuation of power* ambayo nafikiri italitia Taifa katika gharama kubwa ambayo siyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri hiki chombo kikafutwa. Waliomaliza mamlaka yao wakae nyumbani kama alivyosema Marehemu Oginga Odinga au waende kwenye mashamba yao wajilimie wafanye kazi zao na Rais aachiwe afanye kazi kwani ana vyombo vingi vya kumshauri kwa mfano ana Baraza la Mawaziri, pia ana Tume mbalimbali na hivi vyote ni vyombo muhimu ambavyo kwa mujibu wa sheria vinamshauri katika mambo muhimu na hapana haja ya kuwekwa chombo hiki ambacho kwa maoni yangu mimi itakuwa ni nafasi ya kuwapa watu fursa ya kuendelea kutawala ilhali Katiba na Mamlaka ya nchi yameshawasitisha katika utawala huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie kifungu hiki kinachozungumzia mabadiliko katika Ibara ya 19, nchi yetu haina dini hiyo ni kweli lakini kwa upande labda wa Zanzibar kuna vyombo ambavyo vinashughulika na mambo ya dini na viko chini ya Serikali. Tuna Kamisheni ya Wakfu na Maadili ya Amana, Ofisi ya Mufti, Mahakama ya Kazi ambayo inatambuliwa na Katiba yenyewe. Sasa pale nilipokuja nikazungumzia *supremacy* najaribu kuoanisha hapa hivi baada ya kupita Katiba hii akatokea mtu mmoja kutoka upande mwingine wa Tanzania akahoji kwenye Mahakama hivi, kwani hivi

vyombo vipo katika sheria gani? Tunafanyaje katika hilo? Sasa hayo yote hayo ni mambo ya kuyazingatia ili tuweze kuweka misingi mizuri ya utawala ambayo baadaye hayataweza kusababisha manung'uniko kama inavyojitokeza kwa baadhi ya vitu mbalimbali vilivyopo katika Katiba. Hivi sasa kutokana na kutoangaliwa vizuri hapo mwanzo au kwa kuviangalia vitu kwa kina kidogo kumbe athari yake ni kubwa katika utawala wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza na mimi nitoe rambirambi za wananchi wa Jimbo langu kwa wananchi wa Jimbo la Kasulu Mashariki kwa kumpoteza Mbunge wao na wengine wote ambao wamepata maswahib hayo, Mungu aweze kuwafariji. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kuna vipengele vichache tu ambavyo mimi naangalia. Nataka kuchangia kuwa Katiba ndiyo Sheria Mama na kutokana na Katiba ndiyo sheria za nchi zinaweza zikatungwa, kwa hiyo, nafarijika kwamba mambo hayo yatazingatia vile vile sheria ambazo zitakuwa zimefafanua mambo vizuri kwa sababu Katiba haiwezi ikafafanua kila kipengele. Lakini ni kitu ambacho hakiwezi kikafanyiwa mabadiliko kila siku ila tunashukuru kwamba tumekuwa liberal au watu ambao wanakwenda na wakati ndiyo maana tunaendelea na mabadiliko haya ya 14 .

Katika ile Ibara ya 18 sina tatizo na (a) lakini (b) na (d) kuna mambo ya haki pale, haki ya uhuru wa mawazo. Mimi ninazisoma zote zile mbili naona bila kuangalia sawasawa kwa mfano (b) inasema; "Mtu mwingine anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari." Sawa, anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake. Sasa hiyo mimi naona siyo sawa kwani ni lazima pale itakapoonekana mawasiliano yake ni hatari lazima aingiliwe.

Mheshimiwa Spika, kuwe na udhibiti wa namna fulani kama mtu anafanya mawasiliano ya kutaka kuangamiza nchi au kufanya jambo baya kwa nchi ukiliacha loose namna hii inaweza ikawa ni hatari sana kwa nchi. Kwa hiyo, ni lazima kuwe na *control* ambayo inaonyesha kwamba hapa mtu anafanya lakini siyo kwa hatari ya nchi ni kwa manufaa kwamba anakuwa *excess* lakini hawezi kuiingiza nchi katika matatizo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nimeona nichangie ni mamlaka ya nchi na dini. Hapa ilivyoandikwa pale ni kana kwamba mtu anaweza akafanya dini apendavyo tu bila kudhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema zipo dini sasa hivi ambazo haziendani na maadili ya nchi yetu sasa huwezi kuachia tu watu wajiendeshee mambo yao ya dini bila hata kudhibitiwa. Wapo watu ambao wanakwenda wanaanza kutokana wenzao hawahubiri dini bali wanahubiri kutokana na wenzao sasa watu hawa lazima wadhibitiwe. Tumekumbana na mtu anaingia pale mimi nasema hivi huyu kweli anahubiri dini au amekwenda kutoa *lecture* kuhusu mambo anayotaka yeye. Anatumia muda mwingi anatukana wenzake na anafanya anavyotaka mwenyewe ama yuko

Kanisani na Makanisa yenyewe yamegawanyika, kuna Makanisa ya sisi Wakristo kuna wenzetu Waislam sasa inawezekana katika kundi tu la Wakristo wengine wakajitenga wakaanza kutukana wenzao kwamba wale ni hovyo, ni washenzi, ni mashetani.

Haya katika mambo mengine ya dini, kwa wenzetu Waislam, wengine wakasema hawa ni makafiri na nini. Kwa hiyo, tukikubaliana na vitu kama hivyo kwamba wawe na uhuru kiasi hicho lazima Katiba ilindwe, kama unakwenda kuhubiri na umesajili kuhubiri, hubiri dini yako sio uende ukaanze kuhubiri watu wengine, hapana. Mimi nadhani hili lazima tuliangalie kwa sababu tunapoelekea inaweza kuleta matatizo, watu wakaamua kwamba hatuwezi kutukanwa namna hii ngoja tuwafuate huko huko Kanisani au Msikitini tupambane huko huko, halafu ikawa vurugu.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri hili hapana, lazima Serikali, mamlaka ya nchi idhibiti kwamba ahubiri kile alichoandikisha yeye sio kuhubiri kitu kingine kama kutukana wengine kwa sababu dini ni kumshawishi mtu aje kwako sio umtukane, hata kidogo. Watu wengine wanasema kama wewe ni mwoga unaswali, endelea kuswali, yangu yanakuhusu nini, mimi nikienda motoni inakuhusu nini, watu wanasema, nikienda motoni sio lako, niache mimi niendelee na shughuli zangu, kama wewe ni mwoga endelea na shughuli zako. Kwa hiyo, mtu asiingilie uhuru wa mtu mwingine kabisa katika masuala ya kuabudu, lakini Serikali lazima idhibiti vitendo kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, hilo linafanana na ile Ibara ya 20, pale ambapo kuna mambo ya itikadi na falsafa yoyote ile ya siasa, mtu anaruhusiwa kuendelea. Hapana, zipo siasa zingine zinaleta kuvunja umoja na amani. Sasa hiyo lazima tuikatae, hatuwezi kukubali bwana, watu wanasema watatumia upanga, lazima watu waingie kwenye Chama chao, tuseme aaa, endelea tu. Hilo hapana, hilo ni lazima Katiba iweke wazi kwamba ili mradi havunji sheria na akivunja sheria abanwe na Chama ambacho kinaleta siasa ambazo ni mbovu kiondolewe au kifutwe, kwa nini kiwepo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii habari ya kubembelezana imeshapitwa na wakati tuna encourage, tumechochea mambo mengi ambayo hayana hata maana tunamwogopa mtu wakati analeta hujuma, wewe kama mwanasiasa piga siasa nzuri watu waokoke wafuate siasa yako, lakini kusema wataingia kwa upanga, jino kwa jino, sijui itakuwa nini, mtu ataipata, damu itamwagika. Ahaa, sasa hii tena itakuwa nchi ya namna gani. Kwa hiyo, Katiba lazima iseme wazi ahubiri siasa, a-*convince* watu ili wamfuate kwenye Chama chake, iwe CCM, *CUF* au *UDP*, hubiri siasa tu lakini sio kutaja damu, damu unataja za wenzio tu wewe zako mbona hutaji! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kutaja damu za wenzake zitamwagika wakati yeye yupo London anakula kule, watu wanakufa huku, hakuna kitu cha namna hiyo. Kwa hiyo, hilo lazima tukubaliane kabisa kwamba Katiba inasema hakuna kitu cha namna hiyo ambacho tunaweza kukiendesha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi sijui nisemeje, lakini hii habari ya zile kura ambazo Jimbo ambalo halina mgombea, sasa atapata hiyo asilimia waliyosema kwa zile

atakazopata Rais. Sasa pengine wapo wanaompenda Mbunge wao na wamempigia Rais mwingine, sasa hapo si utampunja mtu! Maana kuna mahali fulani Mbunge na Rais wanapishana sana kura, wanampigia Mbunge kura nyingi kuliko Rais.

Sasa katika utaratibu huu mtu si anaweza kuumia hapa? Halafu kule kwingine wanasema asilimia hamsini au hamsini na moja za wale ambao wamejiandikisha lakini ukweli ni kwamba sio wote wanaojiandikisha wanapiga kura. Mara nyingi wanajiandikisha watu wengi lakini wanaopiga kura ni wachache. Sasa basi labda hiyo asilimia hamsini na moja iwe kwa wale ambao walipiga kura siku hiyo, lakini kusema waliojiandikisha wanajiandikisha wengi na wanapiga kura wachache, kwa hiyo mwingine anaweza kupunjika katika hili. Kwa hiyo, hili nalo lifikiriwe na liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, hili jambo lingine la Wabunge wa Viti Maalum linatakiwa liwekwe sawasawa, unaweza kuonekana wewe unapinga mambo haya, lakini kuna mwenzetu alichangia jana nilimsikiliza vizuri sana. Tunasema haya mambo kuweka kwenye Katiba yasiwekwe kwa utaratibu huu. Sasa hivi tunatawala sisi na baadaye hatujui huko tunakoelekea, hili labda linaweza kuwekwa kwenye sheria ya uchaguzi, ile Tume ikatafuta namna nyingine. Kuiweka namna hii mimi sioni kama inafaa, tunahitaji akinamama sawa, lakini mwenzetu mmoja alisema *let us encourage them,* tutafute namna nyingine ambayo akinamama wataingia Bungeni kwa wingi na wapo akinamama wamepigania wamepita, lakini kuna wengine wameingia kwa Viti Maalum na wao wanasaidia sana nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba hii sio dawa. Kwanza dunia nzima wanaipinga hii imebaki nchi kama tano au sita, wanasema hakuna haki ya namna hiyo. Tunataka tuwe na akinamama, hiyo ni lazima kwa sababu kweli akinamama wana mawazo mazuri sana, lakini sehemu nyingine wanasema mnawadhalilisha. Sasa tutafute namna gani wanawake wanaweza kuwa wengi Bungeni bila kusema ni viti Maalum, upendeleo na nini, uwepo utaratibu mwingine na pengine kwenye sheria sio kwenye Katiba namna hii.

Mheshimiwa Spika, halafu mkija kufuta hii baadaye na watu wamezoea utaratibu huu wanaweza wakarudi katika kuangua kule kule kwa zamani. Ni lazima watu waanze kujifunza mbinu za kugombea, lakini kwa utaratibu mwingine wa namna akinamama wanaweza kugombea ili tuwapate wengi. Hii tunasema Viti Maalum, upendeleo na nini sidhani hata kama wenyewe wanapenda kuitwa viti maalum vya upendeleo na nini. Inatisha! Sehemu zingine ukienda ukatamka hii watu wanacheka, wanasema ni kitu gani mnafanya, tafuteni namna ya kuwawezesha akinamama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili nadhani lifikiriwe, lakini bado tunahitaji akinamama na tunashukuru sana Rais amejitahidi sana katika nafasi mbalimbali kuweka akinamama na wameonyesha uwezo wao, huo ndio ukweli wenyewe, wamekamata Uwaziri, Ukuu wa Wilaya, Ukuu wa Mkoa kama Mheshimiwa Hilda Ngoye ni mmojawapo, akina Anne Makinda walishafanya hilo. Kwa hiyo, kuna njia nyingine ambazo akinamama wangeweza kujaa lakini sio kwa kusema kuna upendeleo hapa Bungeni, hapana, tunaweza kutafuta utaratibu mwingine. Lakini tunampongeza sana

Rais kwa kujitahidi sana kufanya *balancing,* nadhani katika Afrika amejitahidi mzee wa watu, tunamshukuru sana katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii Tume ambayo inataka kuundwa ambayo wanasema wataweka na wanasiasa humo ndani. Mimi nadhani itakuwa na vurugu kweli sijui kama wanasiasa wakikutana wanaweza kupatana kweli. Mwalimu Nyerere aliwahi kusema, kura zinapigwa, chombo cheupe kabisa, kimekung'utwa, jamani mmeona, tumeona, wote mmedhibitisha, ndio. Haya kura zinapigwa. Tunahesabu hapa hapa jamani, ndio. Watu wote wanakubali.

Baada ya muda aliyeshindwa anasema bado siamini. Siasa inaanza pale pale. Inawezekana kuna zingine zilikuwa nyuma ya meza. Sasa nataka kusema hiyo Tume ambayo itakuwa na wanasiasa itakuwa ni Tume ambayo itashinda hata mwezi mzima au miezi miwili bado wanabishana namna ya kutangaza Rais na majina ya watu waliopita. Nilidhani hiyo si tungetafuta watu neutral, tungeshirikiana wote kama ni Vyama au nini lakini tutafute watu neutral, lakini wanasiasa kuingia kwenye Tume matokeo yake yatakuwa ni mabaya sana hakuna atakayekubali. Kwa hiyo, tutajiingiza katika jambo ambalo tunajua ni tatizo tu wala sio uhuru tena.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kama sisi ambao tunashangilia mpira. Hivi mimi nikienda kushangilia timu ya Simba suala la Yanga kucheza vizuri linanihusu nini. Mimi nasema kwanza yule amekosea tu, fyeka mguu wake pale, kwa nini anapiga chenga, fyeka hapo ili amwangushe yule anataka kupita kwenda wapi kwa sababu nilikwenda kushangilia Simba hata wakimwangusha mtu wa Simba nasema ahaa, bahati mbaya, ametereza tu. Sasa ndio hii kwenye siasa, unakwenda pale kura zinahesabiwa. Lakini mtu amesema hapo turudie, tutachelewesha mambo.

Labda tungeweza kutafuta namna ya kukutana wote kwa pamoja, tukatafuta watu ambao ni waadilifu ambao ndio waunde hiyo itatusaidia, lakini wanasiasa hiyo naona itakuwa ni kazi kubwa sana na ngumu sana. Sasa mimi sijui wengine wanaonaje, lakini hiyo ya kumlazimisha Rais akiteua watu kumi lazima achukue hamsini kwa hamsini, wanawake watano na wanaume watano, mimi binafsi naipinga na naomba nieleweke hivyo. Mimi nadhani Rais apewe uhuru akiteua wanawake wanane, sawa, akiteua wanawake wote, sawa. Lakini sidhani kama Rais mwadilifu atateua wanaume watupu, haiwezekani. Hiyo haifai kabisa na hii *trend* huku inakokwenda sio nzuri, itafika mahali fulani itakuwa ngumu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nashukuru na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii na mimi niungane na wenzangu katika kuchangia hoja hii ya mabadiliko ya kumi na nne ya Katiba ya nchi yetu. Kwanza napenda nitoe pole kwa niaba ya wananchi wa Sengerema na kwa niaba ya familia yangu kwa familia ya Frank Musati, aliyekuwa Mbunge mwenzetu kutoka Kasulu Kigoma. Vile vile nawapa pole

ndugu zetu wengine waliopata misiba mbalimbali. Tunawaombea Marehemu wetu hao Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nina mambo kama matatu hivi ambayo napenda kuyazungumza. La kwanza kabisa, ningependa nitoe pongezi kubwa sana kwa viongozi na wananchi wa Tanzania kwa jinsi tulivyojitahidi kuendeleza amani ya nchi yetu kwa miaka inayofika arobaini sasa. Amani ni kitu muhimu sana. Baada ya uhuru kama viongozi hawafanyi kazi zao vizuri kwa vyovyote vile katika nchi za Afrika migogoro inatokea. Lakini kwa nchi yetu ya Tanzania viongozi wetu kuanzia na Baba wa Taifa mwenyewe mpaka sasa hivi tukiwa tunaongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, wamejitahidi sana kushirikiana na wananchi kuhakikisha kwamba tuna amani inayoendelea na kitendo hiki cha kuleta mabadiliko ya Katiba ni sehemu mojawapo naamini ya kuendeleza amani ya Tanzania kwa njia ya kusikilizana kupitia chombo cha wananchi ambacho ni Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, heshima ya Tanzania huko nje au Kimataifa ni kubwa na hata sasa hivi wapo Watanzania mbalimbali ambao wanaendeleza heshima hiyo na tunadhani kwamba tukiendelea kusikilizana kwa njia ya mabadiliko kama haya ya Katiba tunaweza kuendeleza vile vile heshima ya Tanzania ambayo imetanda katika Afrika na bado imetanda katika maeneo mengine ya dunia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, napenda kusema kwamba ili tuweze kuendeleza amani lazima tuendelee kukubaliana mambo ya msingi na mambo ya msingi ni pamoja na Katiba yetu ya Jamhuri ambayo inagusa utawala wa nchi mbili, Tanganyika na Zanzibar na ndani yake tunatafuta haki. Haki ya mtu mmoja mmoja, haki ya vikundi, haki ya Vyama vya Siasa na haki zingine mbalimbali. Pia ndio maana nakubaliana na wasemaji walionitangulia kwamba hapo mwaka 1984 tulipokubaliana kwamba tunaweka ndani ya Katiba haki za binadamu au vipengele vinavyohusu haki za binadamu, tuliweza kusonga mbele katika kusikilizana na kuendeleza amani kwa sababu mtu binafsi aliyezaliwa na mwanamke siku zake za kuishi lazima atatafuta haki na anastahili haki. Kwa hiyo, tukiwa tunaandaa mapendekezo ya mabadiliko ya Katiba, ni vizuri kuzungumza kwa kina na kwa muda wa kutosha maeneo gani tunapenda kuyafanya mabadiliko ili tunapokubaliana tunakubaliana kama nchi moja ya Tanzania inayotaka kuendeleza amani na haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina hofu kwamba hatutoi nafasi za kutosha katika mazungumzo, hata kama safari hii tunasema katika hoja ya Waziri kwamba *White Paper* ilitolewa, lakini bado ingeweza kutolewa nafasi nyingine ya kusema kwamba Muswada umewekwa mbele ya nchi sasa uzungumzwe kwa kina kadri inavyowezekana ili tujaribu kuondoa dukuduku mbalimbali kwa lengo la kuendeleza amani na kuzuia migogoro.

Mheshimiwa Spika, mimi nafadhaika sana kama mmoja wa Watanzania ninapoona dalili za migogoro. Mathalan kama Katiba haitakidhi wenzetu wa Tanzania Zanzibar wanasema nini, tutakuwa tunaongeza madukuduku na inawezekana tukawa tunaashiria kuleta migogoro. Ni lazima tukubaliane hata kama Bunge litakaa kama Kamati maalumu ya kuzungumza ndani ya Bunge kwamba ni wapi ambapo hatukubaliani ili tuweze kuona kwamba tunafanya mabadiliko ya kutufaa sisi sote. Mimi huwa

sipendezewi hata inapotokea kwamba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanaotoka Zanzibar wanakwenda kuzungumza mahali peke yao. Hii inanipa wasiwasi kwamba hivi ni mambo gani ambayo sisi kwa pamoja hatujaelewana au hatuelewani. Ni lazima kwa kweli tudumishe utamaduni wa kuzungumza kwa pamoja mpaka tunaridhiana na huo utamaduni tumeachiwa na Baba wa Taifa ambapo alisema wakati wake ule kwamba katika siasa ya Waafrika mazoea yetu ni kuzungumza chini ya mti mpaka tunakubaliana.

Mheshimiwa Spika, nayasema hayo kwa sababu napenda kupendekeza kwamba ni lazima tupanue wigo wa mashauriano ili tuzuie kabisa uwezekano wa kuwepo kwa migogoro ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Kisiwa cha amani hiki watu wengi wanakionea maya, wivu, kwa hiyo ni sisi viongozi pamoja na wananchi ambao tunawawakilisha tuendeleze nguvu zote za kushauriana kuhakikisha kwamba tuna amani na ndani ya amani ndio unakuta kuna haki.

Kwanza tunaipongeza Serikali kwa kuondoa lile suala la Baraza la Ushauri kwa Rais. Hilo tunaipongeza Serikali kwa sababu sisi wengine tulidhani kwamba vyombo tulivyonavyo mpaka sasa tukivitumia vizuri hatuna sababu tena ya kumwongezea Rais mzigo wa Baraza la Washauri, anao tayari na busara zake zitaonyesha kwamba lazima atawatafuta.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna suala lingine ambalo napenda niliseme, ni kwamba hivi tumeogopa nini Watanzania kuingia katika sera ambayo wenzetu wanaitumia, nayo ni sera ya wagombea binafsi. Suala hili wala silizungumzi hapa kuunga mkono hoja ya Wapinzani, sio ya Wapinzani hii. Hoja hii ilikuwa ni ya Baba wa Taifa tangu mwanzo, hivi tunaogopa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilidhani Vyama vya Siasa vingeimarika maradufu kwa kuweka utaratibu wa wagombea binafsi. Mimi ndiyo sayansi yangu ya siasa inavyoniambia. Katika mabadiliko haya ya Katiba yanayokuja mwaka 2005 hivi bado tumeogopa jambo hili! Kwa nini tusingeliweka? Mbona Vyama vyetu ni imara lakini kama sio imara bado watatokea watu walioumbwa na Mwenyezi Mungu ambao wangependa kujitegemea. Uzuri wa haki za binadamu ni kwamba binadamu aliyeumbwa na Mwenyezi Mungu na kuzaliwa na mwanamke ana uwezo wake binafsi wa pekee. Ana sifa zake binafsi ambazo huwezi kusema akiingia kwenye Chama fulani ndio zitaongezeka, aaa, kila mtu ana kipaji chake ambacho amepewa na Mwenyezi Mungu na kipaji hicho au uwezo huo ndio anaweza kuutumia ndani ya haki zake ikiwa ni pamoja na haki ya kuwakilisha wenzake.

Mheshimiwa Spika, sasa suala la mgombea binafsi kwa maoni yangu tusingelionea haya, tungelileta wakati huu na tukaanza kulitumia. Kwa maana hiyo ninapendekeza pamoja na maeneo mengine ambayo hayakuweza kuletwa tuzungumze baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu. Tuzungumze mapema juu ya kwenda kwenye maeneo hayo ili tuyafikie, mojawapo likiwa ni hilo la wagombea binafsi kama ni kuanza kujiandaa basi tuanze kujiandaa na taratibu zake. Mbona tumeweza kuleta hili suala la *proportion representation* na japo limepitia kwa akinamama lakini tumeiingiza dhana hii na kuikubali na mimi nashauri moja kwa moja kwamba hili tungeliweka kwenye sheria.

Kukimbilia kuweka mambo kama haya kwenye Katiba asilimia thelathini, sasa ikitokea kwamba kwenye Majimbo wameshinda akinamama, halafu bado *proportion representation* ikawa ni asilimia thelathini, maana yake utakuwa na Bunge la wanawake asilimia karibu sabini au themanini. Tungeweka kwenye sheria, lingeweza kutusaidia sana. Tunapenda, sisi tumekubali, wanaume tunawapenda wanawake zetu, tunawakubali, tumesema kwamba wawepo katika asilimia hiyo ambayo imekubaliwa na nchi za *SADC,* lakini tuiweke kwenye sheria siyo lazima tuiweke kwenye Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wangu umekwisha napenda niungane na wenzangu waliosema kwamba wateuliwa wa Rais kuingia Bungeni sio lazima tuweke watano watano, tumwachie Rais uhuru wake atapata watu wenye busara.

Mheshimiwa Spika, la mwisho napenda niseme kwamba ili kuweka utawala bora katika siku zinazokuja Bunge lithibitishe viongozi wakuu wanaoteuliwa na Serikali. Hii ni hoja kamili ambayo hapa ndani tulikwishaizungumza, mimi kwenye Kamati yangu ya Mambo ya Nchi za Nje tulikwishaizungumza, tukaipendekeza kwako, ukatukemea kidogo tulikuwa tunavuka mipaka. lakini bado tupo kwenye Bunge lako Tukufu. Tunadhani kama Waziri Mkuu sasa atakuwa kwa wakati wake *Acting President* na huyu tunamthibitisha Bungeni, sembuse hao wanaomsaidia!

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kabisa tuanze na kulifanyia kazi hilo kwa maana ya kulipa Bunge uwezo wake wa Kikatiba kuweza kusimama katika utawala bora. Kwa maana hiyo Waziri Mkuu atathibitishwa, Mawaziri watathibitishwa, Majaji watathibitishwa na Bunge na viongozi wengine kadhaa wanaoteuliwa. Hilo ni pendekezo langu na kwa ufahamu wangu naona pendekezo hili litatusaidia sana katika kuendeleza utawala bora ambao tumeanza kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme kwamba namuunga mkono Mheshimiwa Waziri ayaweke mawazo yangu mengine katika akiba na tuyafanyie kazi. Wale ambao Mwenyezi Mungu atatujaalia uhai tuwe Bungeni au nje ya Bunge tuyaendeleze kama mabadiliko ya Katiba ambayo yatakuwa msingi wa Tanzania kuwa na amani na kuwa na mshikamano kama Taifa lenye heshima.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri na pia nitumie fursa hii kwa niaba ya wapiga kura wangu na wananchi wote wa Jimbo la Bukoba Mjini kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Musati. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu kama ilivyoelezwa kwenye *presentation* ya Mheshimiwa Waziri kwamba unatoa mapendekezo ya mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 yanayopokelewa na Serikali baada ya

mjadala wa Kitaifa kupitia Waraka wa Serikali Namba Moja wa Mwaka 1998 *(White Paper).*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yetu ya maoni ya Kambi ya Upinzani tulitoa hoja kwamba kwa kweli mabadiliko kumi na nne kwa Katiba ambayo iliandikwa mwaka 1977, ni mengi mno. Ingekuwa kwamba ni marekebisho yanayofanyika kwenye sheria mbalimbali mtu anaweza akaelewa. Hii ni wastani wa mabadiliko ya kila baada ya miaka miwili na nusu.

Mheshimiwa Spika, Katiba kama sheria mama ya nchi mimi nafikiri hoja hii ni ya msingi na inaonyesha udhaifu ambao tunao ndani ya Katiba wa kwamba Katiba inarekebishwa kufuatana na matakwa ya kikundi cha watu au watu fulani au kwa mazingira fulani kwa wakati fulani. Sasa hiyo mimi naamini haitoi sura halisi ya Katiba ya nchi na tunainyima heshima halisi ya kuitwa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nina Chama changu cha Ujima kule Bukoba kinaitwa Kibeta Development na kingine kinaitwa Mwatani Wabaki. Hivi vikundi vina katiba yake, lakini nataka kukuhakikishia kwamba ndani ya miaka zaidi ya kumi ya kuundwa vikundi hivi vya ujima katiba haijawahi kubadilishwa, lakini Katiba ya nchi ndani ya muda huu mabadiliko kumi na nne, kwa kweli hatuipi haki.

Mheshimiwa Spika, pia nitamwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu kama alivyozungumza kwamba mabadiliko haya ni kutokana na *White Paper* na vile vile yanachukua zaidi hata mawazo ya Tume ya marehemu Nyalali, lakini ningeomba tu ajaribu kulieleza Bunge kwamba ni lini hasa au ni *projections* ipi imewekwa ambayo inaweza kulieleza Bunge na Watanzania kwamba ni muda gani haya mawazo yote yaliyokusanywa kwa fedha nyingi yatakuwa yamefanyiwa kazi au kuna tatizo gani kukaa kwa wakati mmoja na kuyachekecha mambo hayo yote yakawekwa ndani ya Katiba, yenye kukataliwa yakakataliwa, yenye kukubaliwa yakakubaliwa ili tuondokane na suala la kuletewa kwa kudonoa donoa sehemu ya mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri mimi ni mjumbe ndani ya Kamati hii. Nilipata bahati ya kushiriki vikao kuwasikiliza wadau. Nilipata bahati ya kusafiri hadi Mwanza na tukakutana na baadhi ya wadau. Kama alivyozungumza Mheshimiwa Mutungirehi jana, alisema, sehemu kubwa ya binadamu ni walemavu. Mimi nataka kusema jambo nililoling'amua, Watanzania tulio wengi tuna kirusi cha kutoelewa Katiba, hatuielewi. Hata haya mabadiliko yanayofanyika ni bora tuseme tu ni mabadiliko yanayotokana na mawazo ya watu wachache sana ya sehemu ya Watanzania, hilo nitaliamini.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa pale Mwanza, mimi nilitegemea kwamba baadhi ya Watanzania kuwa wangejua programu ya Kamati ya Katiba na Sheria kwamba itawazungukia wadau mbalimbali, kumbi ambazo zilikuwa zimepangwa kukutana na wadau hawa zingefurika kiasi cha kukosa nafasi. Lakini nataka kulihakikishia Bunge hili kwa jumla kwamba, hali iliyojitokeza na ninaamini hata katika maeneo mengine ambayo wajumbe walipokwenda ni kwamba watu hawakupatikana. Watu hawana habari

kabisa na mabadiliko haya ya Katiba, wala hayawagusi, hawaoni umuhimu wa ku-*attend* kwa sababu inaonekana Katiba si yao. Hata yale maneno yaliyotumika kama alivyozungumza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwamba sisi Watanzania, mimi naamini ni maneno tu yamewekwa pale kujaribu kuwabeza Watanzania hao hao kwani Watanzania hawaielewi Katiba.

Kwa bahati nzuri siku ile baada ya kuwa imetangazwa kwa Mji mzima wa Mwanza kwa magari ya matangazo lakini tukaja kuambulia watu 35 na nasikitika wa Ukerewe hawakuja kwa sababu hawaijui Katiba. Sasa kati ya watu hao 35 waliokuja, nakumbuka tulipoanza kugawa zile copy kwanza walishangaa ahaa, kumbe rangi ya Katiba ndiyo hii, watu hawaielewi. Sasa yale yaliyomo ndani ndio usiseme, watu hawaelewi hata rangi ya Katiba. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba kwa Taifa ambalo ni serious tufike mahali tuone kitu hiki kinachoitwa Katiba kwa kweli kiwe haki ya msingi ya kufahamika kwa kila Mtanzania. Tukitaka Katiba ifahamike kwa kila Mtanzania ni vema basi tukaweka mazingira ya kulazimisha Watanzania wakaielewa na hii ni kupitia labda kwenye *syllabus ya* shule za msingi ili tuweze kuandaa umma ambao utaweza kufahamu Katiba ili yanapokuja mabadiliko ionekane kwamba watu wapo *concern.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu huo wa Katiba mimi naamini tunapokuja kuzungumzia suala la kuondoa umaskini itakuwa ni rahisi kuondoa umaskini kwa mwananchi anayejua haki zake kwa misingi ya Katiba lakini kumwacha Mtanzania asielewe Katiba ataendelea kuiona Serikali kama vile inamfadhili kila kitu ambacho inamfanyia. Ndio maana mwananchi kwa kutojua kikatiba kwamba ana haki ya kuidhibiti Serikali kupitia hata kwa wawakilishi wake kama Wabunge, ataona kwamba Mbunge kwenda kwake Bungeni yeye tu haki aliyonayo ni kumpa glasi ya pombe ya kienyeji, kupika pilau basi wamemalizana. Lakini kama angekuwa anajua kwa mujibu wa Katiba maana ya Bunge na maana ya uwakilishi wa Mbunge. mimi naamini angekuwa anazidai haki hizo kwa mujibu wa Katiba na misingi inayomlinda Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwamba mabadiliko yanayofanyika katika Ibara ya 74 kuhusu wajumbe wa tume kwamba inatolewa nafasi mbili ambazo zitapatikana kutokana na Rais kuwateua wajumbe wawili ambao ni kutokana na mapendekezo kutoka kwa kiongozi wa shughuli za Serikali ndani ya Bunge, pamoja na kiongozi wa shughuli za Kambi ya Upinzani lakini kupitia ushauri wa vyama vya Upinzani, tunalipongeza suala hili.

Wako ambao wamejaribu kuzungumza kwamba labda suala hili linaweza likaleta migogoro ndani ya tume yenyewe, mimi naamini Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza. Kwanza mimi nashukuru kwamba niliwahi kutembelea nchi ya Norway kujaribu kuangalia namna wanavyoendesha uchaguzi wao. Wenzetu kule wamefikia mahali ambapo hata tume haina kazi ni kwamba shughuli za uchaguzi zinaendeshwa na vyama vyenyewe. Vinajipanga vyenyewe vinaendesha uchaguzi na anayeshinda anatangazwa na wote wanamkubali.

Kwa hiyo mimi naamini hii ni *transformation* moja ambayo inaweza ikaongeza *transparency* katika *system* nzima ya kiuchaguzi. Kwa bahati nzuri sisi tuna-*experience*

na kule Zanzibar ambako baadhi ya wajumbe wanatokana na vyama vya siasa, vyama vya Upinzani wameingia kwenye tume.

Mimi naamini sijawahi kusia kwamba hawa watu wamepigana kule ndani ya shughuli zao, pale kitu kinachofanyika tume inafanyakazi kwa *principle,* inafanyakazi kwa jinsi walivyojipangia na kwa mujibu wa sheria na kanuni hawafanyi tu kwa jazba za vyama.

Lakini suala la *transparency,* angalau na kuchungulia nini yanayofanyika mimi ndiyo nafikiri ni suala la muhimu kwa ajili ya kuwa na uchaguzi uliyo huru na haki.

Lakini pamoja na uzuri huo wa kuweka wajumbe kwenye tume hii mimi ningeishauri Serikali kwamba, pamoja na uzuri huo lakini mfumo wa tume si vyema ukaishia kule juu peke yake kwenye tume. Shughuli za uchaguzi zinakwenda mpaka chini na huko chini ndiko kunakofanyika madudu ya ajabu hata kuliko kwenye ngazi ya juu ya Tume.

Kwa hiyo sura hii, sura ya tume ambayo tunaikubali kwamba at least iweke wajumbe kutokana na vyama ni vizuri ikaonekana sura hiyo hiyo mpaka huko chini ambako kuna tendeka shughuli za kila mara za uchaguzi. Mfano, hivi sasa wakati zoezi la uandikishaji linafanyika kwenye kata ya Mbwega huko Karagwe kuna mahali ambako watendaji tu pamoja na kwamba wanaiwakilisha tume wamekaa tu wakaamua kwamba nafunga zoezi la uandikishaji kabla ya tarehe yenyewe kwa mantiki kwamba kiwango alichokuwa amepewa cha uandikishaji kimekamilika ile *percentage* imekamilika. Kwa hiyo akafunga vituo, sasa mimi naamini kama kungekuwa na wawakilishi mbalimbali mimi nafikiri matendo kama hayo yangeweza kurekebishwa, na pia itakuwa namna moja wapo ya kuwadhibiti hata hao watendaji walioko huko.

Katika uchaguzi uliyofanyika wa vijiji, vitongoji na mitaa tume-*experience* mambo ya ajabu, kwamba hata mapingamizi niliyokuwa najaribu kuchukua sasa kuna mapingamizi watu wamewekewa pingamizi 7280 kutogombea, na sehemu moja wapo niliwahi kwenda kuangalia sababu zilizosababisha watu kuwekewa pingamizi. Sehemu moja watu wamezuiwa kugombea eti kwa sababu wakati unatoka kwenye chama cha CCM kwenda chama cha Upinzani hukuaga, sasa sijui huyu mtu hizo kariri alizitoa wapi. Mahali pengine mtu wakati anaoa hakulipa mahari eti alikiuka maadili na misingi ya mila za kidesturi za ki-Afrika nalo ni pingamizi. Hii nafikiri haya mambo yasingeweza kujitokeza kama kwa kweli hawa watu hawaachiwi mazingira ya kuendesha uchaguzi wanavyotaka.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwamba katika Ibara ndogo ya kwanza ya Ibara ya 107 (a) inayofutwa na kuandikwa upya, inasema kwamba mamlaka yenye kauli ya mwisho ya kutoa haki itakuwa ni Mahakama ya Tanzania, Mahakama ya Zanzibar na hakutakuwepo na chombo chochote kile zaidi ya vyombo hivi.

Mheshimiwa Spika, lakini kifungu cha 125 sehemu ya saba kinazungumzia Mahakama maalum ya katiba ya Jamhuri ya Muungano. Mimi ningeomba wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*sum up* atueleze hii Mahakama ya maalum ya katiba ya Jamhuri ya Muungano inawekwa upande gani, na ina nguvu zipi kama haijapewa kuwa chombo vile vile cha kutoa haki kama chombo cha mwisho.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha hayo machache, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipatia nafasi hii ninayo machache na mimi naomba nichangie katika muswada huu. Mimi nimewasikiliza sana wenzangu na inanipa woga kidogo kila anayezungumza ukisikiliza sana anavutia upande wake. Sasa tukianza kufanya katiba ni kwa manufaa ya watu hatutakwenda mahali. Tutaleta matatizo na ndiyo ugomvi uliyoko katika nchi za ki-Afrika kila mtu anataka yeye aongoze yeye anufaike na hii ni hatari sana katika maendeleo na kuzingatia katiba.

Mimi naamini katiba iwe na lengo la kutazama manufaa ya taifa tuachane na vyama hivi, imani za dini zote hizi ni za watu binafsi hazina sababu ya kuzifuata sana tulenge kujenga taifa letu. Sasa mimi nadhani Azimio la Arusha lilikuwa ni zuri sana, hata kama watu watasema lilikuwa la CCM lakini lile lilionyesha msingi wa watu wote tufanye nini kwa maendeleo yetu wote bila kujali chama chochote, na hiyo ndiyo nia tunayoitazamia. Lakini tukianza kusema sijui hili litakuwa kinyume cha chama cha Upinzani hatuendi mahali tutaleta mikoroganyo na kutokufanikisha maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, hili suala la Rais kuchagua Wabunge kumi sasa sijui kama Rais huyu tunayempa kibali hicho kikatiba tumlazimishe, tunamwamini huyu? Yeye ndiye mwenye mamlaka yote ndiye atakaye angalia hakuna sababu ya kumuingilia, akiona wanawake wote kumi watafaa kwa kuweka mafanikio ya maendeleo yale anayoyataka awaweke, akiona wanaume wanafaa kumi wote kwa lengo lake awaweke. Hatuna sababu ya kuuliza, hivi tunamuweka Rais atakuwa ni Rais wa kusukumwa sukumwa tu kuambiwa, na hili mimi ningeomba hata Bunge lisiwe na sababu ya kumuingilia. Katiba isiandikwe hiyo tumemkubali achague watu kumi wamsaidie kufanikisha maendeleo ya uongozi wake basi. *(Makofi)*

Hii ya mtu kumfuatafuata ni dalili yakumvuruga na kuleta matatizo bure tu katika nchi, tuondoe hilo.

**MBUNGE FULANI:** Wawe wanaume.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Hata wakiwa wanaume kumi kama watafanya kwa maendeleo ya nchi ni sawa tu, hakuna wa kunung‘unika, wakiwa wanawake sawa mbona Sweden tumewaona wanawake ndiyo wengi katika uongozi wa namna hiyo na wanaume kule hawanung‘uniki pamoja na kwamba ndiyo wanaoshughulika kupika na kuosha watoto hawanung‘uniki, wanakubaliana tu, na sisi tuwe katika hali hiyo. Hii ya kunung‘unika nung‘uka mtu kwa manufaa yake ni kuvuruga utaratibu wa maisha ya watu wetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni la dini, dini tuachane na masuala haya, haya ni imani ya mtu peke yake wala hakuna haja ya mtu hata kusema sijui iwe sheria ya kufuata imani ya dini hiyo ni mtu mwenyewe na Mungu wake. Hilo lina nafasi yake huko peponi ambako siasa hii tuliyonayo haitakuwa na nafasi. Tuachie siasa katika dunia ya siasa, Serikali ione tu mambo haya ya dini yanakwenda kwa amani na utulivu, suala la dini hili hakuna sababu. Mimi naunga mkono lisiwepo kabisa, tukifanya hivi ndiyo hii iliyofanya hata Warusi wakafanya mapinduzi. Maana makanisa na imani za dini ndizo zilikuwa zinamiliki uchumi wa nchi nenda Urusi hata Mimbali zote ni dhahabu tupu.

Kwa nini uweke mimbali zinakuwa dhahabu tupu uchumi wa nchi unaingizwa Kanisani, haliwezekani hayo wangoje peponi huko kama wanataka kwenda kufanya hayo wakafanye huko peponi siyo duniani hapa, hapa ni petu kisiasa tukubaliane kwa manufaa ya kuishi sisi hapa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba tena hili la Mkurugenzi nadhani Mkurugenzi wa mashtaka tusimpe nguvu ya kutokuhojiwa na mtu, nadhani Bunge lipate nafasi ya kumhoji. Kwa sababu mashitaka kama anaweza kufuta ndiyo manung'uniko ya watu, kama anaweza kufuta makosa ya jinai anayoona yeye lazima Bunge liulize au atoe taarifa Bungeni tuelewane. Kwa sababu sisi ndiyo tunawatu kule sasa watu kule kama hawaelewi tutaweka mtu mmoja hapa mwenye nguvu ya kudhalalisha watu wengine, na binadamu ni binadamu huwezi ukasema atakuwa kama malaika hata malaika nao wana matatizo yao. *(Kicheko)*

Hii nadhani mimi nisingeona kuwa ni tatizo kwa kweli katika hali hii ya nafasi za akina mama, hii jinsia ya akina mama mimi ninakubaliana na mmoja aliyeshauri kwamba labda tuongeze tu ni kweli kwamba ni wengi na haki hiyo wanayo. Tukubaliane kila jimbo liwe na jumuiya, washindane kule nao waje huku hata tukija nusu kwa nusu Bungeni wanaume na wanawake sawa sawa ndiyo tutapambana vizuri katika kujadiliana mambo. Lakini na yeye akija huku awajibike kule alikotoka. Hii ya kuwekeana tu umaalum, viti maalum anabaki hana nguvu kule, tuwape nguvu nao watokane kule kule washindane kule waje kwa ushindi huo na wakajibu hoja na kusimamia maendeleo kule vijijini.

Lakini utaratibu huu wa viti maalum hawana nguvu ya kusimamia maendeleo kule ndiyo maana hata ofisi hawana kule kwenye majimbo. Sasa watafuatwa wapi, tuwape nafasi wawe na nguvu na wao wabanwe kule wasukumwe ndipo wafanye maendeleo ya kuangalia tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Spika, hili la mwisho mimi nadhani hii tume ya uchaguzi yote hii ni lengo la kutaka kuainisha kwamba nani anapata au nani anafanya nini, kwa nini tuwe na mashaka ya namna hii. Hivi tukiweka wale watu basi tuweke watu wa dini ambao hawamo katika siasa wawekeni watu wa dini wao waamue wasimamie kwa misingi ya imani ya Mungu, tuweke hao. Lakini tukiweka hapo uweke *CUF,* uweke CCM, uweke CHADEMA, vurugu. Mimi ninaomba kwa kweli hili tuliangalie sana, hakuna sababu hii ni katiba ya maendeleo yetu ilenge katika kusukuma kuondokana na umaskini na iondokane na maradhi na kuondoa ujinga hilo ndilo liwe msingi wetu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa mimi nina omba sana Waziri atakapokuwa anajibu ni vizuri mambo mengine yale ambayo yamesemewa hapa ambayo yanaonekana hayana msingi ajaribu kabisa kuyagusia na kutuhakikishia kuwa haya kwa kweli hayatakuwepo. Kuliko hali inavyoonekana sasa na katiba ni vema ichukue muda mrefu wa kujadialiana siyo kwa muda mfupi kama huu. Sasa tukipitisha hapa uchaguzi ukifika vurugu tutafanya nini naomba haya yazingatiwe na tuweze kwenda sawa sawa na tuondokane na matatizo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi na nina unga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii. Lakini kwanza kabisa naomba nitoe salamu za heri ya mwaka mpya kwako mwenyewe na Wabunge wenzangu humu ndani nawatakia kila mema na mafanikio mema katika mwaka huu wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, pia niungane na wenzangu kwa kutoa pole kwa wenzetu ambao wamefiwa nasema pole sana na Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Ameni.

Mheshimiwa Spika, mimi ninalo moja tu lakini kwanza naomba nianzie pale ambapo panahusisha uchaguzi wa Serikali za Mtaa wa mwaka jana. Niliyoyaona wakati ule yamenitia wasiwasi kidogo hasa idadi ya watu ambao walifika kwenye uchaguzi. Asubuhi na mapema siku ya uchaguzi wa Serikali za Mtaa kwa mkoa wa Dar es Salaam hasa jimbo langu wengi walikuja kujiorodhesha ili baadaye wapige kura zao. Lakini kama tunavyofahamu ilikuwa ni siku ya Jumapili, mimi mwenyewe nilifika kwenye kituo hicho saa moja asubuhi, nikawa nimeandikishwa ilipofika saa sita lakini sikupiga kura mpaka saa kumi, na bahati mbaya kwa maana hiyo sikuweza kwenda kuabudu Mungu wangu.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachotaka kusema ni kwamba ninaomba Serikali kwa vile tunasema ni Serikali ambayo haina dini basi ibadilishe siku ya uchaguzi wa Serikali za Mtaa na Serikali kuu, uchaguzi mkuu. Badiliko ninaloliomba ni kwamba pale katiba inaposema kwamba uchaguzi mkuu utafanyika Jumapili ya mwisho wa mwezi Oktoba basi isomeke Jumatano ya mwisho wa mwezi Oktoba maana yangu ni kwamba tuwaachie wenye dini waende kwenye dini zao kwa uhuru pasipo kuingiliwa na mambo ya uchaguzi. Naambiwa kwamba hili linaweza kubadilishwa, kwa hiyo kama nilivyosema kwa kweli kabisa ombi langu ni hilo dogo tu katika muswada mzima huu. Hicho kipengele cha siku ya uchaguzi mkuu kibadilishwe. Tukumbuke kwamba kuna siku ya 1825 kwa maana ya kipindi cha miaka mitano na tunaiomba Serikali badala ya kufanya uchaguzi siku za *weekend* ifanye uchaguzi siku ya kazi na iwe ni siku maalum kwa ajili ya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba siku hiyo iwe ni siku ya Jumatano. Nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niwe miongoni mwa wachangiaji wa mada iliyo mbele yetu kwa mchana huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nami nitangulie kuungana na wenzangu kwa kuwapa pole wenzetu waliyofiwa pamoja na pole kwa familia ya Marehemu Mbunge mwenzetu ambaye ametangulia mbele ya haki. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu familia hizi azipe subira wakati huu wa kukabiliana na hilo jambo la lazima lakini ni gumu sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo sasa nielekee moja kwa moja kwenye mada zilizokuwepo mbele yetu. Kwanza nami nitangulie pia kumpongeza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba pamoja na watendaji wao kwa kazi hii kubwa ngumu na muhimu kwa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nikianzia na Ibara ile ya 19 ambayo inazungumzia uhuru wa kuabudu. Niseme kwamba kwa mabadiliko haya ambayo tuliyapokea jana naipongeza Serikali kwa kuzingatia uzito wa jambo hili ambalo pengine lingetufikisha mahali siyo pazuri sana kwa maslahi ya taifa letu. Suala ambalo linagusa imani za watu ni suala zito na ni nyeti sana. Kwa hivyo nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa busara aliyoitumia kwa mabadiliko haya. Kilivyokuwa kikisomeka mwanza na kinavyosomeka sasa hivi ninaamini tofauti ni kubwa sana iliyopo, ile Ibara ya 19 ambapo mabadiliko yamefanyika kati ya Ibara ndogo ya 2 na ya 3 ambayo inavyosomeka sasa kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni uhuru na jambo la hiari ya mtu binafsi. Shughuli na utekelezaji wa jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi. Ibara ndogo ya 3 inasomeka hifadhi ya haki zilizotajwa katika Ibara hii itakuwa chini ya taratibu zinazowekwa na sheria ambazo ni muhimu katika jamii ya demokrasia kwa ajili ya usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umoja wa Kitaifa.

Hatua hii mimi nasema ni nzuri kwa maoni yangu, na itatusaidia kubakia na ule umoja wa Kitaifa pia kuepukana na dhana ambazo pengine zingeliweza kututawala katika mfumo ambao ulikuwepo mwanzo kwa hivyo hatua hii hatuna budi kuipongeza na tuseme kwamba itatusaidia na pengine kazi tuliyonayo sasa kuelewesha wenzetu na Watanzania wengine ambao wanatuangalia na kutusikia hivi sasa kuona kwamba lile tatizo ambalo tulikuwa tukilidhania kuwepo au tukilishuku katika yale mapendekezo ya mwanzo sasa natumahi litakuwa limeondoka.

Mheshimiwa Spika, nikiondoka hapo niende katika Ibara 37 ya katiba ambayo inafanyiwa mabadiliko ambapo kwa utaratibu wa sasa unaopendekezwa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa na nafasi ya utendaji wa kazi za Rais anapokuwa hayupo. Utaratibu huu kwa hali ya sasa hivi tunaweza tukasema kwa mujibu wa katiba ilivyo twende nao hivyo sawa. Lakini tu mimi niseme kwamba utaratibu huu si mzuri kwa kuzingatia umoja wa Kitaifa na tukizingatia kwamba tunazungumzia taifa la Jamhuri ya Muungano kwa nini nasema hivyo.

Mheshimiwa Spika, ki-ujumla wengi katika kuzungumzia wamelizungumzia hili tatizo moja kwa moja kwa nafasi ya Waziri Mkuu kushika nafasi ya Rais. Lakini tatizo hili halikuanzia hapa limeanzia pale tulipofanya mabadiliko ya kumuondoa Rais wa Zanzibar kuwa ni Makamu wa Rais katika Jamhuri ya Muungano, tatizo tumelianzia pale. Pamoja na mabadiliko tuliyoyafanya kusema iwapo Rais anatoka upande mmoja *let say* kama ilivyo sasa hivi Makamu anatoka upande wa pili, kwa maana hiyo ametokea Zanzibar.

Lakini katika hali ya sasa hivi muundo wetu kiutawala Makamu wa Rais hana nafasi yoyote ndani ya Serikali ya Zanzibar. Kwa maana hiyo cheni yetu kiutendaji hapa imekatika, na vile vile Rais wa Zanzibar hana mamlaka ya kiutendaji ndani ya Serikali ya Jamhuri ya muungano. Kwa hivyo ile dhana nzima ya kuwa na Jamhuri ya Muungano katika ngazi ya juu hapa pana hitilafu, kwa hivyo hilo ningelipendekeza tulione na nimshauri Mheshimiwa Waziri ni vyema wakalifanyia kazi ili kuondoa tatizo hilo.

Kwa sababu katika hali ya sasa hivi ya baraza la Mawaziri itakapokuwa sasa Waziri Mkuu ndiyo anayeendesha baraza la Mawaziri maana yake nini, limekaa baraza la Mawaziri, Rais wa Zanzibar awahi kuingia mwanzo na akae amsubiri aje Mwenyekiti, Waziri Mkuu akiingia naye ainuke, na akitaka kuzungumza anyanyue mkono aombe ruhusa.

Wakati yeye yule ni kiongozi wa juu upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano, Waziri Mkuu katika mtiririko wa uongozi sina hakika nafasi yake ya ngapi. Kwa hivyo hii ni hitilafu ni hitilafu kwa kuwa inasawazishika tutafute njia ya kuisawazisha kuhakikisha umoja wetu wa Kitaifa hauathiriki, na hicho ndicho kinacholalamikiwa hapa. Kwa hivyo ningeishauri Serikali ikalifanyia kazi tatizo hili kuona kwa kiwango gani lina athiri umoja wetu wa Kitaifa pia linatoa nafasi ya malalamiko katika muundo huu tuliyonayo hapa.

Mheshimiwa Spika, labda nifafanue tena tunapokuwa na Sherehe zetu za Kitaifa nimejaribu mara nyingi ninapohudhuria kuona viongozi anayekuja mwisho kabisa mgeni rasmi Rais wa Jamhuri ya Muungano kabla yake anafuata Makamu wa Rais na kabla ya Makamu wa Rais hufuata Rais wa Zanzibar, sasa ile ni *protocol* inayotumika kwenye Sherehe. *Protocol* ndani ya Serikali kiutendaji ikoje kwenye katiba nadhani hiyo haina ufafanuzi kwa hivyo ni vyema tukapata ufafanuzi mzuri sana kiutendaji kuondoa matatizo madogo madogo lakini hili si dogo lakini madogo madogo na makubwa tukapata ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Spika, niende kunako baraza la taifa la ushauri hichi kipengele kimeondolewa na kwa hatua hii ya kukiondoa pia niseme naipongeza hatua hii ya Serikali ambapo imeondoa suala ambalo lilionesha kutokukubalika na Wabunge waliyo wengi. Kwa sababu katika hali ya mwanzo kabisa kitu tulichokuwa tukijiuliza hivi washauri waliokuwepo sasa hivi wamepatikanaje, hata kukawa na ulazima wa kuwemo kwenye katiba.

Kwa hiyo, kuondoa hili suala na mimi kwa upande wangu naliunga mkono na naamini iliyotumika ni busara ya hali juu.

Kwa hivyo, pia si vema kwa Serikali kauli ya Mheshimiwa Waziri alisema kwamba analiondoa kama sikosei kitu kama kwa muda kwa kulitafakari tena. Si vema kulirejesha tena, tukirejesha turejeshe chombo cha utendaji siyo cha ushauri na mimi ningeshauri chombo tutakachokirejesha cha utendaji ninajua kwamba kulikwa kuna mapendekezo ambayo Serikali iliyapokea.

Mapendekezo haya yalikuwa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ushauri kwamba kwa nini tusifikirie kuunda chombo ambacho tukakipa jukumu moja kwa moja la kutanzua matatizo yetu ya Muungano. Kwa hivyo ni vizuri tukafikiria tuunde chombo cha kikatiba kuipa nafasi hiyo ya utendaji badala ya suala la ushauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, huu ulikuwa ni ushauri wangu katika kipengele hicho ambacho kimepelekea kuondoa baraza hili la ushauri. Niende katika maeneo mengine ambayo pia pamoja na kwamba yapo nje ya hii katiba *I mean* nje ya haya mapendekezo yaliyopo lakini pia ningeliomba kwa upande wa Serikali ikafikiria ni wa kuwafanyia kazi ambayo bado nina amini ni matatizo makubwa ili tutakapofikia hatua ya kuwa na mabadiliko mengine mambo haya nayo yakazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 147 ya katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazungumzia suala la Majeshi, Ibara ile ya 147 Ibara ndogo ya kwanza inazungumzia mamlaka yale yakuweka Majeshi katika Tanzania. *(Makofi)*

Naomba kukariri "Ni marufuku kwa mtu yoyote au shirika lolote au kikundi chochote cha watu isipokuwa Serikali kuunda au kuweka Jeshi au kuweka Tanzania Jeshi la aina yoyote". Na Ibara ndogo ya 3 inafafanua madhumuni ya Ibara hii "Mwanajeshi" maana yake ni askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa. Sasa huku juu kimetajwa Serikali ndiyo yenye mamlaka hayo. Kwa mujibu wa Katibu yetu Serikali inajumuisha na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha vikosi. Kuna vikosi KMKM, JKU, Chuo cha Mafunzo lakini kwa bahati mbaya sana hivyo havikutajwa kama ni Majeshi. Kwa maana hiyo kuwepo kwake kama vinaelea na kiasi ninachofahamu kikosi cha KMKM kilishiriki katika vita vya Kagera.

Sasa hii ni hitilafu juu ya uhalali wa kuwepo kwao ndani ya Katiba hii. Kwa hivyo hiyo ni upungufu na ningeliomba Mheshimiwa waziri akaliangalia kwa kina suala hili, akalipatia ufumbuzi hasa tukizingatia vikosi hivi mimi ninaamini vina mchango mkubwa sana na vinahitajika sana kwa maendeleo ya Zanzibar. Kwa hivyo hilo pia ningelikuomba Mheshimiwa Waziri ukaliangalia na kulifanyia kazi kwa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende sehemu nyingine katika Ibara ya 4 ya Katiba hii ile nyongeza kule mwisho katika mambo ya Muungano. Mambo ya Muungano yako 22 mimi ningeliomba tuyataje kwa usahihi wake.

Nadhani kwa hesabu yangu mimi nikihesabu napata 32, hapa tunaambiwa 22. Nasema hivyo kwa sababu nikija katika kile kipengele kidogo nambari 8 kinasema mikopo na biashara ya nje, kukopa kitu kingine na biashara kitu kingine.

Kwa hivyo pendekezo langu tuziweke nambari kwa usahihi ili kila kimoja kisomeke kwa nafasi yake na kwa peke yake. Hali hiyo pia unaikuta katika kipengele cha mfano cha 11. Kinasomeka bandari hicho ni kitu kimoja, mambo yanayohusiana na usafiri wa anga hicho ni kitu kingine, Posta ni kitu kingine, simu ni kitu kingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili leo niweze kuchangia.

Naomba pia kwa awali kabisa kutoa rambirambi kutokana na vifo vilivyotokea kwa kuanza kifo cha Mheshimiwa Frank Mussati ambaye alikuwa jirani yetu katika bench hili tulilokaa na tunakumbuka siku ya mwisho alisimama na akatuaga hapa alitangulia kuondoka kabla ya kikao cha Bunge hakijamalizika tukapeana mkono. Mungu aiweke mahali pema roho yake peponi. *(Amin)*

Naomba pia kutoa rambirambi kwa wale wote ambao wamefiwa kwa kuwapoteza wazazi wao na kupoteza wake zao. Na hivyo hivyo tunasema Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema peponi roho za hao wote. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia mabadiliko ya Katiba na tunapozungumzia mabadiliko ya Katiba tunasema mabadiliko yoyote katika Katiba yoyote ya nchi ni muhimu na ni ya lazima. Ni ya lazima kwa sababu kwanza yanalinda haki ya demokrasia ya wananchi lakini vile vile yanasaidia sana katika utekelezaji wa maendeleo ya wananchi. Kwa hiyo kubadilisha maeneo mbalimbali ya Katiba ni jambo la lazima ili kuweza kuitikia hayo niliyoyasema. Kwa mfano katika kulinda demokrasia kumekuwa na mabadiliko ya kutoka katika mfumo wa chama kimoja kwenda katika mfumo wa vyama vingi, hiyo ni demokrasia. Nchi inapotoka katika mfumo huo wa chama kimoja kwenda kwenye mfumo wa vyama vingi maana yake lazima Katiba ya nchi hiyo ifanyiwe marekebisho ili kuweza kuruhusu kuwepo kwa zaidi ya chama kimoja cha siasa. Lakini vile vile unapokuwa na vyama vingi vya siasa lazima vile vile Katiba irekebishwe ili kuelekeza muundo na utekelezaji wa vyama hivi vipya ambavyo vinakuwa zaidi ya chama kimoja katika nchi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kufanya mabadiliko katika Katiba ni utaratibu wa kawaida kabisa katika dunia nzima ambapo nchi zinaendeshwa kwa mfumo wa vyama vya siasa. Aidha iwe chama kimoja cha siasa au mfumo vyama vingi vya

siasa. Kutokana na hilo tunasema kwamba basi si vyema watu wakaanza kubezabeza utaratibu huu na kusema kwamba Katiba inawekwa viraka, huku ni kubeza utaratibu ambao ndio mfumo wa utekelezaji dunia nzima. Kwa hiyo lazima tukubaliane na hilo kwa sababu linazingatia demokrasia na linazingatia maendeleo ya watu na ni lazima kuyatekeleza kwa sababu Katiba ndiyo chombo kikuu na mwongozo unaoashiria utekelezaji na kuashiria utungaji wa sheria kuendesha nchi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia kidogo haya mamlaka ya Rais katika uteuzi wa Waheshimiwa Wabunge. Jambo hili linatokana na Katiba na ni moja kati ya sharti linalotokana na Katiba. Sasa kwa sababu ni sharti linalotokana na Katiba si vyema kuongeza sharti juu ya sharti yaani sasa unasema Mheshimiwa Rais katika uteuzi wake lazima ateue idadi kadhaa ya hao watu kuwa wanawake. Huku ni kuongeza sharti ndani sharti linalotokana na Katiba. Sasa tusiipindishe pindishe na kuichezea chezea Katiba. Tunaamini Mheshimiwa Rais ni mtu mwenye busara sana na sisi ni mashahidi wa busara za Mheshimiwa Rais katika kipindi cha miaka 10 iliyopita awamu mbili za uongozi wake amefanya kazi ya uteuzi wa Wabunge kwa nafasi aliyopewa na Katiba. Wote tunafahamu kwamba amefanya kazi ambayo watu wengine wengi imewashangaza hasa pale alipofikia hatua hata ya kuteua Wabunge kutoka katika Vyama vya Upinzani, hata vyama vyenyewe vya Upinzani havikujua kwamba Rais angeweza kufanya kazi hiyo. Lakini ametumia busara na hekima na akafanya uteuzi na kuwashirikisha viongozi kutoka katika Vyama vya Upinzani. Kwa hiyo, busara hiyo ni busara ambayo kwa kweli tumwachie Mheshimiwa Rais atatumia nafasi hiyo vizuri na sisi tutaridhika kwa busara atakazokuwa anazitumia.

Mheshimiwa Spika, jambo muhimu ambalo ni vizuri tukaliangalia katika Katiba vile vile ni kutambua nguvu na uwezo wa vijana. Tumepata fundisho kubwa sana hivi karibuni katika chaguzi zilizopita za Serikali za Vijiji na Vitongoji. Tumeona jinsi vijana walivyoshiriki kinyume kabisa na ilivyokuwa katika miaka iliyopita. Sasa hivi vijana wamekuwa na mwamko mkubwa na wameshiriki vizuri sana na kule katika jimbo la Muheza vijana wamechukua nafasi ya uongozi katika Serikali za Vijiji na Vitongoji katika umri mdogo ambao wengi hatukuwa tumetegemea. Hilo ni fundisho kwamba sasa lazima tuwashirikishe vijana katika kuongoza nchi. Ile dhana tuliyokuwa nayo ya kuamini na fikra za kusema kwamba vijana ni viongozi wa Taifa la kesho nadhani ipo haja ya kuifikiria mara mbili tuibadilishe. Vijana lazima pia washiriki katika uongozi wa Taifa la leo. Ni nafasi yao. Kwa hiyo, tuangalie namna tutakavyoweza tunapozungumza kuongeza idadi ya ushiriki wa akinamama, wanawake basi tuangalie vile vile namna ya kuweka na kuongeza uwezo na ushiriki wa vijana katika uongozi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuangalia sasa jinsi tutakavyoweza kuainisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa sababu tusipofanya hivyo inawezekana tukagongana katika masuala mbalimbali. Kwa mfano masuala ya uraia na makazi. Tusipokuwa waangalifu katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania suala hilo hilo linaweza likawa linazungumzwa tofauti na Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa lipi litakaloanza kutekelezwa kwa sababu bado tunaamini kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litatekelezwa lipi

kikatiba hili lililopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au lile lililopo katika Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, upo umuhimu sana katika kuainisha Katiba hizi. Lakini umuhimu huo pia unaongezeka kwa sababu sasa hivi tunaelekea katika Muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na lengo ni kufikia Shirikisho la Afrika ya Mashariki na maana yake ni kwamba kutakuwa na Katiba itakayokuwa inaainisha Katiba ya Serikali zinazoshiriki katika Umoja wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kenya, Uganda na Tanzania. Ni muhimu lazima Katiba hizi ziainishwe ili baadhi ya mambo yawe ya msingi kuwezesha sheria zitakazowezesha kutumika ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kenya na Uganda vinginevyo tutakuwa na migongano tu.

Sasa kama tunaelekea huko na tutaweza kuwa na Katiba itakayokuwa inaelekeza mwelekeo wa Shirikisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki wenzetu wa Zanzibar watakuwa na Katiba ngapi sasa. Watakuwa na Katiba ya kwao ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, watakuwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sasa tunaelekea katika Shirikisho, watakuwa vile vile na Katiba nyingine ya Shirikisho ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sasa hapa kweli tutakosa kuwa na migongano. Kwa kweli lazima tuchukue hatua ya kuainisha hizi Katiba, tuwe *serious* katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika kuzungumza hili upo mfano mmoja ambao lazima niuzungumze hapa ni mfano ambao unatokana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikaiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuahirisha kuleta Bungeni pendekezo la kurekebisha Sheria ya Utafutaji wa Mafuta. Sasa umepita mwaka tangu ombi hilo litolewe na sheria hiyo haibadilishwi sasa hili linatokana na nini. Je, kuna tatizo kikatiba, je, kikatiba hilo kweli ni sahihi kwamba tunaweza tukazuia mabadiliko ya sheria iliyopitishwa na sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania isifanyiwe marekebisho kutokana na ombi kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivi Katiba ndivyo inavyosema inaruhusu?

Sasa katika hatua za namna hii lazima tufikirie hatua za uchumi wa Tanzania. Utafutaji wa mafuta ni suala la kiuchumi la Tanzania. Tunapozungumzia dhana na fikra za kusema kwamba mahali fulani kuna mafuta nilizungumza wakati nikichangia mwaka uliopita katika kikao cha Bajeti kwamba hizo sio dhana sahihi huwezi ukasema mahali fulani kuna mafuta bila wataalamu kufanya utafiti pale na kudhibitisha kwamba mafuta yapo pale. Sasa hilo linaleta migongano isiyokuwa na sababu. Wenzetu wa Shell wanataka kufanya kazi hiyo ili wadhibitishe kama kweli mafuta yapo au hayapo, lakini wapo watu wanasema yapo yapo umefanya lini utafiti wewe na bila kazi hiyo kufanyika huwezi kuwa na jibu hilo kwamba mafuta yapo.

Sheria hii lazima ibadilishwe kwa sababu wakati ilipoundwa kwa mara ya kwanza sheria hii ilikuwa haitoi nafasi ya kuruhusu kufanya *exploration* katika kina kirefu cha bahari *(deep sea).* Sasa teknolojia inatoa mwanya huo na wenzetu wa Nigeria, Cameroun wamepata mafuta katika *deep sea* na sisi tunataka kutafuta mafuta katika *deep sea* hatuwezi kupata bila kufanya utafiti. Kwa hiyo, lazima urekebishe sheria ili uweze kufanya *exploration* kwenye *deep sea,* mgongano unaotoka wapi katika Katiba zetu hizi

mbili ya Serikali ya Mapinduzi na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika suala hili la kiuchumi ambalo tunasema ni la lazima. Nchi hii haiwezi kuendelea kama hatutakuwa tunaangalia mambo haya kiuchumi yanayoweza kusaidia nchi ikabadilika.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa muda wangu unakaribia kwisha na haya ndiyo muhimu nilikuwa nikitaka kutoa kama mchango wangu. Naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS S. NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hoja ya Mabadiliko ya Katiba.

Nianze kwa kutoa rambirambi zangu kwa kifo cha mpendwa wetu Mheshimiwa Frank Mussati ambaye aliyekuwa Mbunge wa Kasulu na nitoe pole kwa wote waliofiwa wazazi au mke, Mungu aziweke mahali pema peponi roho zao. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, mwanzo kabisa niseme hivi katika kuendelea kimoja kitakachodumu ni mabadiliko. Haitawezekana kabisa mabadiliko yaondoke katika kuendelea. Chama cha Mapinduzi kingefanya uzembe wa kutokukubali na kuleta mabadiliko wakati kwa wakati na pekee kwenye Katiba *bench* ya Wapinzani haingekuwemo humu Bungeni. Mimi nilitarajia wao watakuwa wa kwanza kuona umuhimu kwamba leo tunaingia badiliko la 14.

Mheshimiwa Spika, lakini jingine ni kosa sana kwa nchi kama Tanzania kiongozi anatoa mfano eti wa Denmark, Sweden, Norway ni binadamu kujaribu kujilinganisha na kitu ambacho hana uwiano nacho, hakuna mahali popote tunapowiana na nchi hizo kijamii, kiuchumi, kifalsafa sasa ya kazi gani kujilinganisha na kitu ambacho wewe huna uhusiano nacho ni kwamba huna nia. Kwa hivi mimi niwaombe Wabunge wenzangu tujenge fikra zetu kwa Tanzania na kama tunataka kujilinganisha tujilinganishe tulio sawa nao Kenya, Uganda, Zambia, Malawi na kadhalika ya kazi gani unakwenda Marekani wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hoja tuliyonayo yako maeneo machache ambayo napenda kuongelea. Mwanzo kabisa napenda kuongelea sehemu ya ukurasa wa 5 mahali ambapo kuna neno Katiba au sera na baadaye kuna itikadi au falsafa. Ni vizuri Waziri labda inawezekana wenzetu waliofanya kazi ya kuandika hati hii walikuwa wanawaza na kupanga Kiingereza lakini wanaandika Kiswahili. Sasa kama anapotoa majumuisho Waziri hatatupa tafsiri sahihi na bayana hapa tutaingia kwenye tatizo la kupambana kitafsiri, kimaneno na kimpangilio. Nashauri atupe tafsiri ya maneno manne hayo ili wote tufahamu tunapitisha sheria yenye tofauti zifuatazo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda niende kwenye sehemu ambayo inaongelea viti 75 au asilimia 30 ya akinamama katika Bunge hili. Ni jambo jema na wala sidhani yuko ambaye ana mashaka kwa nini akinamama wengi wawepo hapa. Yapo mambo mengi katika jamii ambayo mawazo ya akinamama ni sehemu ya kwanza katika kujihakikishia uelewa ulio muafaka. Tatizo ni utaratibu. Inawezekana hivi sasa tumetumia njia ya asilimia. Njia yoyote ambayo jamii inaamua ni nzuri tu ili mradi

ndivyo tulivyoamua. Lakini linalofuata sasa ni lazima ije sheria itakayotusaidia hiyo asilimia 30 ifike Bungeni kwa njia ambazo zenye uwiano ulio bayana na zenye haki miongoni mwa akinamama wenyewe. Ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vinginevyo inaanza kuleta usumbufu ndani ya vyama mbalimbali. Nirudie tena sina tatizo kubwa sana na Chama cha Mapinduzi. Mwaka 2000 walitoa nafasi kwa kila Mkoa baadaye zilizobaki wakatafuta njia nyingine ya kugawanya kwa hivi karibu kila Mkoa wa Tanzania una Mbunge wa Viti Maalum. Lakini wote tuko hapa vyama vingine kwa sababu mbalimbali vilishindwa vika-*end pitch.* Pengine mtu mmoja ana-*end pitch* fulani na fulani atakuwa au aliyechangia sana gharama ya uchaguzi anasema mimi nitaingiza huyu na huyu. Sasa katika jamii tusijenge vitu ambavyo vinatoa nafasi ya utendaji usiofaa ili kiwe ni jambo la kimaendeleo ni jambo lenye busara kwa Watanzania ni lazima Mheshimiwa Waziri ahakikishe baada ya kupitisha kipengele hiki cha Katiba anaweka sheria itakayosimamia kwa vyama vyote iwe CCM, CHADEMA, na kadhalika atii utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiko kipengele ambacho mimi kwa kweli sikipendi wala hakina sababu kuwepo kwa namna nyingine kinaonyesha hali fulani ambayo wala haipo. Rais amepewa kwa sheria ya Bunge hili, kwa makubaliano hapa ndani kwa sababu tulizojadili vizuri awe na viti 10 vya Wabunge hapa Bungeni. Leo tumegeuka tunataka kumwambia lazima watano wawe wanawake na watano wawe wanaume. Hii hoja imewezekana kwa jumla mtu akaiona ni nzuri lakini si hoja nzuri tunayoongelea ni *Kaiser* wa Tanzania. Watanzania wanamchagua Rais wao kwa misingi bora kwa misingi ya mtu anayefaa kushika wadhifa huo ni lazima aheshimiwa, ni lazima akubalike na ni lazima apewe nafasi ya kujaza nafasi 10 bila kuwa na kipengele kinachomwingilia tena. Hatujapata hali hiyo leo hapa Bungeni tunaye mtu wa Upinzani ameteuliwa na Rais. Tena aliteua mtu ambaye ana uwezo mkubwa ndani ya Upinzani sio ovyo ovyo tu hapana. Hii ni busara ya Rais. Tuheshimu busara hiyo na tuendelee kuenzi busara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nashauri sehemu hii ya kumpa masharti Rais iondolewe kwa sababu haitujengei lolote jipya zaidi ya kufanya upindishaji wa mambo tuliyoamua na baadaye tunafikia kuona kinyume cha tulivyoamua. Ni vizuri sana Rais katika nchi ndiyo dira ya umoja wa taifa kama ni masuala ya siasa kila mtu ana itikadi yake na ana chama chake, kama ni masuala ya dini kila mtu ana dini yake ana imani yake. Mahali tunapokutana Watanzania wa dini mbalimbali wa vyama mbalimbali ni kwa Rais wa nchi pale ndipo wote tunakutana. Kwa hivi huyu mtu asifikishwe mahali kupewa masharti yasiyo na msingi wowote ule. Nimwombe sana Waziri alizingatie hili kwa makini sana. Naomba atumie hekima aliyotumia katika kuondoa kipengele cha kuweka Baraza la Ushauri. Hekima hiyo hiyo aitumie katika vipengele vingine ambavyo vinaleta mahudhui yasiyo na malengo yenye maana ndani ya Katiba yetu.

Mheshimiwa Spika, liko eneo ambalo pia nalo kidogo linasikitisha sana. Wenzetu wa Upinzani wamekuwa msitari wa mbele siku zote kutaka tuwe na Tume Huru ya Uchaguzi. Mimi siku zote niliona ni watu makini kabisa, hakuna sababu ya kuwa na Tume inayoegemea upande mmoja wala hakuna sababu ya kuwa na Tume isiyo huru.

Sasa leo wananishangaza wanasifu kuingizwa watu ambao ni wa CCM, CHADEMA na kadhalika sasa suala la Tume Huru tena limekwisha au tafsiri ya Tume Huru ndiyo hiyo? Sasa tunakwenda wapi? Si hapa Serikali nayo inaanza kunishangaza. Ni vizuri sana mkasikiliza watu wanayoyasema.

Lakini si vizuri ukasikiliza yatakayokuua. Kwa vyotevyote vile atakayesema ni busara kuwa na watu wa vyama na hapa inasema hao wawili waendelee na vyama vyao kwani vyama viko viwili? Mbona vyama viko kumi na plus. Basi waingizwe mmoja mmoja kila chama ili wakapambane pale.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli busara ya Tume Huru tunaiondoa tunaweka Tume ya Vyama . Mimi ninachoogopa ni pale ambapo wa chama kimoja ataumbua jambo mle ndani kuwa kura nyingine zimechomwa maana akisema zimefichwa ataambiwa onyesha ziko wapi, walipoficha. Akasema zimechomwa. Ni majivu majivu utaonyesha majivu mangapi. Atasema jambo ambalo namna ya kulidhibiti na kuhakiki ni vigumu

**MBUNGE FULANI:** Sema !!!!!

**MHE. THOMAS S. NYIMBO:** Na huyu ni Mjumbe wa Tume hii ataliweka Taifa katika hali ngumu ya ubishani na ubishani ambao yumkini utatupelekea kwenye kuondokana na amani yetu. Itatupelekea kwenye kuondokana na Umoja wetu.

Mheshimiwa Spika, mimi sioni Mheshimiwa Waziri alikuwa anataka kupata nini, alikuwa anawaweka mimi najua anataka mambo ya kujifurahisha kisiasa.

Sasa katika kusimamia nchi kubwa kama Tanzania tukianza kufurahishana tumetafuta matatizo. Utafurahisha wangapi. Mtu huyo huyo anasema nataka Tume Huru na mtu huyo huyo anasema ni vizuri sana kuwa na Vyama vya Siasa ndani ya Tume sasa utafuata lipi?

**MBUNGE FULANI:** *Shame!!!!!*

**MHE. THOMAS S. NYIMBO:** *It is a problem.* Kwa hivi mimi nawaomba sana suala la hawa wanasiasa mnaowapeleka kwenye Tume msiwapeleke. Ondoa wanakwenda kuzalisha fujo, wanakwenda kuleta matatizo ambayo hayapo. Hivi leo huko vijijini huwa tunakaa mnahesabu kura juu ya meza wote mnaona bado anaamka mmoja kuwa mimi siamini halafu tunamwambia hili ni suala la taratibu, sheria na kanuni sio suala la imani ondoka hapa na imani yako. Sasa tunaingia mahali kwenye imani ya vyama, itikadi ya vyama ndani ya Tume ya Uchaguzi. Mimi nionye tu ni vizuri tukaelewana leo kuliko fujo itakayokuja. Hakuna mantiki yoyote ya kujidai tunajenga Tume Huru yenye vyama ndani ni huru katika lipi? Uhuru huu alioleta Nyerere au uhuru gani mnaongelea? Kama ni uhuru wa Wakoloni wote tupo huru hapa hakuna anayetawaliwa na Wakoloni hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Kengele ya pili.

**MHE. THOMAS S. NYIMBO:** Ile ya kwanza ilikosewa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi niombe sana mambo makubwa yafuatayo matatu. Moja..........

**SPIKA:** Ulituambia mwenyewe kwamba ustaarabu ni kufuata sheria na kanuni. Sasa muda wako umekwisha. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. THOMAS S. NYIMBO:** Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia mabadiliko haya ya 14 ya Katiba.
Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Frank Mussati na nimwombe Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kutukumbusha kwamba tuendelee kufuata taratibu na sheria katika Bunge hili. Kwa bahati nzuri mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati hii ya Sheria Katiba na Utawala. Katika ma-group ambayo tulipangwa kwenda kukutana na wadau mimi nilibahatika kwenda Zanzibar. Kule Zanzibar tulibahatika kukutana na wadau mbalimbali wakiwemo Viongozi wa Serikali, Makatibu Wakuu, Viongozi wa Dini na wananchi kwa ujumla. Lakini nilipata wasiwasi na kuona kwamba Zanzibar bado kuna tatizo. Nilipata wasiwasi baada ya kukutana na Viongozi Wakuu wa Nchi na kusema kwamba wao wanashangaa kuona mabadiliko haya yameletwa yakiwa yao ya kwao ambayo walitoa mapendekezo hawayaoni na hawakuona umuhimu wa Muswada huu kwa nini haukuhusisha yale ambayo yalikuwa wamependekeza wao. Hivyo ningeomba Serikali zote mbili zikae chini kwa pamoja watafakari hayo wanayoyalalamikia ya Serikali ya Muungano na waone ni vipi wanaweza kutatua kama kweli tunataka Muungano wenye nguvu basi tuyapitie haya yote na tuweze kuwa na usikivu wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye Muswada napenda kuipongeza Serikali kwa kuongeza asilimia ya viti vya wanawake ndani ya Bunge. Hii inaonyesha kwamba Serikali inaona kazi zinazofanywa na wanawake na ndiyo maana ikaamua kuongeza idadi hiyo. *(Makofi)*

Wako baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wameonyesha wasiwasi lakini mimi ningependa tu kuwaondolea wasiwasi na kuwaambia kwamba hatutaendelea kung’ang’ania wanavyoviita viti vya upendeleo au Viti Maalum na sisi tuko kwenye kujifunza na tutaingia kwenye Majimbo. Ilishasemekana hapa Bungeni tunapopita kwenye Majimbo wanakuwa na wasiwasi wengine waliomba tuwe tunatoa taarifa kwao. Sasa nashindwa kuelewa kama mnalalamika tunapata viti asilimia 30 Bungeni huku tukipita kwenye Majimbo mnatulalamikia tuombe ruhusa kwenu sasa uzoefu sijui tutaupata wapi.? *(Makofi/Kicheko)*

Lakini mimi nawashukuru Wabunge wa CHADEMA ninapokuwa kwenye Majimbo yao wanafurahi na sidhani kama watalalamika nitakapochukua jimbo mojawapo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo hiyo ndiyo maana CHADEMA wametangaza kuwa mgombea wa Urais au mgombea mwenza lazima mmojawapo awe mwanamke. Nitashukuru ikiwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya mwisho ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa ndani ya Bunge hili, alisikitika kwa kuona Upinzani kwamba hauna nguvu. Mimi nilitegemea ile rasimu ya kwanza iliyotoka ikiwa na vile viti 28 kwa kupitia ile hotuba ya Mheshimiwa Rais tungetumia nafasi hiyo ili kuongeza nguvu ya Upinzani ndani ya Bunge. Ninasema hivyo kwa sababu watu ndani ya Upinzani ambao wana mawazo mazuri na wanao uwezo mzuri wa kuishauri Serikali, lakini kwa sababu moja au nyingine wameshinda kuingia ndani ya Bunge. Tungetumia viti vile basi nao wangepata nafasi ya kuja katika Bunge na kutoa mawazo yao. Lakini kinyume na hapo nafasi zile hazikurudi tena kwenye rasimu hii ya pili na sielewi ni kwa sababu gani Serikali, iliondoa viti vile tungeiomba Serikali itueleze ni sababu zipi au ni wasiwasi gani ambao waliona au waliupata. Mimi naamini sipigii debe aidha Wenyeviti wa Vyama au Makatibu Wakuu au Viongozi Wakuu wa Vyama vya Upinzani kwa kuwa kwa bahati nzuri mimi chama changu viongozi wote wakuu wapo ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo, mimi natetea vile vyama vingine ambavyo havina uwakilishi lakini wako watu wenye uwezo ambao wangeweza kuja kutoa mawazo yao ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye viti kumi vya Rais, ningemuomba Rais wetu atakayekuja mwaka 2005 viti hivi aweze kuvitumia vizuri. tusigawe viti hivi kama zawadi tuwape wale wote ambao tunaona wana sifa ambao Rais anaweza kuwatumia katika Bunge hili. Wasipewe tu watu kwa sababu either amehama chama fulani akarudi chama fulani na wakaweza kuwakosoa au kuwatupia tuhuma vyama vile vingine. Tunaomba tutumie nafasi hizi vizuri. *(Makofi)*

Lile la kwamba wanawake wawe watano, wanaume watano, mimi naona suala hili tumwachie Mheshimiwa Rais, atakavyoona inafaa ateue kwa sababu mimi naamini kabisa kwamba akina mama wako wengi na ni wasomi na wana uwezo, tusijiwekee limit maana yake anaweza akachagua akina wote sasa sijui tutafanyaje atakapochagua akina mama wote. Hilo naona Rais, atakayechaguliwa atakuwa na busara na ataitumia busara hiyo kuchagua wale watu ambao anaona wanafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu tume huru ya uchaguzi, mimi naipongeza Serikali kwa kuwapa angalau nafasi moja wapinzani awe mwakili ndani ya Tume hiyo. Huu ni mwanzo mzuri na tunategemea siku zinavyokwenda mambo mengi yanaweza kubadilika. Ingawa wengine wamepinga na kusema kwamba tunaingiza siasa kwenye Tume na kwamba haiwezekani kukutanisha wanasiasa wawili ndani ya Tume. Lakini mimi naomba kuuliza mbona muafaka uliwezekana kati ya CCM na *CUF* kwa nini hili lishindikane wanasiasa kuwa kwenye Tume? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kukutana na wadau tulibahatika kukutana na watu wa Baraza la Kiswahili na hili ningeiomba Serikali ilichukue hili ili iweze kuingiza katika Katiba kwamba Kiswahili ni lugha ya Taifa ya Tanzania ili iweze kutambulikana duniani pote kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na hayo tu na kwa kuwa nilikuwa mjumbe wa Kamati hii nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu ya mabadiliko ya 14 ya Katiba yetu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Mwanasheria Mkuu wetu wa Serikali na wasaidizi wao kwa kazi kubwa sana ambayo wameifanya katika kuandaa na kutuletea mapendekezo yaliyo mbele yetu. Pia Mheshimiwa Waziri, nisije nikasahau wananchi wanakushukuru sana kwa kutuwezesha kupata Mahakama ya kisasa ya Wilaya tunasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijachangia chochote na mimi kwa niaba ya wananchi Kongwa nitoe salama za rambirambi kwa wananchi wa Kasulu kwa kuondokewa na Mbunge wao ndugu yetu Marehemu Frank Mussati ambaye tulikuwa tukikaa naye hapa, alikuwa ni rafiki yangu wa karibu sana. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, naanza kuunga mkono mabadiliko haya ya 14 kwa kutoa pongezi zifuatazo; baadhi ya wachangiaji wamesema mjadala huu haukuwa umezunguka sana kwa wananchi wetu. Lakini Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hapa alituambia kwamba kinachoendelea mabadiliko haya ya 14 ni matokeo ya mjadala wa kitaifa ulioitwa white paper no. 1 wa mwaka 1998. Hii ni awamu ya pili ya utekelezaji wa yanayotokana na mjadala huo wa kitaifa. Sasa wanaposema baadhi yetu kwamba mambo haya hayakushirikisha nashindwa kidogo kujua wanafikiri nini kwa sababu kutoka 1998 mambo haya yameshirikisha mpaka leo na sisi wengine tunashiriki kama hivi mnavyotusikia. Kwa hiyo, yameshirikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napongeza pia kwa zoezi hili kuondoa zile *(clobber clauses)* kuondoa maneno bila ya kuathiri sheria za nchi kwenye Katiba kwa sababu haya yalikuwa yanathoofisha Katiba kwa kuzipa kipaumbele baadhi ya sheria nyingine za nchi wakati Katiba ndiyo inatoa haki za msingi za mwananchi wa Tanzania. Kwa hiyo, napongeza sana jambo hili.

Pia napongeza mabadiliko tuliyoletea yanayoondoa neno Idara ya Mahakama kwa nguzo nzima ya dola kuitwa idara kwa kweli ilikuwa inafifisha uwezo wake.

Kwa hiyo, naunga mkono mapendekezo yaliyoletwa kwamba sasa itaitwa Mahakama ya Tanzania na siyo Idara ya Mahakama. Jambo hili ni jema linaipa hii nguzo hadhi yake inayostahili na mapendekezo mengine ambayo yameletwa ya nafasi za Majaji, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani kwa kweli ni katika kuimarisha suala zima la Mahakama ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napongeza pia Mheshimiwa Waziri kwa kutokuleta lile suala la *proportion representation* kwa nafasi za Wabunge. Kwa hiyo, hilo wala sitalisemea napongeza kabisa kutolileta. *(Makofi)*

Pia niungane na wenzangu kuhusu kutokukubaliana na suala la baraza la ushauri kwa kuwa limeshasema sina haja ya kulirudia. Migongano yake ni mikubwa sana japo Mheshimiwa Waziri, ametuambia limeahirishwa lakini naiomba kama walivyosema wenzangu liahirishwe moja kwa moja hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja kwenye ushauri wangu ibara ya 19 imesema hapa kwamba mamlaka ya nchi haitakuwa na dini yoyote. Mimi nasema sawa.

Lakini katika mabadiliko yajayo napendekeza Katiba imtambue na kumtaja Mungu na ianzie hapo. Japo tuko Watanzania wenye dini mbalimbali na madhehebu mbalimbali lakini wengi wao asilimia kubwa tunaamini jambo moja la msingi kwamba Mungu yupo. Hata tunapokuja kwenye Bunge lako kila siku asubuhi huwa unaanza kwa Dua. Dua hili huwa lina sentensi mbili zinazoanza ewe Mwenyezi Mungu.

Kwa hiyo, tunakubaliana kimsingi kabisa katika taifa hili. Suala la mwenyezi Mungu kuwepo ni wazi ndiyo la *majority,* kwa hiyo mabadiliko yajayo ya 15 ningependekeza sana kwamba jambo hili lipatiwe nafasi, Katiba yetu imtambue Mungu kwamba yupo. *(Makofi)*

Ibara ya 66 (e) kinazungumzia habari ya Rais kuteua Wabunge na watano kati yao kuwa akina mama. Wenzangu wamelisemea na mimi nipitie hapo hapo kusema kwamba ibakie vile vile Wabunge 10 tusimuweke Rais wetu katika majaribu ya kumlazimisha kuteua aina fulani ya jinsia ya watu katika nafasi zake 10 kama ilivyoelezwa kwa sababu yako makundi mengine ya jamii ambayo nayo yangelipenda kuwakilisha nafasi hizi hizi chache sana 10 na hasa kundi la vijana, tunaposema vijana tuna maana wa kike na wa kiume ni kundi muhimu sana linalokuja juu ambalo lazima lipewe nafasi huko tunaelekea.

Kwa hiyo, tumwachie nafasi zake 10 tuunge mkono zile asilimia 30 na hata hizo nafasi za akina tunaomba, akina mama ni pamoja na vijana wa kike kwa hiyo, nao hao waangaliwe kinamna yake ili nao wawakilishwe katika Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo tuliyoletewa ni mengi ni mazuri. Lakini katika yale ambayo hayakuja moja ambalo ningelipenda katika mabadiliko yajayo ya mwendelezo wa mchakato huu ni kuchambuliwa vema zaidi suala la Muungano. Siku nyingi tungependa kusimama na kuzungumza yale tunayofikiri na kuyaona kuhusu Muungano kwa sasa, Mwenyezi Mungu akijalia tutazungumza huko mbele ya safari.

Lakini nisemee tu kwamba mwelekeo sasa wa vijana wa nchi hii ni shirikisho la Afrika ya Mashariki na wenzetu wanatabiri huenda likawa mwaka 2013 ambalo ni miaka 8 tu ijayo. Huko ndiyo tunakoelekea kukubwa zaidi, kupana zaidi. Kwa hiyo, mjadala

wetu uelekee huko badala ya kujifunga kamba tunarudi nyuma kila dakika sasa twende kule kupana zaidi kwenye soko kubwa zaidi la ajira, kwenye biashara kubwa zaidi, kwenye suala la Afrika ya Mashariki. Tuna tumaini kwenye mabadiliko ya 15 tutajielekeza huko. *(Makofi)*

Pia kwenye mabadiliko yajayo suala la mgombea huru liwekwe vizuri. Mimi nalisema hili kwa sababu kwa masikio yangu mwenyewe niliwahi kusikia wakati ule Mwalimu Nyerere aliliunga mkono kabisa jambo hili. Ukikaa ukifikiri sana unaona ni jambo jema tu labda linahitaji muda kidogo kuliweka sawa sawa. Kwa kuwa sisi tunasema lazima mawazo ya Mwalimu tuyaenzi na moja ya mawazo yake lilikuwa ni hili nadhani alisemea Mbeya na alianisha vizuri sana. Basi ningependekeza Mheshimiwa Waziri, kwa kikao kijacho kitakachokuja kuzungumza mabadiliko ya 15 hebu hili nalo litazamwe kwa undani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakubaliana kama walivyosema wenzangu wananchi wengi wa Tanzania bado hawaielewi vizuri Katiba yao, vitabu hivi vya Katiba ni vichache sana nchini kwetu. Ningelipendekeza sana Serikali ijitahidi baada ya mabadiliko haya vichapishwe vitabu vingi sana, visambazwe kwa Watanzania wengi iwezekanavyo katika maofisi ya Serikali, mashuleni, vyuoni na mahali pengine ili Watanzania wapate kujua nini kipo ili waweze kushiriki vizuri zaidi katika mabadiliko yanayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho niunge mkono wazo la nafasi ya Bunge, kama mwakilishi wa wananchi kushiriki katika kuthibitisha viongozi wakuu wa taasisi zetu au wa vyombo vyetu vya dola. Baadhi ya *appointments* kubwa kubwa Serikalini kadri itavyoonekana busara, *appointments* za Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa, Bunge lipate nafasi yake ya kuthibitisha wateuliwa hao.

Hii itawapa nguvu ya ofisi hizo watakazokuwa wakifanyia kazi. Lakini pia natoa nafasi kama anateuliwa mtu ambaye kwa namna moja au nyingine si vizuri akathibitishwa basi Bunge, likapata nafasi ya kuzuia uteuzi wake kwa nia na manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hayo naomba kusema nashukuru na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunakaribia mwisho wa kipindi cha asubuhi, lakini kwa kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge, ambao wako kwenye orodha ya mwanzo kwa kipindi cha mchana ni bora niwataje ili wasije wakaitwa kabla hawajaingia Bungeni. Wabunge hao ni Mheshimiwa Shellukindo, Mheshimiwa Kiwanga, Mheshimiwa Maghembe na Mheshimiwa Mwanri. Hao ndiyo Waheshimiwa Wabunge wanne wa kwanza katika kipindi cha jioni. Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.55 mchana Bunge lilifungwa Mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo hoja hii ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya 14 katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa mchango wangu, napenda kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wamefiwa na wapendwa wao na vilevile kuwapa pole familia na wananchi wa Jimbo la Kasulu Mashariki waliofiwa na Mbunge wao Mheshimiwa Frank Mussati. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu wote mahali pema Peponi na awape subra wafiwa wote. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa ni mdogo tu katika mambo machache. Katika mabadiliko ya Katiba ninavyoona mimi ni kwamba iwe na malengo ya kuimarisha demokrasia ndani ya mfumo wa Bunge na kuweka wazi zaidi suala la uwajibikaji na udhibiti au *checks and balances.* Haya yakizingatiwa, kwa kweli tutakuwa tumeifanya kazi ambayo inatakiwa. Mabadiliko haya ninavyoona mimi yanagusa karibu mihimili yote mitatu; Bunge lenyewe, Mahakama pamoja na Utawala au Serikali. Kuhusu Bunge, nadhani kuna jambo ambalo mara nyingi linasahauliwa, halijitokezi sana nalo ni hili la madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa ninukuu Ibara ya 63(2) inayosema, “Bunge ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba”. Kwa maana nyingine, mimi ninavyoiona, Bunge ndiyo Baraza Kuu la Ushauri kwa Rais na Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapoingiza vitu vingine, tunafifisha madaraka ya Bunge. Nadhani hili limekuwa wazi. Bunge ndilo linamshauri Rais pamoja na vyombo vyote juu ya utekelezaji wa shughuli za Serikali. Kwa hiyo, kuunda chombo kingine zaidi ya Bunge, mimi ningelisema ni sawasawa na kwenda kinyume cha matakwa ya Sheria na Katiba. Tunakwenda nje na kinyume na Katiba ambayo imetoa madaraka kwa Bunge kutoa ushauri na kusimamia Serikali.

Kwa hiyo, mimi napenda kuishauri Serikali kabisa kwamba hili suala la Baraza la Taifa la Ushauri wala siyo kuahirisha, ni kuliacha kabisa na Bunge lisihusishwe kushughulikia Baraza hilo. Hilo Baraza liwe ni la Rais na utawala wake anavyoona, atatumia watu mbalimbali kumpa ushauri. Lakini nje ya matakwa ya Katiba. Kisiwe kitu kinachoingizwa kwenye Katiba kwa sababu kwenye Katiba nchi imeshapewa Bunge ambalo ni chombo cha kusimamia Serikali chini ya Rais pamoja na vyombo vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la uwajibikaji wakati mwingine tunalikwepakwepa. Nadhani ni vizuri tukawa wazi kabisa kwamba katika kutoa

madaraka kwa chombo chochote, basi suala la uwajibikaji liwekwe wazi na kama kuna ukiukwaji kwa wawajibikaji basi, vyombo ambavyo vimepewa kazi ya kudhibiti *checks and balances* vifanye kazi yake. Hapa nataka kuipongeza sana Serikali kwa kuchambua upya nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na naipongeza kwa kufikiria kumpa msaidizi ambaye anatambulika kikatiba ili wakati wote kama hayupo, basi kazi za Mwanasheria Mkuu ziweze kutekelezwa ipasavyo. Vilevile kitu ambacho kimenifurahisha ni kuainisha sifa za Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyeti sana katika Taifa. Kwa hiyo, si vizuri zikaachwa tu wazi, wakaingia watu na sifa ambazo hatuna uhakika nazo. Kwa hiyo sifa hizi zikiingia kama zilivyowekwa katika Katiba, kukaa katika muda uliopangwa katika eneo la Sheria, basi una uhakika kwamba nafasi hiyo itakuwa na uwajibikaji mzuri na kama kuna dosari basi zinaweza kurekebishwa kwa mujibu wa Katiba.

Hili suala la *checks and balances* naona tunalizungumzia juu juu tu. Sijapata Kiswahili chake kinachoelezea vizuri, udhibiti wa vyombo na viongozi ambao wanapewa madaraka. Asubuhi nilimsikiliza mwenzangu Mheshimiwa Ndugai akizungumza kitu ambacho nadhani ni wachache ambao wamekigusia. Hiki cha kuthibitisha *confirmation or ratification* ya Viongozi na Maofisa ambao wametajwa katika Katiba. Maofisa hawa ni wa nguzo nyingine. Sasa Bunge kuwathibitisha kwa kweli ndiyo udhibiti wenyewe, ndiyo *checks and balances* zenyewe hizo kuliko kuacha tu mambo yanakwenda hivyo hivyo, bila udhibiti.

Kwa hiyo, naungana na mwenzangu Mheshimiwa Ndugai kwamba hili suala kwa kweli liwekwe kwenye Katiba na nakumbusha kidogo kwamba mwaka 1998 Bunge lilimtuma Mheshimiwa Diria wakati huo alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mashirika ya Umma kwenda kuchunguza na kuangalia wenzetu wa nchi ya Zambia wanavyotekeleza hii kazi ya Bunge ya kusimamia Serikali *(the over sight role of Parliament*) ya udhibiti wa Serikali. Zambia wameweka utaratibu kwamba wale Maofisa wote waliotajwa katika Katiba wathibitishwe na Bunge na kazi hiyo imetolewa kwa Kamati zake kutegemeana na *portfolio.*

Kwa hiyo, kama ni Kamati inayohusu mambo ya Sheria, basi masuala ya Majaji yanakwenda huko na yanachambuliwa halafu Bunge linaletewa mapendekezo na Kamati. Kwa upande wetu ni kwamba, nafasi ambazo hapana budi Bunge lithibitishe kwa sababu wanaozishika wanafanya kazi za Umma na kunapotokea dosari Bunge linalaumiwa kuwa pengine Sheria hazikufanya kazi vizuri. Kwa mfano, Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano ambayo mimi kwa bahati nzuri ni Mwenyekiti, ningeomba Bunge lingepewa nafasi ya kuthibitisha *(confirmation)*. Hiyo ndiyo *checks and balances.* Tunazungumzia Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume au Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Tume ya Uchaguzi. Kuna hoja hapa zinaelezwa kwamba Tume ya Uchaguzi ingekuwa huru, ifanye nini?

Nadhani kama ile kazi ya udhibiti *(checks and balances)* ingefanyika, Bunge lingekwishasema kama kuna dosari na ingekwishajulikana na ikarekebishwa. Majaji ni

watu wazito sana katika nchi. Mwanasheria Mkuu wa Serikali tuko naye hapa, athibitishwe na Bunge, akae hapa, tuone uhakika zile sifa zote hakuna, mahali ambapo panaleta dosari pamoja na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka.

Asubuhi mwenzangu Mheshimiwa Njelu Kasaka, alizungumzia Maofisa wengine katika utendaji, aachiwe Rais. Rais ndiye ambaye tunashughulika naye, wale walio katika nguzo yake, *Executive* aachiwe mwenyewe jinsi atakavyowapanga. Lakini hawa wengine kwenye vyombo ambavyo vinatoka au vinaundwa kwa Sheria maalum za Bunge, hao ndio ambao ninazungumzia. Kwa hiyo, hakuna kazi kubwa, wengi na siyo wengi wanaoteuliwa katika nyadhifa hizi. Mfano wa hizi Tume ni katika miaka mitano, kama wanabadilisha hapo sawasawa kutakuwa na haja ya kuwathibitisha. Hili tusilionee aibu.

Sasa hivi tuna Mheshimiwa Mkapa ni mtu mwadilifu sana. Lakini Ma-Rais wengine wanaokuja tunawafahamu sisi tuwaachie tu-*blank cheques* wafanye wanavyotaka, lakini tutakuja kushtukia hapa vyombo vingine vimekaa, mtu, mke wake, watoto wake na wajukuu humo ndani! Ndiyo! Ni Rais na Katiba imempa madaraka hayo ya kuteua na huwezi kumwuliza lolote. Kwa hiyo, ni vizuri tuwasaidie ili sisi tusifike mahali hapo.

Nazungumza kwamba sasa hivi tuna Rais mwadilifu, lakini huko tunakokwenda ataweza kutokea Rais yeyote yule na Katiba haisemi kuwa kuna kuthibitisha. Utakuwa unafanya kosa kama utasema hakufanya vizuri, utolewe ushauri. Wakati mtu unapothibitisha na si mapambano, ni kumwangalia mtu, kama umeleta mtu mzuri, atapita; lakini kama mtu una wasiwasi naye, utasema hapa huyo hatufai!

Kuhusu Ibara ya nane ya Muswada inayohusu kufanya kazi za Rais kama Rais hayupo, nadhani Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kwamba kuwe na mgawanyo mzuri wa madaraka. *Executive* wapangane wenyewe, chombo kingine kisiingie humo. Kwa mfano, mwenzangu mmoja alizungumza hapa kwamba ikiwa Jaji Mkuu atahusika katika jopo na limemhukumu mtu kifo na Rais anatakiwa athibitishe kifo hicho, halafu Jaji Mkuu anakwenda kufanya kazi ya Rais, anakaimu; ataicheleweshа adhabu hiyo, ataisogeza kando atasema nilihusika. Lakini kwa nini tufike hapo? Kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hoja yake, ni kwamba, Rais atapanga kazi zake ili wakati wote Makamu awepo.

Kwa hiyo, hata kukaimu kwa Waziri Mkuu kutakuwa ni kwa nadra tu. Kwa hiyo, nadhani tuwaache hao kwenye mhimili huo wajipange wenyewe. Kama Rais hayupo, kazi zake zifanywe na Makamu; kama Makamu hayupo, Waziri Mkuu atakaimu. Huku kwenye Bunge tujipange wenyewe na kama Spika hayupo Naibu Spika, afanye kazi zake. Hizo kazi za Naibu Spika tutampaje Waziri? Tumpe Waziri mmoja awe Naibu Spika na kama Spika na Naibu Spika hawapo! Tutaendeleza matatizo kwenye uwajibikaji. Kwa hiyo, tuwe makini katika hili. Siku zilizopita ilikuwa rahisi kwa kuwa tulikuwa kwenye Chama kimoja. Sasa tuko katika Vyama vingi.

**MHE. CHIFU ABDALLAH FUNDIKIRA:** *Deputy Speaker, point of information Sir.*

***DEPUTY SPEAKER:*** *Yes Sir!*

**MHE. CHIFU ABDALLAH FUNDIKIRA:** *I think we should understand quite clearly that Office of the President has two functions. He functions as the Head of the Government and also as the Head of State. Things like confirming, appointments*

***DEPUTY SPEAKER:*** *Honourable Shellukindo, can you sit down please*!

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** *Okay!*

**MHE. CHIFU ABDALLAH FUNDIKIRA:** *Things like confirming or appointing Judges, appointing other senior positions of high rank in the country are done by the President as the Head of State. And therefore, I don't think that all the members of his Government, such as the Prime Minister or anybody else can perform those functions. Those are reserved only to the Head of State.*

***DEPUTY SPEAKER:*** *Honourable Fundikira, could you kindly ask the Speaker time to speak, so that you could give us those wonderful ideas, instead of interrupting another Member of Parliament in the form of point of information! Yes! Go ahead Sir. (Applause)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Muda wangu umeingiliwa, nadhani utaufidia. Mimi namheshimu sana Mzee Fundikira. Lakini mimi katika Afrika ni mmoja wa wataalam wa *Public Policy Management Specialists.* Kwa hiyo, naelewa sana hiyo kwamba sio kila mtu anaweza kukaimu. Nilikuwa nasema wacha watu katika *Executive* wapangane wenyewe. Rais kama hayupo, yupo Makamu, Makamu naye kama hayupo, yupo Waziri Mkuu. Huendi tena chini huko kwa sababu Katiba nayo ndivyo inavyotaka.

Halafu nimesema watu wa *Executive* msiwaguse, mwache Rais ateue watu wake, Wakuu wa Majeshi, ateue anavyotaka yeye kwa kuzingatia utaalam wao. Nazungumzia hawa. Tume hizi za Uchaguzi, zina watu ambao wanatoka nje ya Serikali. Serikalini ni *professional consideration* ndiyo hutumika huku. Huku kwingine kuna p*olitical, influences* na vitu kama hivyo. Nafasi hizo ndiyo zinaletwa hapa *(political appointees).* Hao wengi karibu ni *political appointees.*

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ana sehemu zote mbili, *professional and political considerations.* Kwa sababu Rais anayekuja inategemea Chama chake atamteua ambaye anatambuliwa na Chama chake. Hawezi kumteua mtu mwingine hivi hivi tu. Nilitaka hili niliweke wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya saba ya Muswada kuna sehemu pale inayosema kwamba kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali yake.

Mheshimiwa Njelu Kasaka aliizungumzia hii. Nilitaka niseme hivi, ingeongezwa mali aliyopata kihalali. Kuna suala hili la *money laundering* ambalo tumelizungumzia sana hapa. Mtu anaweza kumiliki fedha kwa njia ambazo si halali. Sasa Sheria ikikaa tu hivi, hifadhi ya hizo fedha zake au mali zake nadhani alizozipata kwa njia halali ili uache nafasi kwamba ikijulikana hakuzipata kwa njia halali, basi hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. ABU TOWEGALE KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nishukuru kwa kupewa nafasi hii ili nichangie kwenye zoezi hili muhimu ambalo linahusu uhai wa Taifa letu. Katiba ni sura ya nchi na umuhimu wake ni kuwa nchi ni lazima ibakie kama nchi, iwe na sehemu yake maalum katika dunia bila kuhatarisha kumezwa na wengine.

Mabadiliko katika Katiba yameainishwa karibuni 24, badiliko Na.3 kidogo linanitia wasiwasi ambalo lionazungumzia mtu awe na uhuru wa fikra zake. Nadhani tuzungumzie fikra zake kwa mujibu wa Sheria ama sivyo tuna hatari ya kuwaunda akina Hitler, akina Musolin ambao hatimaye kesho na keshokutwa kama tusipoweza kuwafuatilia na kuwadhibiti watatuletea majanga katika nchi.

Pia kuna badiliko Na.5 linazungumzia juu ya Vyama vya Siasa kutoandikishwa. Kwangu ingawaje hilo wazo ni sahihi, nadhani hiyo tu ni kurejea Katiba na kuzungumzia mabadiliko tuliyoyaleta mwaka 1992 kuhusu Vyama Vingi. Lakini mantiki yenyewe ni kuhakikisha Chama kinaleta mabadiliko kwa manufaa ya nchi, basi kule kutokuandikishwa lazima pia kutazame kwa muda wa nyuma kwa Vyama vingine ambavyo huenda vimeandikishwa. Lakini kwa taratibu za badiliko hili Na.5 pia ni hatari. Kwa hiyo siyo kusema isiandikishe, bali pia iwekwe na kufutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina matatizo ya mabadiliko Na.8, Na.9 mpaka Na.11. Naamini kabisa ni nia njema ya kuhakikisha kuwa tuna Serikali. Mihimili yetu mitatu yote kila moja ina kazi yake. Sheria tutatunga Wabunge, Serikali itaendesha kazi yake na Mahakama itatenda haki. Kwa hiyo, kwenye taratibu za kuweka Serikali, iweze kutekeleza mambo yake kwa mabadiliko haya manane, sina utata nao. Ila tu kama nilivyosema hapo awali kwamba Taifa ni Taifa. Naamini kabisa utulivu, amani tulioupata katika nchi hii, tumeleta kwa misingi ya Katiba hii. Kwa hiyo, tusibadilishe kwa sababu tu mabadiliko yanatokea duniani. Utandawazi ni mzuri, lakini utandawazi ni hatari.

Tanzania lazima ibakie kama Tanzania na picha yake ya Tanzania ni Tanzania Bara, Tanzania Visiwani. Tumeungana kwa kutambua kabisa kuwa kuna kitu kilichotutenganisha hapo awali ya kutufanya sisi tuwe siyo wa karibu. Tumeungana, tumeunga Tanzania; Tanzania Bara, Tanzania Visiwani. Hilo ni la umuhimu. Kwa mantiki hiyo, ninazungumzia suala lote zima la kujaribu kufikiria nani kapata, nani kakosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mjumbe mmoja alivyozungumza hapa asubuhi juu ya utafiti wa mafuta, faida ya mafuta inaweza kuwa ni moja tu. Lakini faida yetu kubwa sisi ni Muungano. Sidhani kama tukitathmini mafanikio ya Muungano kwa nchi zote mbili kwa sehemu zote mbili za Muungano tutapata hesabu ambayo itakidhi faida kama ni *balance sheet* itakayokubali pande zote mbili. Cha muhimu kwetu sisi ni Muungano wenyewe. Sisi ni kitu kimoja, lakini kuna kitu kilitutenganisha hapo awali, kimetuunganisha tena. Kwa hiyo sidhani kama ni kitu cha busara kubadilisha chochote kile ambacho kinatusababisha sisi kutokuwa wamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mnyamwezi Unguja, kuna Mhehe Unguja, kuna Mhehe Bara, kuna Mtumbatu Pemba, lakini wote ni Taifa moja ambalo lazima libakie kuwa Taifa imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, utandawazi ni hatari. Sina sheria ya kusema kuwa mimi nahitaji Rais, nahitaji mihimili mitatu ya Serikali ambayo kesho na kesho kutwa itabakia kuonekana kama ni Tanzania. Pale ambapo tutaweza kuamua kama ni vita, basi Rais kwa madaraka tutakayompa aweze kuamua. Baraza la Ushauri linalopendekezwa kwenye mabadiliko, sina utata nalo. Lakini ninaamini kabisa tunahitaji Rais ambaye atatumia hilo Baraza kwa madaraka tuliyompa kupitia kura zetu tulizomchagua. Tumemchagua Rais, tumempa *mandate* ya kuendesha nchi na lazima awe na *mandate* na nguvu za kutosha ili kulibakiza Taifa hili liwe Tanzania tuliyoiunda Kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sina la zaidi la kuongezea, ila tu ninaamini kabisa Watendaji, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na Kamati ya Katiba imefanya kazi nzuri sana. Haya mabadiliko yameandikwa kwa lugha rahisi na ya kuweza kufuatiliwa. Kwa hiyo, ninaamini itatuongoza siyo kufanya mabadiliko tu, bali kuleta Tanzania ambayo itakuwa *consolidated* isije ikaleta *dis integration* hapa mwisho. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Muswada huu. Awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo langu la Siha, kutoa pole sana kwa wananchi wa Kasulu Mashariki kwa kuondokewa na rafiki yetu mpendwa.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kama mnavyojua, Mheshimiwa Frank Mussati tulikuwa tunakaa naye hapa. Alikuwa rafiki yetu wa karibu sana na tulishirikiana naye sana. Tulipopata taarifa kwamba amefariki dunia, kwa kweli tulisikitika sana. Naomba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Siha, niseme kwamba tunamwombea Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua pia kwamba hawa Wabunge wenzetu mbalimbali humu ndani wamepoteza jamaa zao na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu pia ningependa nichukue nafasi hii kutoa pole kwa wote kabisa wale ambao wameondokewa na jamaa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ninapozungumzia jambo hili, nisingependa kupoteza mwelekeo, inahusiana pia na Katiba. Tumetoka katika chaguzi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wananchi wa Jimbo langu la Siha walifanya kazi kubwa katika kuwachagua Wenyeviti wa Vitongoji na Wenyeviti wa Vijiji. Kwa asilimia 99 walichagua Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Ni wajibu wangu kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Siha na kuwaambia ahsante kwa kazi nzuri walioifanya. Ninachoweza kuwaambia wananchi wa Jimbo la Siha ni kwamba nitajitahidi kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia niweze kuona kwamba ninapigania maslahi yao ndani ya Bunge na nje ya Bunge. Ninawashukuru sana na ninawapongeza sana kwa kuchagua Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaozungumza mwisho mwisho, tunapata matatizo kwa sababu maeneo mengi yameshazunguziwa. Nataka nijielekeze katika yale maeneo ambayo hayajazungumziwa. Natamka kwamba kwa taratibu ambazo zimeelezwa na Mheshimiwa Bakari Mwapachu, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba na utaratibu mzima uliotumika katika kuhakikisha kwamba mawazo ya wananchi yanaingizwa katika Katiba hii na mabadiliko haya nayaafiki na kwa msingi huo natamka hapa kwamba mimi mabadiliko haya nayaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda katika maeneo ambayo nilikuwa na wasi wasi kwamba yanaweza yakaondolewa. La kwanza, kuacha maneno ujamaa ndani ya Katiba ni kitendo cha kunifanya mimi niunge mkono moja kwa moja jambo hili tunalolizungumza. Hilo la kwanza na hili nataka nilielezee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyoangalia ile ibara ya tatu hapa, ambayo inasema, "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa;" Narudia tena, "ni ya kijamaa, yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa"; Mimi nikasema habari hii imekwisha. Mheshimiwa Mwapachu, akiondoa kitu kinachoitwa ujamaa ndani ya Katiba hii, watu watakufa katika nchi hii. *(Makofi)*

Ndani ya Katiba hii ukiondoa maneno ujamaa, huzungumzi habari ya ruzuku, huzungumzi habari ya pembejeo; Serikali unaweka mkono wako kule, mikopo kwa vijana, akina mama, huwezi kuzungumza tena. Huwezi ukazungumza habari ya kuondoa kodi ya maendeleo kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Huwezi ukazungumzia mipango mbalimbali ya MES na MEM kama ndani ya Katiba hii huzungumzi habari ya ujamaa. *(Makofi)*

Juzi hapa tumeambiwa *school fees* kwa ajili ya watoto wa shule za msingi, hakuna *school fees* tena ni kwa sababu *reference point* yetu iko ndani ya Katiba ya nchi na kwamba nchi hii ni ya kijamaa. Katika mambo ambayo *we have to be very conservative* habari hiyo, ni kuhakikisha maneno haya hayatoki humu ndani. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema hivi siyo kwamba nasema, unajua tulipokwenda huku tukaingia katika mambo haya ya soko huria, tumekosea. No! Natambua kabisa kwamba kuna nafasi yake. Watu wengine tunajenga ubepari katika nchi hii. Upebari haujengwi hivi. Ubepari haujengwi kwa jembe la mkono. Marx alipokuwa anazungumzia habari ya Uingereza kuwa nchi ya kwanza ambayo ita-*socialize* alikuwa anaangalia *the industrial society* ile ya Uingereza. Ndiyo aliyokuwa anaangalia. Alikuwa anaangalia mitambo ya kutoa mitambo. Alikuwa haangalii habari hii ya majembe. Hawa watu wanachukua mbegu wanatupa hivi! Unasema kwamba sisi tujenge ubepari hapa, haujengwi hivi. *(Makofi)*

Kwa hiyo sisi tusifikiri kwamba mbona huyu anataka kuleta mawazo ya kijamaa, yanatoka wapi? Ujamaa haujengwi hivi, wala ubepari haujengwi hivi! Hapa kuna mwelekeo na mawazo tu, kuna msimamo tu, kuna mawazo yanaangalia! Tunafikiria kwamba sisi *framework* ambayo tutafanyia kazi ni ya kijamaa. Hilo la kwanza, likanifanya niseme kwamba jambo hili naliunga mkono. Ukiondoa maneno ya ujamaa utapata matatizo makubwa sana.

Katiba ni jambo la kihistoria, ndiyo maana nimesimama hapa. *You need a lot of luck* kupata nafasi ya kujadili. Katiba ni roho ya nchi, ni picha ya nchi, ni namna ya watu wanavyoishi katika nchi. Ukianza ku-*temper* na Katiba, unawekea mambo ya ajabu ajabu huitii, unafika mahali unaitupa pembeni unaiacha ndiyo unazaa mafashisti na ndiyo unapata madikteta. Ndiyo unawapata akina Shaa wa Iran, ndiyo unapata akina Iddi Amin, akina Samoza kwa sababu hawakuheshimu. Ukisikia Rwanda, Darfur, Somalia wanapata matatizo, ni kwa sababu Katiba haikuheshimiwa, imetupwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili jambo ambalo tunalizungumza hapa si jambo ambalo tunaweza tukasema kiutani utani oh, unajua ni vitu vya ajabu. Watu wastaarabu wanafanya hivi tulivyofanya. *White Paper* ilikuwa ni shughuli ya Serikali. Ingeratibiwa na nani? Nani angesimamia? Nani angepeleka kwa wananchi? Mimi nakumbuka nilikuwa *District Commissioner* wakati akina Mudhihir wanakuja pale, ninakasema barabara. Hii ilikuwa ni shughuli ya Serikali inasimamiwa na Serikali inapelekwa kwa wananchi kwa kuratibu maoni ya wananchi. Ungefanyaje? Huna njia nyingine! Ungetoka tu unasema wape *NGO* waende wakatangaze*, it was proper.* Hapa Katiba unazungumzia *management* na *administration, politics* na *economics* za nchi.

Hapa Tanzania tuko watu milioni 35. Kama kila mtu anataka apate za kwake, kila mtu ana akili. Lazima kuwepo na *proper channel* itakayoweka mawazo sahihi na iseme huu ndiyo utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni hilo la kwamba ndani yake iwe na ujamaa. Mimi nilitaka lifahamike kwamba ni sawasawa kabisa.

La pili, sikusikia humu ndani *contemporarily.* Sasa hivi katika Afrika ukisikia watu wanazungumzia kubadili Katiba ni kwa ajili kuongeza kipindi cha Rais aende kipindi cha tatu au cha nne. Mimi huku sikusikia, wewe sikiliza Afrika nzima watazungumzia mambo yanayoitwa *Third Term (TT)*. Hapa kwetu kwa sababu ya

ustaarabu wa kuheshimu Katiba ya nchi hujasikia hapa wanazungumza, la sivyo ingekuwa sokomoko hapa. Watu wangejaa nje huko wanasema sasa wanataka kuongeza Katiba, wanasema Rais ni mzuri, kwa hiyo anafaa, tunataka tumuongezee kipindi, ndio mambo yanayozungumzwa katika Afrika. Lakini hapa sijasikia.

Maana yake ni kwamba amemaliza miaka yake mitano, ameweka mingine mitano, kipindi kimeisha. Mzee ahsante baba kwa kazi nzuri uliyotufanyia tumtafute Mtanzania mwingine ambaye anaweza kufanya kazi hii, mnaendelea. Huu ndio ustaarabu. Ooh tumeona damu itamwagika, wakimbizi; Wakimbizi huwa hawabebi mabegi waakaaga wake zao wakachukua na sabuni, dawa ya meno; Wakimbizi wanakimbia tu mnakwenda mnapotezana na watoto, mke na kila kitu. Tuombee nchi hii iwe ya amani jamani, hapa ndio kimbilio la Afrika, hapa ndipo watu wanapokimbilia.

Kwa hiyo mimi nataka kusema kwamba utaratibu huu tunaokwenda nao ni mzuri. Katiba inataka tuvumiliane, Katiba lazima ikiri iseme kwamba *okay* tunahitaji mawazo ya watu wengi, Vyama Vingi vinaingia lakini *tolerance* ni muhimu.

La tatu, tumezungumzia habari ya akina mama kuongezewa asilimia thelathini. Mimi ninasema ni sahihi kabisa. Nilikwenda Ujerumani ya Mashariki ya GDR ya akina Erick Honica wakaniuliza kwa nini nyinyi kule kwenu mna UWT. Nikawaambia UWT ni *movement* ambayo inatetea maslahi ya akina mama. Wakasema ninyi si mmepata uhuru mwaka 1961 hiyo haiku-*take care!* Wanasema sisi hapa Ujerumani ya Mashariki wakati ule *we had a feeling* kwamba sisi wanawake tuna *right* zaidi kuliko wanaume. Wanasema ukileta *revolution* inabeba makundi yote humo ndani yake. Soma *Essays or Socialism* ya Mwalimu Ukurasa (60). Dosari mbili anazizungumza. Moja anazungumza kwamba hali yetu ya uchumi *technology* yetu ilikuwa ya hali ya chini, lakini la pili anasema wanawake walidharauliwa katika jamii yetu ya Kiafrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechukua muda sana kukifanya kitu tunachokifanya leo. *South Africa,* wame-*fight apartheid* wale akina mama Mandela wote wanapambana. Ule uhuru uliopatikana pale na mapinduzi yanayokuja pale yanatakiwa yabebe makundi yote na yote yanufaike na kupata maslahi. Sisi leo hapa unasema mpaka uje ukatafute upendeleo wa Kikatiba humu ndani tuwaingize akina mama. Akina mama wapewe nafasi yao, hii nafasi ni sahihi kabisa kuwapa na tena tumechelewa sana kufanya hivyo. *Problem* yangu ni jinsi gani wanapatikana; tunawapata vipi hawa akina mama? Hiyo ndio *problem.* Chama cha Mapinduzi siyo kwamba ninakipendelea kwa sababu ni Chama changu kimejitahidi, walau wana hiyo *democratic process*.

Huko *South Africa* na hao Wajerumani niliyokuwa nawazungumza, hawamchukui mtu tu kwa sababu ni mwana mama, awe ni mwana mama mwenye uwezo! Unasema mwana mama huyo aende aka-*compete* aingie kwenye tanuru pale tumuangalie. Unampata mwana mama unajua huyo barabara anajua, mambo mengi anajua, utandawazi na dunia inavyokwenda, unamchukua huyu. Siyo tunachukuana tu hivi hivi, kwa sababu tutajazana humu ndani unakuja hapa unasema tu huyu tumemwangalia. Sasa utaangalia vigezo vya namna gani? Ni ndugu yako, rafiki au ni nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kwamba ndani ya Katiba hii tuweke pia maelekezo yanayosema kwamba hata Chama kikituletea mtu, apitie kwanza kwenye *democratic process* siyo tu tuchukuane hivi hivi. Kama mimi nakaa hapa najua kwamba mwaka 2005 nitakuja tu, nina haja gani ya kuwajibika kwa wananchi wa Tanzania? *Obviously* nitakuja tu hata mkifanya nini, mimi nitakuja kwa sababu najua watasema Wenyeviti wote na Makatibu wao huu utaratibu wetu lazima uende Bungeni. Utaratibu wa namna hii ambao ndani yake hauna kuwajibika hautusaidii sana kwamba ni *automatic* nitakuja humu ndani.

Mimi hapa nahangaika nakimbia usiku na mchana kwa ajili ya Wananchi wa Siha kwa sababu najua nikifanya mchezo hapa watanitupa nje, wataniambia wewe hautufai. Kwa hiyo, ni lazima hili litamkwe ndani ya Katiba, iseme sawa. Lile Baraza la Ushauri la Rais tunalolisema hapa lazima tuliangalie. Mimi ninaishukuru Serikali, imepata tu mawazo ya wadau kabla hata hatujaingia humu ndani wadau tu. Hii ni *credit* kwa Serikali. Serikali inasikiliza mawazo ya watu inaambiwa Baraza la Ushauri halina maana, halitatusaidia, inafika mahali inasema, basi tumeliacha jambo hili. *Congratulation* Serikali. Serikali ikifanya vizuri unaiambia hongera kwa kufanya vizuri.

Ushauri ni jambo linaloletwa kwa mtu ili afikie uamuzi mzuri. Ukimpa ushauri ule akaenda aka-*mess-up* na ushauri ule *you hold him responsible,* huwezi kusema, unajua hii Dr. Asha-Rose Migiro ndiye aliyenishauri. *No way!* Huwezi kusema alinishauri, kwa sababu maamuzi yale ni ya kwako. Wewe ume-*mess-up* na hao watu waliokuja hapa eti ukasema utapata matatizo makubwa sana. Tumwache Rais atafute watu wake wa kumshauri aamue yeye mwenyewe, aseme watu wa kunishauri ni hawa na hawa. Akinifuata mimi Mwanri Mbunge wa Siha, nakuomba ushauri wako nasema naam Bwana mkubwa mimi nitakuja kwa moyo mkunjufu, nimpe ushauri. Akifikiri Imamu atampa ushauri mzuri au Askofu amwite ampe ushauri, sawa. Tusimwambie aah, unajua tunataka wewe uwe na Baraza la Ushauri! Hawa wameondoka na tulipoleta wengine wapya labda tumetaka tupate watu wenye mtazamo tofauti na ule uliokuwepo. Sasa tena kama humu humu ndio wanaingia na walioko kwenye Katiba, *it is a problem.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *it is my opinion* kwamba hakuna haja kabisa. Umesema mimi nimeli-*discuss* kwa sababu umesema limeahirishwa, linapoahirishwa maana yake litarudi tena. Usirudishe! Hii usirudishe kabisa! *(Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lile la Tume, suala la kusema ooh, unajua ukiingiza hao watu wawili sasa inaonekana unaingiza *politics* katika Tume; utafanyeje sasa? Wenzako wanasema kule Zanzibar wameridhika na mambo ni mazuri kwa sababu hapa nimezungumzia *management* ya *politics* na *economics* ya nchi hii. Kama kwa kuweka hao watu ndio utawaondoa *doughting,* Thomas' utawaweka kule ndani watakuwa na hakika walau mashaka yatakwishawaweka. Kwa sababu pale unachofanya ni kwamba una-*manage politics*.

Thomas alikuwa hakuamini kwamba Yesu alifufuka akasema mpaka nitakapoona mikono yake na alikuwa ni mteule wa *Jesus Christ. Jesus Christ.* Nyinyi Waislam mnamwita Nabii Issa, akanyoosha mikono yake akaonyesha kule kwenye vidonda

kuonyesha vidole vyake ili ku-*prove* kwamba kweli amefufuka, kwa sababu alikuwa haamini. Sasa kama watu wanafanya kwenda pale kukaa kama mawakala, wawe na hakika kinachofanyika pale na wana-*sight.*

Mfano katika nchi hii Zanzibar walivyofanya ni vizuri, *it is my opinion* kwamba kwa kufanya hivyo una-*manage politics* siyo kwamba unalifanya lile jambo liwe la kisiasa. Unachofanya pale ni kwamba unalipa *management*. Hao wakikaa kule wanaridhika wanajua kwamba na sisi tutaangalia maslahi yetu, watatoa ushuhuda waache wakae. Kama ikishindana mbele ya safari tutasema badilisha utaratibu. *It is neither static nor final.* Mimi ninasema kwamba Serikali ni sahihi. Narudia tena kusema kwamba naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika Muswada huu wa Mabadiliko ya Katiba. Kwanza ningependa niseme moja kwa moja kwamba naunga mkono hoja hii. Lakini kabla sijaanza kuchangia, ningeomba nitoe salamu zangu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Frank M. Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki na Mwenyezi Mungu amjalie maisha mema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa nilizungumzie ni juu ya dhana ya upendeleo kwa wanawake kupata Wabunge asilimia zaidi ya thelathini kwa jinsi ambavyo imeletwa katika Muswada.Dhana hii mimi naiunga mkono kabisa na lazima tuende na dhana hii kwa wakati huu kwa sababu ya hitilafu iliyoko ndani ya jamii kulingana na historia katika mila na desturi zetu kwamba kuna "*prejudices against women".* Kwa hiyo, ni vigumu wao kuweza kushinda vitu vingi kwa kupitia Majimbo ya Uchaguzi. Kwa hiyo kwa wakati huu lazima tutumie njia hii.Wenzetu kwa mfano kama India, ili kufikisha asilimia thelathini kulingana na Azimio la Beijing, wao wamepitisha sheria kwamba kutakuwa na Majimbo ya Uchaguzi ambayo yanakuwa *declared* kwamba ni Majimbo yatakayopiganiwa na wanawake tu. Kwa hiyo wanaume hawaruhusiwi kupigania katika Majimbo hayo ili kuwa na uhakika kwamba wanapatikana. Sasa njia hiyo mimi naiona ni njia mbaya kwa sababu inabagua wanaume, inasimama katika upande wa ubaguzi wa kijinsia. Hiyo inaumiza wanaume. Kwa mfano Jimbo langu linakuwa *declared* ni la wanawake sasa mimi niende wapi? *(Kicheko)*

Kwa hiyo, hiyo njia haifai, lakini hii njia haiumizi mtu. Kuna wazo jipya kwamba pengine ni vyema Jimbo moja liwe la mwanaume mmoja na mwanamke mmoja. Nayo hiyo nafikiri siyo nzuri kwa sababu inaweza ikaleta migongano isiyokuwa na lazima inapofikia wakati wa uwajibikaji. Kunaweza kukawepo na lawama na kila mmoja anamsukumia mwenzake.

Kwa hiyo nasema dhana hii ya Viti Maalum haiumizi na katika *process* hii, jinsi tunavyozidi kwenda na wakina mama wakizidi kugombea, wanazidi kupata Viti vya Majimbo na utafika wakati ambapo itakuwa sasa njia hii ya Viti Maalum ni *redundant*. Itafikia kama wenzetu wa nchi za Scandinavia, Denmark, Sweden unakuta wanawake ni wengi zaidi Bungeni kuliko wanaume. Kwa hiyo ukifika wakati huu, kama ni kizazi kijacho na iwe hivyo. *(Makofi)*

Jambo la pili, ni Tume ya Uchaguzi. Hili suala la kuweka Wawakilishi kutoka Chama Tawala na upande wa Vyama vya Upinzani, mimi hiki kipengele kilicholetwa na Serikali nakipinga kabisa, sioni mantiki yake kabisa kwa sababu tunavuruga maana ya dhana huru ya Tume ya Uchaguzi. Tunapozungumza juu ya Tume Huru ya Uchaguzi, haina maana hii, kwa vile upande wa Zanzibar wameweka utaratibu huu, kwa hiyo anasema tuufuate. Zanzibar ni tatizo lingine. Kulikuwa na matatizo kule ambako ililazimu tuwe na muafaka, sasa kutokana na ule muafaka, kimewekwa kipengele hiki. Ni mtindo wa mpito ili kuweza kurejesha hali ya kuaminiana katika jamii ya wenzetu Wazanzibar. Lakini itafika mahali nao watakuja kuona kwamba hiki kipengele hakina umuhimu tena. Kwa hiyo kwa upande wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hiki kipengele cha kuweka Wanasiasa ndani ya Tume, hakina mantiki yoyote. *(Makofi)*

Unapoweka wanasiasa kwenye Tume una-*politicize* Tume. Ni wazi kwamba kutatokea migogoro isiyoisha. Kama ambavyo wamesema wengine na nimewahi kusema hata mimi mwenyewe humu ndani, inaweza ikafika mahali ambapo inalazimika Tume itangaze nani amechaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kule ndani hawaelewani. Kwa sababu ya migongano. Sasa katika *forces* hizo mbili wata-*influence* na wengine mle ndani. Kwa hiyo watafika mahali wanagawanyika na *especially* kunapokuwa na kura kati ya mshindi na anayefuata tofauti siyo kubwa, mnaweza kukaa muda mrefu hamjampata Rais. Hiki kipengele ni cha hatari kwa kuingiza wanasiasa ndani ya Tume.

Chombo cha Tume ya Uchaguzi siyo chombo cha Uwakilishi. Kwa hiyo lazima kiwe ni chombo ambacho namna ya kufanya maamuzi yake lazima kiwe *cohesive* kisiwe *dynamic.* Kwa hiyo, kuweka hii ni sawa kuweka *virus* ndani ya Tume. *(Makofi)*

Uhuru wa Tume ya Uchaguzi unaipata kwa ku-*entrench* ndani ya sheria, *operations* zake kwamba wao ni huru. Pamoja na kwamba wameteuliwa na Rais, lakini hawaingiliwi na Rais katika utendaji wao, sawa na uhuru wa Mahakama. Rais anateua Majaji, Jaji Mkuu, lakini *operations* za Mahakama Mheshimiwa Rais hana *power* nazo. Kwa sababu kuna sheria ziko *entrenched* ndani ya Katiba na Sheria nyingine ambazo hazimwezeshi Rais kuingia huko tena. Kwa hiyo na Tume hii tuitazame kwa mtazamo huo.

Ukitazama Ibara hiyo ya (74) utakuta huo uhuru unaonekana katika vipengele vya (7)(11), (12) yaani (74) *sub article* (7) (11), (12) vinazungumzia juu ya uhuru wa Tume. Lakini *sub article* (74) (5) inazungumzia jinsi Mjumbe wa Tume anavyoweza kuondolewa kwamba Rais ana *power* naye. Sasa pale tunaweza tukaweka kikwazo kwamba kama anaondolewa, lazima ipitie utaratibu 1, 2, 3 ndipo Rais a-*act* kama vile ambavyo Jaji kama anaondolewa lazima kuna vipengele vyake ambavyo vinamlinda. Kwa hiyo hawezi kuondolewa hivi hivi.

Kwa hiyo mmojawapo ni ile aliyozungumza Mheshimiwa Shellukindo kwamba iwe ni kwamba Wajumbe wa Tume waletwe mbele ya Bunge kwa ajili ya *confirmation*. Hiyo ni kuzidi kuwa-*entrenched*. Lakini suala la kwamba Rais anaweza akashauriana na

Viongozi wa Upinzani pamoja na Viongozi wote juu ya Wajumbe, hilo ni jambo ambalo halina madhara yoyote. Anashauriana juu ya watu *eminent* katika nchi hii wanaoweza wakaingia humo ndani. Halafu baada ya hapo ata-*select* na anaweza akaletwa hapa kuwa *confirmed*. Lakini yeyote anayeteuliwa asijijue kwamba yeye ameteuliwa kwa sababu ya Chama fulani cha Siasa. Ajione yuko huru ili atende haki kulingana na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni juu ya Vyama vya Siasa na Uanachama katika Chama cha Siasa. Kuna jambo moja ambalo naona halijazungumziwa. Ili kuweza kugombea Ubunge, Udiwani na kadhalika lazima uwe mwanachama wa Chama cha Siasa. Lakini ukishachaguliwa unaweza ukafukuzwa kwenye Chama na ukapoteza Ubunge. Sasa hili naliona ni kosa na ni tatizo ambalo linazidi kuwa kubwa. Hii mara nyingi inatokana na migongano ndani ya Chama cha Siasa. Mara nyingi kunakuwa na *aspect* ya kuwepo na *supreme leader* ndani ya Vyama.

Kwa hiyo kunakuwa hakuna demokrasia ya ndani ya Chama. Hawakai kwenye Vikao wakakosoana bila hamaki, hasa kwa *supreme leaders* kukosolewa bila hamaki, hasa inapofikia hapo ndio wengine wanafukuzwa. Sasa kukua kwa Chama cha Siasa chochote kile, ni kule kuwa na uwezo wa kushinda Chaguzi za Vijiji, Mitaa Madiwani ,Wabunge mpaka Rais, ndio kukua kwa Chama. Sasa unapomwondoa Mbunge kwenye Chama, unakidhoofisha Chama na utakuta Chama chochote kilichokomaa, kinalinda Wabunge wake. Hakiwaondoi! Kwa mfano kama Chama cha Mapinduzi hakijawahi kufanya hivyo. *(Makofi)*

Chama cha Mapinduzi kikifanya hivyo basi itaonyesha kuna hitilafu kubwa ndani ya Chama na hilo halijafanywa. Halijafanywa kwa sababu kunakuwa na demokrasia ya ndani kuzungumza na kukosoana bila hamaki mpaka mnafika maafikiano.

Sasa nasema hivi; kuwaondoa Wabunge kutokana na kufukuzwa Chama ni kukiuka Ibara ya (8) ya Katiba ambayo katika Ibara ya (8) (a) na (c) inasema; “Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote. Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii, halafu Serikali itawajibika kwa Wananchi.” Sasa Vyama vinateua Wagombea lakini Wabunge wanachaguliwa na Wananchi, hawachaguliwi na Vyama vya Siasa.

Kwa hiyo kama ni hivyo kwamba Serikali inapata madaraka kutoka kwa wananchi na inawajibika kwa wananchi. Sasa inakuwaje chama cha Siasa kinamwondoa Mbunge aliyechaguliwa na wananchi aliyepata *mandate* ya wananchi? Kinapata wapi uwezo huo baada ya kuwa wananchi wameshafanya maamuzi? Hili ni tatizo ambalo ni lazima tulisahihishe. Wenzetu Kenya wameshalitambua hili la kutengua maamuzi ya wananchi kwamba ni kinyume cha Katiba. Kwa hiyo wao wameweka utaratibu kwamba kama Mbunge yeyote aliyekwishachaguliwa, Mbunge huyo akifukuzwa kwenye Chama chake anabaki kuwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano wa Kenya sitoi mfano wa Marekani. Natoa mfano wa nchi jirani ambao katika *development* ya demokrasia sisi tumewatangulia Wakenya, lakini hilo wao wametutangulia Kwa hiyo na sisi tufanye

hivyo. Basi kama amefukuzwa kwenye Chama, anabaki bila Chama na anandelea kuwa Mbunge. Sasa ikifika hapo italazimu sasa tuanze kufikiria juu ya suala la Mbunge *independent* au *independent candidate.* Lazima hilo eneo tulifikie kutokana na matatizo haya yanayotokea. Vyama vya Siasa lazima viwe *responsible,* viheshimu Katiba na Sheria. Visipofanya hivyo, basi lazima utaratibu uzae *an independent member of Parliament* uanze. Kwa hiyo hiyo inaleta *checks* na *balances* katika Vyama vya Siasa na vile vile sisi Wabunge kama Wabunge wa Bunge hili tunakuwa na *security.* Nimeona nitoe maoni yangu haya na mengine sina tatizo. Utaona nimepinga kabisa suala hilo la Tume ya Uchaguzi, hicho kipengele ndicho nakipinga kabisa lakini vinginevyo naiunga hoja mkono na ninashukuru. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya muhimu sana maana ndio Sheria mama ya nchi. Lakini awali ya yote ningependa kujumuika na wenzangu kutoa rambirambi zangu binafsi mimi mwenyewe na Wananchi wangu wa Musoma Vijijini kwa kifo cha Ndugu yangu Frank aliyetuacha kwa kipindi kifupi kilichopita. Pamoja na hayo ningependa kuungana na wenzangu kwa michango mbalimbali waliyoitoa kuhusu hii Hoja ya Mabadiliko ya Katiba.

Kwa masikitiko makubwa sana ningependa kusema, ingawa tunazungumza juu ya Haki za Binadamu, nikiona Ibara ya (18) (19) mawazo yangu yananipeleka huko Mkoani Mara hususan Wilaya ya Serengeti ambayo tumeona kuna uvunjaji wa haki za binadamu. Tume imekwenda pale imechunguza na kumweka hatiani Mtendaji wa Wilaya ya Serengeti. Huyo mtu mpaka leo bado anapeperusha bendera kuwa *DC* katika nchi ya demokrasia kama ya Tanzania. Lakini leo hapa bado tunazungumza juu ya karatasi kwamba kuna haki za binadamu ziko *guaranteed;* Je, wale wenzetu wa Serengeti tunawaambiaje kama Serikali yetu haisemi chochote kuhusu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana gani kuwa na *guarantee right* ndani ya Katiba lakini wanaovunja bado wanayo madaraka? Mimi nadhani pengine ingekuwa vizuri tuwe makini tunapozungumzia juu ya Haki za Binadamu. Ni kwa maana hiyo ningependa kutoa mchango wangu kuhusu Ibara ya (18), (19), (20) na (30) ingawa najua kabisa ibara ya (30) haikuguswa na mabadiliko hayo. Mchango wangu nimeutoa kwa maandishi lakini nataka kueleza mambo machache pia ambayo nadhani ningependa iingie kwenye *Hansard for record purposes.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeridhia Mikataba fulani kuhusu haki za binadamu. Mikataba hii inatulazimisha sisi Tanzania na nchi nyingine kuwa *comply.* Lazima kabisa tuhakikishe Katiba zetu zinalingana kabisa na Mkataba au *conversion.* Kwa mantiki hiyo, ningependa kabisa Ibara ya (18) isomeke kama ifuatavyo:- “Kila mtu anao uhuru wa kutoa maoni.” Haki hii itajumuisha uhuru wa kuwa na maoni na kupokea na kutoa habari na fikira zake bila kuingiliwa na mamlaka ya Umma na bila kujali mipaka ya nchi. Kwa vile matumizi ya uhuru huu yanaambatana na uwajibikaji, uhuru huu utakuwa chini ya utaratibu, mipaka na adhabu kama inavyoelezwa katika sheria ambazo zimetungwa ama zitatungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni maoni yangu kwamba Ibara hii haitazuia mamlaka ya Serikali katika kuhitaji kuwepo kwa kibali cha kutoa matangazo ya radio na *television.* Pamoja na nyongeza hii ni muhimu kuwepo, kwani katika nchi nyingine kumekuwepo na madai kwamba wanayo haki kupata habari kwa kutoka kwa Vyombo vya Habari bila kulipa angalau leseni. Tusipopanua mipaka ya uhuru huu chini ya Ibara (18) nadhani hapo mbele hatutafika pazuri. Mbali na Ibara ya 18 nadhani, Ibara ya (19) kama ilivyorekebishwa pia ina mapungufu haiko sambamba na Mikataba tuliyoiridhia katika Bunge hili. Tumezunguzia juu ya Mkataba wa *declaration of human right* ya mwaka 1948 ambayo sisi tumeuridhia Mkataba kama huo chini ya Ibara ya (18) na (19).

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini. Pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake, mabadiliko yaliyoletwa mbele yetu yana upungufu kwa kuwa kifungu kidogo cha pili ya Ibara ya (19) kimetoa mwanya wa kuweza kuwabana watu katika uhuru huu ambao ni haki yao. Kwa maana hiyo, ningependekeza tufanye mabadiliko yafuatayo; kila mtu anao uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini. Haki hii inajumuisha uhuru wa kubadili dini au imani na katika jumuiya kutangaza dini au imani yake katika kuabudu pamoja na kufundisha taratibu na desturi za kuabudu. Tukipanua mipaka hii, nadhani matatizo ya dini tunayozungumzia yatapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, huwezi kuwa na haki ndani ya Ibara ya (18) na (19) bila kufanya mabadiliko madogo katika Ibara ya 30. Ibara ya 30 inaondoa kabisa yale yote tuliyotaja katika Ibara ya (18) na (19). Kwa mantiki hiyo ningependa kutoa pendekezo yafuatayo:- Nataka kuboresha tu Ibara ya (18) na (19) haya mapendekezo yasomeke kama ifuatavyo:- Kwa maoni yangu Ibara hii ndogo ya pili ya Ibara 30 ifutwe na badala yake waweke maneno ambayo hayatafanya Serikali ibane watu katika haki ambazo wamepewa ama zipo *guaranteed* chini ya Ibara ya (18) na (19). Nimeeleza na kuyaandika vizuri katika maandishi ili yaweze kusomeka vizuri na wayafanyie kazi. Ningeomba Mheshimiwa Waziri aangalie tena kama kuna uwezekano wa kuboresha Ibara ya 18 na 19 kwa kuzingatia mabadiliko niliyofanya ambayo nayaweka ndani ya Ibara ya 30.

Mwisho kabisa ningependa kugusia jambo la Mwanasheria Mkuu. Mwanasheria Mkuu ama idara ya Mwanasheria Mkuu ina Maofisa wawili wakubwa ambao lazima watambulike kisheria. Naungana kabisa na mabadiliko haya isipokuwa hili Naibu Mwanasheria Mkuu lazima awe Bungeni, maana yake tukiwa na *Attorney General* ndani ya Bunge moja na yeye ni Mbunge pengine akauguliwa ama akaugua, kwa hiyo akiondoka nje hana msaidizi ndani ya Bunge. Sioni kwa nini huyu Naibu wake naye asiwe Bungeni kwa mujibu wa Katiba. Zamani tulikuwa *Solicitor General* mpaka nadhani mwaka 1962.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi ya *Solicitor General* sasa inakaliwa na *Deputy Attorney General,* yeye anafanana kabisa na Naibu Waziri kwa Kazi nadhani. Kwa mantiki hiyo, unaposema *Attorney General* ni lazima pia umuunganishe Naibu wake ashughulikie majambo yote ambayo Mwanasheria Mkuu amepewa na Katiba. Lakini

hawa wanaweza kuvi-*hide* na kuvi-*fight*. Kwa haya machache, nasema naomba kuunga hoja mkono mia kwa mia baada ya kufanya mabadiliko kama haya. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kukushukuru kunipatia nafasi hii na ninaunga mkono Muswada huu asilimia mia kwa mia. Kabla sijaanza kuzungumza na mimi nataka niungane na wenzangu kutoa pole kwa familia na wananchi wa Kasulu Mashariki kufuatia kifo cha Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Frank Michael Mussati. Mungu amlaze mahali pema Peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kabla sijaanza kuzungumzia Muswada huu nataka nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi ya kuisimamia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kweli mafanikio makubwa haya yameonekana. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu sana kwa Taifa letu la Tanzania. Kwa hiyo nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri jana alipowasilisha Muswada huu. Kwa kweli jana alipanda akiwa na nguvu zote tofauti na vile ambavyo tulikuwa tumemzoea. Inaonyesha suala tunalolizungumza sio suala la mchezo na mimi nataka niungane na Wabunge wenzangu wote ambao wameanza kuchangia kwa mawazo yao na mimi nawaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ambacho nataka nizungumze hapa ni kwamba, mafanikio makubwa ya Muswada huu ambao tunaupitisha ni Taifa letu kuendelea kuwa na umoja. Bila umoja mabadiliko haya ya Katiba hayataweza kufanikiwa. Kwa hiyo niitumie nafasi hii kuwaomba Viongozi Wakuu wa Serikali, Watendaji pamoja na Viongozi wa Vyama vya Siasa, kuona umuhimu wa suala hili na tuendeleze umoja na amani katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuwa na umoja katika nchi yetu, hakuna amani wala maendeleo. Kwa hiyo ni vizuri tukawa na mshikamano wa hali ya juu katika nchi yetu ili kuleta mabadiliko makubwa ambayo wananchi wanawategemea. Mimi nitaanza kuchangia ile Ibara ya (19). Mimi haikunitia wasiwasi. Ni kwamba kama ile Ibara ipo na ninataka nimshukuru Mheshimiwa Waziri aliyeitolea ufafanuzi zaidi. Lakini vile vile tukikumbuka Marehemu Baba wa Taifa suala hili alilizungumza kwa uwazi sana na muda mrefu sana, kwamba Tanzania haina dini ila Watanzania ndio wenye dini na alitoa mifano mingi sana na ndio maana tukafikia hapa tulipofikia katika Taifa letu la Tanzania. Pia akatolea mfano kama nchi za Iran. Tunajua kama Irani ina Serikali za kidini na nchi nyingine tofauti. Kwa hivyo kwa wale ambao walikuwa na wasiwasi labda pengine kuwepo kwa Ibara hii inaweza ikaligawa Taifa, haiwezekani hata kidogo! Kwa hivyo namshukuru Mheshimiwa Waziri jana aliliwasilisha vizuri na nashukuru kwamba Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwamba ile hofu iliyokuwepo kwamba labda kuna upande mmoja wa dini ungalikandamizwa, ile imeondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi moja ambalo nimeliona nimeshindwa kuzungumza kwa uwazi ni kwamba, ni kwa nini Zanzibar kuna Kadhi lakini huku Bara hakuna Kadhi. Mimi ningeiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania, ikakaa

ikafikiria mawazo haya na kufungua Ofisi ya Kadhi mara moja huku Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo Ofisi ya Kadhi haisababishi labda kuna hukumu za kidini zitapita, lakini kuna maeneo mawili ambayo ni muhimu sana katika Jamii ya Waislamu, kwa sababu wapo wengine wanaozaliwa nje ya ndoa na kwa mujibu wa ndoa nyingine ili mdhibiti, lazima zikafungwe kwa Kadhi ambapo Kadhi anachukua idhini ya yule mwanamke aliyekuwa anataka kuolewa halafu idhini ile anaitoa kwa Kadhi ili kwa amri yake aolewe na kwa yule ambaye ameidhinishwa kumuozesha. Hili ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili kubwa liko kwenye mirathi, hususani ndoa nyingi za Kiislamu zinamalizikia kwa Makadhi. Kwa hiyo naomba myaone haya masuala mawili msije mkaona labda inawezekana Waislamu wakataka kuweka sheria zao za Kiislamu. Haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanaifahamu Katiba ya nchi na kama hawaifahamu, Zanzibar ina asilimia 95 na zaidi kwamba ni Waislamu, mbona hawajatangaza Serikali ya kidini? Ni kwa sababu Zanzibar ni sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar haiwezi ikafanya mambo yake bila kutii Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kwamba ina Katiba yake ya kufanya masuala yaliyoko Zanzibar. Kwa hiyo Mimi ningeomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuliangalia hili kwa mapana na marefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Lingine, kwa kuwa nchi yetu inakwenda kwenye demokrasia bila hofu, hebu tupangeni mipango turuhusu Wagombea binafsi kwa dhati kabisa. Mimi ninaamini Vyama vitakuwa imara na hapatakuwa na mvutano katika Vyama. Hili naliomba kwa dhati kabisa tuliangalie, tuna hofu gani na kama *system* yetu inaiga mfumo wa Ulaya Magharibi, ipo America. Pamoja na kwamba tunajilazimisha kufuata Marekani, Marekani ipo tangu miaka ya 1977. Sisi tunashindana na mambo yetu toka mwaka 1961 ambaposasa ni miaka arobaini. Lakini ndio wanavyotaka, kwa sababu bahati mbaya kwenye Vyama hivi kuna wasomi wakubwa, mkiamua hili wao wanachotayarisha ni maandamano. Sisi tunajadili Muswada hapa, watu watasema maadamano Dar es Salaam, dhiki kubwa, hatufiki! Lazima tufike wakati tukubaliane na matakwa yao, kama wanasema ni wengi tuache wananchi wawahukumu. Kwa hiyo Serikali ikae iangalie tena juu ya maombi ya kuweka Wagombea binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii bado inastahili kuwepo katika amani ya kutosha, bila hivyo hatufiki. Matokeo yenyewe ni makundi kama haya ambayo yanasababisha kuvuruga nchi, tuiangalie na *Ivory Coast* iko wapi leo? Hamna! Ni nchi ambayo ilikuwa ya mfano katika Afrika, leo imegeuka sehemu mbili Kusini na Kaskazini, Waislamu na Wakristo. Ni watu kama hawa na tumeshindwa kuwadhibiti na mwishowe nazungumza hili, kuna kiongozi mimi nashangaa. Viongozi wa Vyama vya Siasa walipokuja Pemba kuhamasisha lile Daftari la Kuandikisha Wapigakura, wamethubutu kuzungumza kwamba kama tutanyang'anya ushindi, Zanzibar itakuwa Palestina, Zanzibar itakuwa Somalia, Zanzibar itakuwa Cossovo. Jamani tunakwenda wapi? Hawa Palestina hawana Serikali, sisi tuna Serikali tena kinachoshangaza wengine

ni Maprofesa. Ni Maprofesa kabisa tena wanasema wana utaalam wa uchumi, hawafikiri matatizo ya Pemba ambayo wanayo, wataweza vipi kutatua matatizo ya Pemba?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuinusuru nchi hii, ninaiomba sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haya mambo wasiyatazame juu juu tu. Mimi ninataka niendelee katika Ibara hii ya (59) ambayo nitanukuu, Ibara ya (59)(a)(2) inasema kwamba Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa Msaidizi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nashukuru Mheshimiwa Mkono, ameligusia hili na kama liko, hivi ndani Katiba tumelifafanua vipi? Kwa sababu tunaambiwa kwamba Naibu Mwanasheria Mkuu atakuwa ni Msaidizi wa Mwanasheria Mkuu na kazi moja kubwa ambayo tunamwona Mwanasheria amefanya hapa Bungeni ni kutoa ufafanuzi na kuitetea Serikali. Sasa je, huyu Naibu Mwanasheria Mkuu ataingia Bungeni na kama haingii, ni kazi gani ambazo atamsaidia Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali?

Kwa hivyo nashukuru Mheshimiwa Mkono ameligusia, lakini ningeiomba Serikali iliangalie tena kwa mapana kwa mafanikio ya Taifa letu hili kwa sababu itakapofikia Mwanasheria Mkuu hayupo, kuna masuala mengi hapa ya Serikali yeye ndio anayakabili. Kwa hivyo tuangalie ni namna gani na huyu Mwanasheria Mkuu atapata utaalam wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda nilizungumzie ni ibara ya 59(b)(1) inasema, "Kutakuwa na Mkurugenzi wa Mashitaka atakayeteuliwa na Mheshimiwa Rais." Amesema Mkurugenzi huyo atakuwa na uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashitaka yote nchini. Kwa ajili hiyo, atakuwa na mamlaka, ameainisha mambo matatu. Lakini nataka nizungumzie (c) inasema, "Kuingilia kazi kuendesha mashitaka yote ya jinai ambayo hayatafunguliwa kwa mamlaka yoyote."

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala ya kufuta kesi ambayo anafanya Mkurugenzi wa Mashitaka. Masuala haya yanaleta malalamiko kwa nchi. Hili tunaliona vipi uwezo mkubwa aliokuwa Mkurugenzi wa Mashitaka? Tuliangalieni sana suala hili kwa sababu tatizo ni wananchi wetu kutoridhika na maamuzi haya yaliyotoka na tunampa uwezo mkubwa. Kwa hiyo ningeliiomba Serikali tuliangalie hili kwa mapana sana ili kuinusuru jamii kugawanyika ikaonekana labda Serikali inajifanyia tu haya masuala bila mpangilio wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nilizungumze ni hilo la kusema kwamba itakuwepo mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na imeainishwa pale kwamba ni Mahakama ya Tanzania na Mahakama ya Zanzibar. Mimi nataka niwaambie wenzetu watu wa Mahakama kwamba watusaidie kuendesha utawala bora katika nchi yetu Tanzania. Malalamiko mengi sana ya wananchi ni kukosa haki zao katika Mahakama. Kuna kesi ambazo zinawakuta wakubwa au matajiri, zinamalizwa kwa muda mfupi sana na kuna watu wanasota ndani humu karibu mwaka wa saba wako Magerezani, mbona kesi zao haziendi?

Kwa hiyo kama inaonekana kwenye Mahakama kuna haki itapatikana, watekeleze haki kwa mujibu wa Katiba ya nchi inavyosema. Wananchi wana haki zao na moja ni

kuwa huru na tumetembelea baadhi ya Magereza, kuna wananchi wanalalamika kwamba wamebambikiziwa kesi, lakini hakuna Majaji. Kwa hivyo uwezo huo wa kutoa haki, watu wa Mahakama wauone na waweze kuisaidia jamii kuitoa katika matatizo. Watu wengi ni wanyonge, wako Magerezani hawajui hata pa kwenda, hawajui hata wa kuwasimamia. Kwa hivyo mimi ningalisisistiza Serikali ikaliona hilo. Mheshimiwa Waziri wa Sheria tunajua uwezo wake mkubwa, tunajua hekima zake kubwa lakini haki hii ambayo imeonekana ipo kwenye Mahakama, tunaiomba Wizara iisimamie pamoja na Serikali ili haki itendeke katika Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, narudia kuunga mkono Muswada huu asilimia mia kwa mia. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia machache na ninampongeza Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu kwa kuleta mabadiliko haya. Vile vile nimefurahishwa sana kwa kufutwa Baraza la Ushauri kwa sababu ndogo ambazo napenda kuzitaja kwa ajili ya watakaokuja pengine mwaka 2005 au mbele zaidi. Kwamba Rais aliyeko madarakani Zanzibar hakuingizwa na vile vile Waziri Kiongozi pia hakuingizwa na vile vile haikuweka wazi Wajumbe wangapi watatokea Zanzibar. Kwa hivyo mimi nimefurahi sana kwa kufutwa Baraza la Ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya (19) inasema kwamba, "Shughuli za uendeshwaji wa Jumuiya za Kidini itakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi." Serikali haina dini, sawa. Lakini wananchi, watu wake walioitengeneza Serikali wanazo dini zao na suala hili kwa Zanzibar kwa uhakika halikubaliki, kwa sababu Zanzibar ina Serikali na ina watu wengi Waislamu.

Tukipiga mfano, katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani inatolewa marufuku kufungua migahawa yote mchana, tofauti na huku Tanzania Bara. Vile vile kuna Mufti ambaye bajeti yake inatoka kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuna Kadhi Mkuu. Kwa hivyo inakuwa vigumu sheria hii kuwa *applicable* mpaka Zanzibar. Kwa hivyo ningependa Mheshimiwa Waziri awasiliane ili kuondoa migogoro au Baraza la Wawakilishi lijadili suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haitakuwa na dini, sawa sawa tunakubali, lakini mimi ningependa kumnukuu Rais wa Marekani Thomas Jafferson aliwahi kusema kwamba *The Constitution of most of our States assert that, that all power is inherent in the people*, kwamba Katiba za Mataifa yote ya Marekani inasema wazi wazi kwamba nguvu zote ziko kwa nchi. Tuifahamu Katiba tuiheshimu na tuilinde, hatuwezi kuwa kama sisimizi tutakaa kimya tu. Tusiwe tunaiga tu kama alivyosema Mheshimiwa Msindai leo asubuhi, tutafute fikra mpya au kama si hivyo, vile vile leo ilisemwa kwamba tunaashiria kuleta migogoro, tupanue wigo wa mashauriano.

Mheshimiwa Naibu Spika, meli ya demokrasia inaweza kwenda vizuri ikahimili misukosuko yote ya mawimbi na kadhalika lakini itazama pale ambapo wale waliokuwa

humo ndani wakigombana. Hakuna matatizo yoyote katika mabadiliko ikiwa yanaelekea ndiko kuzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi isipokuwa hayo. Nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. Asante.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwa ujumla naiunga mkono ila ningependa kuboresha katika maeneo machache. Eneo mojawapo ni lile la Serikali kutokuwa na dini ila Serikali inaweza tu kujenga mazingira ya watu wake kuwaruhusu kuwa na dini yoyote ile. Hili ni zuri. Lakini pia nilikuwa naomba kuwe na mabadiliko yafuatayo:-

Juma moja ina siku saba, inaanza Jumamosi, Jumapili, Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi siku ya mwisho Ijumaa. Lakini sisi Jumamosi siku ya kwanza ndio *weekend* na Jumapili, wakati ndio siku ya kwanza na siku ya pili; kwa nini isiwe Ijumaa ambayo ndiyo siku ya mwisho iwe ndio *weekend?*

Sasa wanaweza Waislamu wakatuelewa vibaya kwamba tumeweka Jumamosi na Jumapili ili sisi tupate nafasi ya kwenda kusali. Siku ya Ijumaa wenzetu ambao wanasali huwa ni kazi, sasa nilikuwa naomba kuwe na taratibu ya kwamba labda Ijumaa mwisho kazi saa sita ili kuwajengea mazingira Waislamu wakasali, Jumamosi labda saa sita kuwajengea Wasabato wakasali, Jumapili tupumzike kuwajengea mazingira Waroman wakasali, tumemaliza ugomvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Jumamosi na Jumapili ndio siku ya kupumzika wenzetu wanasali, Waislamu Ijumaa, ndio kwanza wiki inaanza. Nadhani nilikuwa naomba kama tunafanya mabadiliko mazuri namna hii, basi vile vile tuwajengee mazingira hawa wenzetu wa dini nyingine wapate nafasi ili ya kuweza kushiriki kwenye dini ili tusionekane kwamba sisi tulio kule juu tunaopanga labda Wakristo ni wengi. Nilikuwa naomba hilo tufanye marekebisho ili twendesawa. *(Makofi)*

Suala lingine ni Mawaziri kuwa Wabunge. Nilikuwa naomba Mawaziri wasiwe miongoni mwa Wabunge, watoke nje ya Wabunge ila waingie humu kuthibitishwa. Maana ukiwa na bahati mbaya ukapakana na Waziri mwenye nguvu jasho litakutoka hata kwenye u-*chancellor* kule unaweza ukawa *messenger* wake. Maana kauli kubwa itakuwa kwa yeye Waziri wa Afya, Waziri wa Ujenzi, wewe utasema nini hauna hata Unaibu, utakachosema wewe nini? Lakini kwenye Wilaya ile tofauti ni ya Majimbo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa katika Kamati ya Katiba, kwa hiyo nisingependa kupoteza muda mrefu kwa Waheshimiwa Wabunge kupitia yale tuliyoyazungumza katika Vikao hivyo. Lakini kwa kuboresha, ningependa kwanza kuchukua nafasi hii kumsifu Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Mwapachu kwa kuleta Muswada na kutujumuisha wengi wetu ambao tunashughulika na mambo ya Sheria na Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetembelea maeneo mengi Tanzania, tumeongea na wadau kadhaa, mawazo yao na maoni yao yameingizwa ndani ya mabadiliko haya nampunguze sana *Sanitor*. Bila kuchelewa mimi nasema Ibara ya (18) ingeweza kuboreka zaidi kama ingesomeka kama ifuatavyo:- Nasema hivi, kwa kuwa maneno machache yametolewa kwenye Ibara ya (18), kama inavyosomeka katika Katiba hii wameyatoa, kwa upande wangu nasema kwa kufanya hivyo unafanya haki za binadamu.

Sasa nilikuwa naomba Mawaziri wasitokane na Wabunge ila waje humu ndani kuthibitishwa. *(Makofi)*

Suala la mwisho ni Tume Huru. Ni kweli kabisa kama wataingia wanasiasa kule hakutakuwa na uhuru. Kwani uhuru unaotajwa hapa ni wa nini? Mimi nadhani uhuru katika utendaji kazi wao, kwa sababu kuna mashindano ya Vyama pale kuingia kwenye Serikali hawa ni waamuzi. Sasa ukiwaingiza kila mtu na Chama chake umewaingiza wanachama kule wa Vyama tofauti, kila mtu atakwenda pale kutetea Chama chake hakutakuwa na uhuru. Asiwe mwanachama wa Chama chochote labda, aingie pale awe wa CCM lakini asiingie kwa sababu ya Chama. Akiingia mtu wa *CUF* kama atachaguliwa lakini sio kwa sababu ya U-*CUF* wake. Lakini wasiingie kule kwa kuwakilisha Vyama haitakuwa wanatenda haki katika uhuru huu.

Suala lingine ni Mbunge akishafukuzwa na Chama chake kwamba aendelee kuwa Mbunge, mimi inanipa mashaka kidogo. Mashaka yangu ni kwamba wananchi walimchagua kwa kumsikiliza vizuri ananadi ilani ya Chama chake. Kilichowashawishi watu ni ilani kwamba, sisi tukipewa wa Chama "A" tutajenga Zahanati, tutakarabati hivi, tutafanya hivi, daraja la Mbwemkuru kufanya hivi, daraja la Kibiti litakuwa hivi kwa kipindi cha miaka fulani itakuwa hivi; watu ikawapendeza wakasema naam! Kwa mtindo huu mimi, wewe, mwingine akasema hapana, mimi wakijenga shule, ninapaka kinyesi, wakasema naam, katika upakaji wa kinyesi mimi ndio ninavyotaka. *(Makofi/Kicheko)*

Mtu kachagua kwa kusikiliza ilani, ikamnogea kupaka kinyesi au kukarabati Zahanati. Sasa katika kupaka kinyesi kule wewe hupaki vizuri, wakikufukuza uwe Mbunge kwa ilani gani? Wewe katika kinyesi hupaki vizuri wamekufukuza kwa sababu si mpakaji mzuri uliwadanganya wananchi kwamba utapaka vinyesi kumbe unategeategea, kwa nini wasikufuze? Wakikufukuza ukiwa Mbunge katika kupaka kinyesi kule utafanya nini? Labda tubadilishe na taratibu kwamba kuwe na malengo ya Kitaifa, Vyama vitueleze mikakati pekee itakayofanya Chama hicho kikipata kufikia lengo lile kiasi kwamba huyo akifukuzwa kwenye Chama bado malengo ni yale yale sasa hupo taabuni, mbinu zake yeye za kutekeleza, labda kufikia malengo yale yale. Lakini ikiwa tunaingia kwa sababu ya ilani ukifukuzwa kwenye Chama wana *weight out,* vinginevyo tubadilishe pia twende zaidi katika kubadilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba marekebisho haya . Kwa maoni yangu ni kwamba yakifanyika, basi hii Katiba itakuwa bora zaidi kwa ninavyoona mimi. Naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kabla ya yote napenda kuwatakia heri ya mwaka mpya wa 2005 Wabunge wenzangu wote na haswa ukiwa mwaka wa Uchaguzi. Nawatakia kila la kheri.

Lakini pia ningependa kutoa pole zangu nyingi sana kwa wananchi wa Kasulu Mashariki kwa kumpoteza Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Frank Mussati, pamoja na wale Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamewapoteza wapenzi wao wa karibu wakiwemo wazazi na wake zao. Lakini napenda kutoa rambirambi kubwa kwa Mheshimiwa Waziri ambaye alikuja Mafia mara tu baada ya siku chache tukampoteza mama mwenzetu Mheshimiwa Arcado Ntagazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ilikuwa hata siku kumi hazikufika yule mama tulikuwa naye Mafia na tukawa tunataniana naye kwa kumwombea kila la kheri ili maradhi yote aliyokujanayo ayaache kwenye Bahari ya Hindi na haswa Bahari ile ya Mafia baada ya kwenda kuona mandhari nzuri ya Hifadhi za Samaki, naye akafurahia sana. Kwa kweli tulishtuka na tulisikitishwa sana na kifo chake. Mungu amlaze mahali pema Peponi na Mungu ampe faraja mwenzetu Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na wale wengine wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi wenzangu wameyaongea na nisingependa kuyarudia, lakini nimesimama kwa ajili ya machache. Nitaomba radhi kama itabidi nirudie na pengine kuongezea ya kwangu ambayo nayaona ipo haja ya kuongezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, si lingine ila ni yale ya kubadili au ya kuongeza idadi za Wabunge Wanawake katika Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano. Mimi naunga mkono kabisa kuongeza ile asilimia 30 na kuingiza kwenye Katiba. Tunajua kwa vyovyote vile baada ya muda tungefikia asilimia 30, lakini kuliweka kwenye Katiba inaonyesha wazi jinsi gani nchi hii inavyowathamini wanawake na kuona kwamba haki za wanawake ni lazima zitambuliwe Kikatiba ambayo ni sheria mama ya nchi yetu.

Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na wale wote waliochangia kuona kwamba hii *percent* iongezwe kabisa kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia mimi naomba tuelewane vizuri na wenzetu wale ambao labda huenda wakawa wanaona hii asilimia 30 imekuwa kama tutakuwa wengi. Bahati mbaya kuna siku moja ilitamkwa humu Bungeni jambo ambalo hata mimi sikuridhia, tamko hilo ni kusema kwamba wanawake tutazidi mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viti Maalum haimaanishi kwamba sisi tunaweza kuwa wengi kiasi hicho cha kufikia wingi wa kuona kwamba tunawameza wenzetu wanaume. Lakini ni nia tu ya kuongeza haki za wanawake na jinsi gani mnavyohitaji mchango wetu katika nchi hii katika kutunga sheria mbalimbali, kuona kwamba tunasimamia Serikali yetu na kushauri Serikali yetu *gender* zote mbili tukiwa pamoja. Kwa hiyo, kwa hilo nasema msiwe na wasiwasi, Ukumbi mpya unajengwa tutakaa wote hakuna atakayekaa kwenye jamvi wala hakuna ambaye atasimama.

Nina hakika isingeweza kusemwa hivyo kama tungekuwa tunajua kwamba hatutakuwa na ukumbi wa kutosha kukaa wanawake asilimia 30 na wale ambao nina hakika tutaendelea kugombea majimbo tutaongezeka. Nina watakia kheri wale wote ambao wana nia ya kwenda kwenye Majimbo kugombea ili tuongezeke idadi yetu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naunga mkono hizi nafasi kumi kutamka wazi kwenye Katiba, kwamba nafasi kumi apewe Mheshimiwa Rais lakini tusisahau kwamba kuna neno moja tunalisahau wakati tukichangia. Imetamkwa wazi kwamba angalau hili neno angalau katika hao kumi, watano wawe wanawake na Baraza la Wawakilishi katika wale watano wawili wawe wanawake, sasa neno angalau lina maana yake. Kwa hiyo, mimi nasema ibaki hivyo hivyo na naomba sana wale wote ambao wanajua kwa nini imewekwa hivyo , nina hakika mnajua, isipokuwa tu hamtaki kukubali.

Maana yake mara nyingi wengine hata kama ukweli upo wazi basi ataupindisha pindisha kwa kuona kwamba tunamwingilia Rais. Hatumwingilii Rais, tumempa nafasi ya kuchagua watu kumi lakini tumempa nafasi pia ya kuchagua watano wanaume na angalau watano wanawake yaani wasipungue. Sasa tunapokuja kwamba baadhi ya Wabunge wamesema basi na vijana, tutasimamana sisi wazee tuseme basi na wazee, watasimama wale warefu watasema basi na warefu na wafupi hapa hatukutamka katika hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuposema kwamba wanawake, wanawake vijana ndani wamo, wanawake walemavu ndani wamo, wanawake wazee ndani wamo. Mfano mzuri umeonyeshwa na Waheshimiwa Wabunge ninyi mtakuwa mashahidi ndani ya Bunge hili, mkisema hakuna vijana mimi nakataa. Kwa sababu nina hakika mnajua kwamba mmeunda Chama cha Wabunge Vijana, wametoka wapi? Tuna Chama cha Wabunge ndani ya Bunge hili, bado Chama cha Wabunge Wazee tu hakijaundwa. Lakini sasa mnapogeuka kusema kwamba ndani ya Bunge hakuna vijana basi watengewe nafasi za vijana, kwa kweli mnajipinga wenyewe au hakuna chama hicho? Mimi nina hakika kipo na mikutano inakutana.

Kwa hiyo, nasema vijana wanaingia katika kila hali, wanaingia kwenye Majimbo, wanaingia kwenye nafasi za wanawake, wanaingia katika kuteuliwa Rais hakuwekewa mipaka ya umri. Kwani unapotafsiri ujana si kwa sura, ujana ni umri kwa hiyo wapo Wabunge wa umri wote ndani ya Bunge hili bila kujali jinsia. Hapa tunatamka wanawake. Kwa hiyo, nasema bado neno wanawake ni maumbile kwa hiyo Rais achague wanawake wasiopungua angalau watano wakiwemo wazee, vijana, wakiwemo wa kila umri hiyo nafasi ibaki hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeomba kuongelea kidogo juu ya suala la Mheshimiwa Waziri Mkuu kukaimu au kushika nafasi ya kiutendaji akiwa Rais na Makamu hayupo. Mimi hili naliunga mkono mia kwa mia kwa sababu fani zao zinafanana, taratibu zao za kazi zinaendana kwa hiyo, hiyo itakuwa ni rahisi kabisa kwa nchi yetu kubakia katika mtiririko wa uhakika wakati Rais na Makamu hayupo basi Mheshimiwa Waziri Mkuu ashike nafasi hiyo.

Lakini naipongeza pia mabadiliko ya Katiba haya pale mahali niliposema kwamba na kusisitiza kwamba nchi yetu Serikali yake itakuwa haina dini ila sisi Wananchi tumekuwa na dini zetu. Hilo ni jambo muafaka kabisa na ni jambo ambalo, nasema linalinda heshima na Uhuru wa Mtanzania na raia safi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa kurudia kusema kwamba sisi bahati nzuri kwenye nafasi za wanawake chama chetu kina taratibu nzuri. Basi tungeomba Serikali iwashawishi, sisi hatukutungiwa Sheria na Serikali jinsi gani ya kuwapata Wabunge Wanawake. Lakini kwa taratibu za Chama tumeweza kutunga taratibu nzuri za kuweza kuwapata Wabunge wa Viti Maalum. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iwashawishi na vyama vingine pamoja na kwamba hatujui, lakini tunawaona, tunasikia, nikiambiwa kuleta ushahidi nitakuwa sina, nasema tuwashawishi na wenzetu kuwe na utaratibu ulio wazi wa kuweza kuwapata Wabunge wa Viti Maalum.

Kwa mfano, sisi tuna utaratibu wa kuwakilisha Mikoa, sina hakika kama kweli na wenzetu wa vyama vingine wanao utaratibu wa Viti Maalum kuwakilisha Mikoa. Tunajua hawawezi kupata nafasi hizo zote za Mikoa yote, lakini basi iwe angalau kwa Kanda na kwa hili naweza nikasema ipo dalili ya kuonekana Kanda moja kuna Wabunge wa Kanda hiyo wengi na Kanda nyingine hakuna kabisa. Basi tuone ni njia gani za kusaidiana kuona kwamba wawakilishi hata wa vyama vingine Viti Maalum vinapata wawakilishi kama sio kwa Mikoa basi angalau kwa Kanda zao.

Mwisho kabisa narudia kusema nashukuru kupata nafasi hii na ninarudia kusema nafasi za Wabunge Wanawake asilimia 30 zibaki kama zilivyo, kumi wa kuteuliwa na Rais angalau watano wakiwemo wanawake ibaki kama ilivyo. Baraza la Wawakilishi watano angalau wawili wakiwa wanawake ibaki kama ilivyo na hapa ndio tutakuwa na nafasi nzuri ya kuchangia na kwenda pamoja kwa jinsia zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nashukuru na ninaunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba radhi sauti yangu ni mbaya sana lakini nitajitahidi.

Kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo kuhusu hoja iliyoko mbele yetu. Lakini kabla ya kusema chochote cha ziada nipende tu kutakiana heri na baraka za mwaka huu wa 2005 ambao una shughuli nyingi za Uchaguzi na mengineyo.

Pia naomba kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Frank Mussati, kama walivyosema wenzangu tulikuwa tunakaa naye mstari mmoja na mimi alikuwa ananiita dada. Kwa kweli sikuamini siku hiyo niliposikia kwamba tena ajali imetokea katika maeneo yale yale ya Morogoro.

Pia natoa rambirambi kwa Waheshimiwa waliofiwa na wazazi wao akiwepo Mheshimiwa Daniel Yona na Mheshimiwa Parmukh Hoogan, zaidi pia kwa wale ambao wamefiwa na wake zao, kwa sababu mke anakuwa ndio kiungo cha karibu hasa katika wakati wa matatizo nao ni Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Benito Malangalila. Kwa wote hawa Marehemu naomba Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu tangu mwanzo kwamba mimi naiunga hoja hii mkono ila katika kuiunga mkono basi kuna sehemu chache chache ambazo labda nitatoa ushauri au nitaomba ufafanuzi wa ziada. Kwanza kabisa nakubaliana na Serikali kwa kujaribu kuangalia suala la kuongeza idadi ya Wabunge wanawake ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Serikali imeona ukweli wa kihistoria kwamba wanawake kama wanawake dunia nzima hii walikuwa ni watu wa kudharauliwa, watu wa kubaguliwa kwamba hawana uwezo. Lakini Serikali yetu imeuona ukweli huo pamoja na kushirikiana na nchi zingine kama *SADC* ambapo walitoa maamuzi kwamba hapana sasa wakati umefika wanawake hawa tukiwapa tu nafasi, kwa kweli wameonyesha kwamba wana uwezo kiuongozi, kiutoaji ushauri na kusimamia madaraka wanayopewa sambasamba na wanaume na wakati mwingine hata zaidi ya wanaume.

Kwa hiyo, hili nalishukuru ni mwanzo mzuri na iishie kufikia hata 50% kwa kufikia taratibu zingine lakini si lazima kuwe na Viti Maalum. Kwa uamuzi huu mimi ninasema Tanzania imejijengea uaminifu wa utekelezaji wa maamuzi kadha wa kadha ya Mikataba ambayo inasaini huko nje tunapowaomba au tunapowatuma wenzetu Mawaziri kwenda kutuwakilisha. Lakini pamoja na kukubaliana na wingi huu na kwamba marekebisho yameeleza kwamba lazima pawe na mfumo mzuri wa kuwapata Wabunge hawa.

Mimi nashauri mfumo huo uwe mzuri tena mzuri kwa vyama vyote vya siasa ambavyo vitasimamisha wagombea au ambavyo vitateuwa wagombea akina mama kwamba uchambuzi wa wagombea hao ufanyike ndani ya Vyama vyao kwa kufuata taratibu na Vikao husika vya Vyama hivyo ili hatima yake uchambuzi huo wa makini mapendekezo yaweze kupelekwa kwenye Tume hiyo ya Uchaguzi, ili pia kuweza kurahisishia Tume ya Uchaguzi kufanya uteuzi wa mwisho wa kuwatanga Wabunge hao kihalali zaidi.

Wenzangu wamezungumzia kwa *experience* ya Chama Cha Mapinduzi. Mimi nashukuru sana kwamba kwa kweli kuna utaratibu wa kuchujwa tangu huko pamoja na kwamba tunasema upendeleo hapana. Ndani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kweli hakuna kuteuliwa ndani ya Viti Maalum, isipokuwa tu Rais, tunachaguana kabisa na kuna kuchujana kikamilifu kwa kugombea mnakuwa saba mnaishia mmoja, mnakuwa 80 mnaishia kuwa 13 ni kwa kuchuana. Kwa hiyo, hilo nalo la kusema ni upendeleo kwetu sisi kwa Chama Cha Mapinduzi kuna utaratibu ulio mzuri. Kwa hiyo, labda aliyetangulia kuzungumza kwamba sasa basi Serikali iweke mfumo *uniform* kwa Vyama vyote jinsi

ya kuwapata Wabunge wa Viti Maalum. Madaraka hayo yasiachwe tu katika Vyama ndipo hapo ambapo tunaweza tukaleta vitu tofauti ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono suala Baraza la Ushauri kuondolewa ndani ya Katiba. Kama wenzangu walivyosema, Rais tumwache huru, ana njia nyingi tu za kupata ushauri. Lakini katika kumfunga kama wenzangu walivyosema, hivi ikiondokea kwamba Marais wa nyuma labda mtu hakupatana nao sawasawa tunategemea nini hapo, hata inawezekana wa itikadi tofauti itawezekana kuwa kitu gani hapo? Kwa hiyo, tumwache huru kama wengine walivyosema ili aweze kufanya kazi zake kama ambavyo tutakuwa tumemkubalia ndani ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nitakalolizungumza sasa hivi labda linaweza likawa nje ya mapendekezo yaliyomo au ambayo yanapaswa kuyaweka. Lakini naomba iwe akiba ya baadaye kama wenzangu walivyosema. Mimi nashauri kabisa na naungana mkono na Kamati iliyoleta maelezo haya mbele yetu jana kwamba katika kushauriana na wadau mbalimbali huko walikopita, Kamati ilipata mawazo ilipata maelekezo, ilipata maombi kwamba pawe na uwezekano wa kuongeza uwakilishi wa watu wenye ulemavu ndani ya Bunge. Ama kujumlisha tu kwamba pawe na uwakilishi wa makundi mbalimbali ya jamii ndani ya Bunge, sasa mimi nazungumzia zaidi la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye ulemavu ni kama wanawake kihistoria, ni kama walivyokuwa wanawake kihistoria hawatambuliki, hawaonekani kwamba wana uwezo lakini niseme kabisa kwamba wana uwezo wakipewa nafasi. Kwa hiyo, pana haja kwa Serikali kufikiria, kuona uwezekano wa kuongeza uwakilishi wa watu wenye ulemavu ndani ya Bunge na vyombo vingine vya maamuzi kwa sababu tukichukulia mahesabu ya *UNO.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wao wanasema kwamba nchi yoyote ile idadi ya watu wenye ulemavu ni asilimia kumi ya idadi ya watu wote walioko katika nchi ile. Sisi tulikuwa na sensa hapa nadhani jumla tuko kama milioni 34. Sasa hiyo ukiiweka katika kumi ni wengi hawa milioni tatu *point* kitu na kundi lenye watu wenye matatizo maalum mengi tu, sasa tukijumlishwa jumlishwa hivi inakuwa wakati mwingine vigumu kuweza kuyasema yale ambayo yangeweza kusemwa na kuweza kupangiliwa ndani ya mipango mbalimbali ya nchi yetu.

Kwa hiyo, nilikuwa natoa ushauri hii iwe ni akiba wakati utafika, huku tunavunja Viti Maalum ili kila mtu aende Jimboni, basi ndio hapo hapo tuingize upendeleo maalum kwa watu wenye ulemavu. Kwa sababu wao *its all the same* kwamba hawawezi kupita Majimboni, labda sijui kwa bahati ya namna gani kwa sababu gani ya kujengeka kwa imani na taratibu zetu kwamba watu wenye ulemavu wa aina fulani hawana uwezo.

Lakini kwa kweli mimi nasema wana uwezo hebu wapewe nafasi, si vibaya kuiga kama Uganda, si vibaya kama Afrika ya Kusini na si vibaya kuunda muundo wetu wenyewe tunavyoona unafaa lakini ingependeza watu hawa waweze kuongezwa.

Baada ya kusema hilo mimi ningeomba tu ukurasa wa tano nadhani wa Muswada huu tunaourekebisha huu, kisehemu cha nne kinachosema: "Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kulazimika kujiunga na Chama." walivyosema. Huko sina matatizo. Lakini hii ya "itikadi au falsafa ya Chama hicho" naomba ufafanuzi hasa falsafa hii mtu utaijuaje kwamba hapa ndio inabidi iwe ni marufuku? Ningeomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba hili la watu wenye ulemavu wakati umefika hata na dunia sasa inawatambua na Tanzania basi tuweze kuona wanatambulika vipi. Mimi ninashukuru ndani ya Chama Cha Mapinduzi, UWT ilikuwa na busara tu kwamba tumbukiza mmoja vinginevyo asingekuwepo humu hata mmoja. Sasa hiyo isiwe tu kwa Chama fulani kwa sababu tu ya busara zake, iwe ni mfumo wa Kitaifa kwamba watu hawa lazima waingie watetee wawawakilishe wenzao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema narudia kusema tena kwamba naunga mkono hoja. Ahsanteni. *(Makofi)*

**MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niwe ni miongoni mwa wale wanaochangia Muswada huu wa marekebisho ya Katiba.

Kwanza kama ilivyo kawaida yetu, panapotokea msiba au mambo ya aina yoyote ya kutokufurahisha basi hutanguliza maelezo yetu kwenye sehemu hiyo na mimi nawapa pole wale wote waliofiwa, pia na wafiwa wote nawapa pole kwa kufiwa na mpendwa Mbunge wetu ambaye ameshatangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo hayo nadhani maelezo yangu ya kuchangia Muswada huu yatahusiana zaidi na Ibara ya 37 pamoja na Ibara ambayo kwa bahati imeondolewa kwenye yale maelezo ya sehemu ya nne ya Baraza la Taifa la Ushauri. Lakini kwa vile Mheshimiwa Waziri alisema hili lilikusudiwa kuletwa kwenye Bunge, dhamiri ipo na Serikali ni sikivu kwa hivyo nikaonea kwamba nalo niligusie. Kwenye hii Ibara ya 37 inahusu Mheshimiwa Waziri Mkuu kushika nafasi ya Urais wakati Rais na Makamu hayupo.

Hii nadhani inatokana na lile wazo la kupanua wigo wa demokrasia ambalo lilikuwemo kwenye *White Paper*. Watanzania walichangia vizuri na wakatoa baadhi ya mapendekezo na sasa nafurahi kuona kwamba Serikali inaanza kuyatekeleza mapendekezo hayo. Sasa huu ushauri wa Ibara ya 37 mimi sina pingamizi nao sana kwa sababu unapanua wigo wa demokrasia na naunga mkono isipokuwa tu nina mambo mawili, matatu.

Kwanza ni tahadhari, pili ni kuitaka Serikali iangalie zaidi suala hili hasa kwa kuangalia kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mujibu wa itifaki zetu za Tanzania anachukua nafasi ya nne ambayo inaweza kumwezesha kushika nafasi hiyo. Kuna mtu ambaye anachukua nafasi ya tatu kiitifaki, lakini bahati mbaya bado hajafikiriwa kuwemo kwenye mlolongo huu. Sijui ni kwa sababu gani lakini inawezekana ni kwa dhana ambayo tulijijengea katika utaratiabu huu wa kubadilisha Katiba, ninaye mkusudia hapa kumtaja ni Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Zanzibar kiitifaki ni mtu wa ngazi ya tatu. Rais wa Jamhuri, Makamu wa Rais halafu anakuja Rais wa Zanzibar. Haitoshi katika kuwaapisha viongozi hawa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaapishwa na Jaji Mkuu, Rais wa Zanzibar naye anaapishwa na Jaji Mkuu, naye ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyojua mimi anaingia ndani ya Baraza la Mawaziri kama Rais sio kama Waziri. Kama nakosea labda Mwanasheria Mkuu au Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba anaweza kunieleza wakati anatoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kuna haja ya kumuingiza Rais wa Zanzibar kwenye mlolongo huu. Unaweza kumuingiza, ukaweka na maelezo kwa sababu kama kuna mawazo kwamba kuna mwaka ambao sidhani kama utatokea Rais wa Zanzibar akawa anatoka Chama cha Upinzani ambayo nafikiri ni dhana hiyo inaleta wasiwasi wa kumuingiza Rais wa Zanzibar, wanasheria wanazo lugha za kutumia.

Huyu Rais wa Zanzibar anaweza kuingizwa lakini anaweza kushika nafasi hii mradi tu atakuwa anatoka Chama Tawala, hii inawezekana. Kama Rais wa Jamhuri ni CCM kwa hiyo, Rais wa Zanzibar ni CCM hakuna haja ya kumzuia Rais wa Zanzibar kuchukua haki yake hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haki yake kwa sababu Rais wa Zanzibar kama hii Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni raslimali ya Watanzania basi mdau mkubwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar. Kwa maana hiyo mdau mkubwa wa Muungano wetu ni Rais Benjamin Mkapa na Rais Amani Abeid Karume, kwa mawazo yangu. Kwa hiyo, ukasema mtu huyo umtoe kabisa kwenye suala hili, nafikiri humtendei haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa kuna kitu napenda nikieleze kidogo nacho ni suala ambalo linaweza likaletwa hapo baadaye tunaita kutokuelewa au dhana potofu. Mfano Waziri Mkuu ameshika nafasi hii ya Urais wakati Rais na Makamu wa Rais hayupo, yupo Dodoma anataka kumwita Rais wa Zanzibar kwenye kikao fulani, mfano tu, sasa Rais wa Zanzibar pamoja na busara zake zote kama hatakuja kwenye kikao kile ataambiwa amedharau na pia ataambiwa haiheshimu Katiba. Anaweza kuwa na dharura muhimu lakini kwa sababu ile nafasi imeshikwa na Waziri Mkuu na yeye ni Rais wa Zanzibar ana nafasi kubwa zaidi katika itifaki yetu asipohudhuria kikao kile ambacho ataitwa na Waziri Mkuu basi tafsiri itakayotokea ni kwamba Rais wa Zanzibar anadharau na haheshimu Katiba. Hilo nalihofu sana lisije likatokea. Kwa hiyo, nashauri Rais wa Zanzibar naye aingizwe kwenye mlolongo huo kwa lugha yoyote itakayotokea, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba sisi binadamu wakati mwingine tuna chupa mpaka, kwa mambo yetu. Hili nililolitolea mfano la mkutano inawezekana huyo Waziri Mkuu akalifanya makusudi kumtazama huyu mtu atakuja au haji. Hiyo inaitwa kuchupa mpaka, inatokea. Mfano mwingine sijui kama ni Zanzibar au Serikali ya Tanzania Bara lakini kuna wakati kwa tabia ya mwanadamu tu Rais hakuwepo, Makamu wa Rais hayupo, kuna kiongozi akapewa nafasi hii matokeo yake

tukamwona anaanza kuwa na vimulimuli, sijui nani aliyemzuia hili lisitokee, ni tabia ya binadamu kuchupa mpaka. Tabia hizi ndio huo mfano niliozungumza kwa makusudi anaweza akaitisha mkutano katika tabia ya binadamu ya kuchupa mpaka, anaweza kufanya hivyo, matokeo yake yanakuwa sio mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine sitowahi kuuzungumza lakini hata kwenye *Quran* umo wa tabia ya mwanadamu kuchupa mpaka ni kwamba Firauni alijifanya ni Mungu mkubwa wakati ni mwanadamu lakini Mwenyezi Mungu akamtuma Musa akamwambia nenda kwa Firauni kwa sababu amechupa mpaka. Hii ni mifano ambayo ipo duniani na inatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mfupi, nizungumzie lingine ambalo ni hili suala la kuundwa kwa Baraza la Taifa la Ushauri, limeondolewa lakini kwa sababu Mheshimiwa Waziri amesema dhamira ipo na Serikali ni sikivu, nashauri Serikali itafute utaratibu wa maoni zaidi na inawezekana kwa urahisi tu. Mheshimiwa Rais anayo nafasi ya kuwaita wazee hawa akawaambia nakupeni kazi ya kunishauri jinsi ya kuliunda Baraza hili, wanaweza kufanya kazi nzuri sana kwa sababu wana uzoefu wa mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu pia katika kufanya hivyo, naiomba Serikali iangalie pia Ibara ya 125 ya Katiba ambayo inasema: "Kutakuwa na Mahakama Maalum ya Katiba," sijui lini. Kwa hiyo, ili kuiondoa Ibara hiyo ya 125 wafikirie hili Baraza la Ushauri lifanye baadhi ya kazi ambazo zinazungumzwa kwenye Ibara hiyo ya 125 na liwe na sura ya kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Tanzania na kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mambo ya Muungano. Tukifanya hivyo, tutafika mahali ambapo yale ambayo tulikuwa tunaita kero ambapo mimi nimeshaondoka kwenye kero sasa nayaita maudhi jambo hilo halitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo haya, yaliyobakia yote sina pingamizi nayo lakini mawili haya kwanza la Baraza la Ushauri nataka Serikali ifikirie kuliweka kwa utaratibu ule ambao wadau wenzao waliwashauri kwa sababu mwaka huu wadau wenzao wa Muungano walitoa ushauri mzuri kwa mambo haya na yapo Serikalini na nadhani Mwanasheria Mkuu anayajua. Kwa hiyo, wayafikirie yale pamoja na haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayatoa kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu nafasi ya Waziri Mkuu pia liingizwe jina la Rais wa Zanzibar kutokana na umuhimu ambao nimeuzungumza katika mchango wangu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, haya mawili nina *question mark* yaliyobakia yote nayaunga mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona watu wengi wanajiandaa, nadhani kufikia hapo kwa leo tuseme tumefanya kazi ya kutosha. Wale waliobaki na hawa pengine waliokosa leo kuna nafasi ya kesho siku nzima jambo ni hili hili.

Kwa hiyo, kufikia hapo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.09 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa Tarehe 4 Februari, 2004, Saa Tatu Asubuhi)*